

nan, 3000-

UNGAMO

Wazi yangu mwenyewe na kaulimwoko kwa madhuni ya shahada

**ATHARI YA DUKSI KATIKA UFUNZAJI NA UJIFUNZAJI WA  
KISWAHILI: MTAZAMO WA UCHANGANUZI LINGANISHI**

TASNIFU

YA

WENYAA NASABA SALOME

ILİYOTOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA  
KENYATTA

2007

Wenyaa, Nasaba  
*Athari ya duksi  
katika ufunzaji na*




08/322527

**KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine chochote.


  
\_\_\_\_\_

**WENYAA NASABA SALOME**

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu kwa idhini yetu kama wasimamizi

  
\_\_\_\_\_

**PROFESA IRERI MBAABU**

  
\_\_\_\_\_

**DKT. P. MBATHA MATHOOKO**

# TABARUKU

Kwa wapenzi wangu: mume wangu *kuka* Maurice, watoto Sheila, Mercy, Tina, Amy, Sam na Mannu. Kujali kwenu kulinipa ari na moyo wa kupiga hatua zaidi hususan mlima ulipoonekana mgumu kuukwea. Licha ya masaibu, masikitiko na machozi mengi, ushawishi wenu ulinipulizia msukumo wa kuendelea hadi tamati.

## SHUKRANI

Kwanza natoa shukrani zangu kwa Muumba. Kazi hii ni tunda la neema zake Mwenyezi Mungu. Ninawashukuru wasimamizi wangu wa heshima, Profesa Ireri Mbaabu na Dkt. P. Mbatha Mathooko kwa uongozi, ushauri, maoni, na maarifa kando na kunipa moyo wa kuendelea katika kila hatua. Ninawashukuru kwa maelekezo yaliyoniwezesha kufanikisha maandalizi na maandishi ya tasnifu hii.

Siwezi kusahau kuwashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili na lugha za Kiafrika kwa mchango wao. Mwenyekiti wa Idara, Mwalimu Peter Mugambi, Dkt. E. Masinde na Mwalimu E. Mudhune. Mlinichochea kuendelea bila kukata tamaa kila nilipohisi kuiacha kazi hii. Dua langu kwa Mola ni kuwa; *kila mnalolifanya na liweze kukutana na heri.*

Asanteni wasomi wenzangu tuliongo'a nanga pamoja, safari ya kitaaluma. Hakika tulifaana kwa mengi. Masomo na mashauri tuliyobadilishana kando na kuangua vicheko au kupanguzana machozi makali ilipobidi. Tulikuwa marafiki wa kufa kufaana. Tulioneana imani na kuvumiliana kwa yote yaliyotukumba. Tuliposhikwa tulishikamana vilivyoy. Hellen, Kea, Mungai, Nelly, Wachira na Kihara mlinikwamua kila nilipoona giza totoro. Mhazili, shangazi Mary Khaemba, kwako natoa shukurani kwa himizo nzito na za mara kwa mara ulizozitoa nilipoihangaikia na kuisumbukia kazi hii.

Kukamilika kwa kazi hii kulitegemea sana mchango wa watafitiwa walioshirikishwa nyanjani. Walihojiwa na pia walijaza hojaji. Lakini kwa sababu ni muhali kutaja kila

mmoja wao kwa nafasi hii, nimeamua kuwashehenekezea shukrani zangu kwa maoni yenu yaliyokuwa tunu. Asanteni sana.

Katika kutamatisha, ninakuomba upokee shukrani zangu mume wangu mpendwa *Kuka Maurice*. Hakika ulinifadhili. Ulijitolea kwa hali na mali. Kwa yote uliyonifanyia kukulipa siwezi. Ninamwomba Mwenyezi Mungu akunyoshee yote yaliyo mema huku akikuondolea kila chembe la shari. Kwa wanangu wapenzi; Sheila, Mercy, Tina, Amy, Sam na Mannu, ninatamani usomi wa mama wa uzeeni uzidi kuwachochea. Mpate ari na msukumo wa kutaka kusoma zaidi ya mama. Asanteni kwa ustahimilivu wenu mlioonyesha. Aghalabu ilinilazimu kuwanyamazia na kuwawashia taa usiku kucha. Samahani kwa kuwapunguzia starehe zenu muda huo wote. Hata hivyo, ninawahakikishia kuwa kamwe hamtaujutia mchango wenu.

## Ufafanuzi wa Istilahi

- Abjadi* : Herufi za Kiarabu. Zinaweza kuwa irabu au konsonanti.
- Akhlaq* : Mafunzo ya kidini ya Kiislamu yanayozingatia adabu.
- Alama* : Michoro maalum inayoambatanishwa kwa Irabu za Kiarabu ili kuleta au kukamilisha maana ya maneno yanaposomwa na kuandikwa.
- Chuo* : Kituo kinachotoa mafunzo kama vile mafunzo ya kidini ya Duksi.
- Duksi* : Neno la Kiarabu lenye maana ya utaratibu wa elimu ya Kidini ya kimsingi. Inahusu kujifunza na kukariri abjadi inayomwezesha mtu kusoma Korani. Elimu hii hutolewa mapema katika Kiarabu na sambamba na elimu ya shule ya msingi.
- Fiqhi* : Neno la Kiarabu linalomaanisha mafunzo juu ya sheria, masharti na hukumu katika dini ya Kiislamu.
- Hifdhi* : Kuhifadhi. Kulingana na elimu ya Duksi mafunzo yote yalikusudiwa kuhifadhiwa.
- Loh* : Kibao cha kuandikia katika darasa la Duksi. Kinatumika kama kitabu. Watoto huandika hapo.
- Maalim* : Mwalimu anayeendesha mafunzo ya kidini ya Kiislamu. Anaifanya kazi sawa kama Sheikh.

- Madrassa* : Chuo maalum cha kiwango cha juu kinachotoa mafunzo ya kidini ya Kiislamu pamoja na masomo mengine kama vile lugha ya Kiarabu na Hesabu.
- Mfumo wa Lugha:* : Mpangilio wa vipengele vya kisarufi unaoongozwa na Sheria za lugha.
- Sheikh* : Mwalimu wa kidini ya Kiislamu. Anaifanya kazi sawa na Maalim.
- Sira* : Neno la Kiarabu lenye maana ya mafunzo ya Kiislamu yanayohusu maisha ya mitume na manabii.
- Tawahidi* : Mafunzo ya Kiislamu kuhusu sifa za Muumba kama ukuu, uwezo na utukufu.
- \* : **Makala ya kidini yaliyochapishwa bila miaka.**

## IKISIRI

Kazi hii imekusudia kuchanganua athari ya elimu ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa mujibu wa mtazamo wa nadharia ya Uchanganuzi Linganishi. Vipengele vya kisarufi yaani abjadi, maendelezo, msamiati, mtindo wa kuandika, mpangilio wa maneno katika sentensi ndivyo vilivyochunguzwa katika utafiti huu.

Sampuli mseto ndiyo iliyochaguliwa na kuhusishwa. Watafiti walioshirikishwa walitoka katika wilaya ya Garissa, mjini pamoja na viunga vyake. Tajriba, imani, elimu, mielekeo na maoni ya wanajamii wa viwango mbalimbali yalizingatiwa. Kazi hii pia ilizingatia mbinu za kufunzia Kiswahili madhumuni yakiwa ni kuboresha na kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha hii katika mkabala wa mazingira ambapo lugha ya Kiarabu inazingatiwa. Yaani hutumiwa kwa kuendeshea shughuli za kidini.

Kutokana na utafiti huu ilibainika kuwa elimu ya Duksi ina athari chanya na hasi. Mbinu za kufunzia zimedhihirisha njia tofauti tofauti zinazoweza kusaidia kuinua kiwango cha kufunza lugha. Papo hapo kutokana na ukinzano kati ya vipengele vya kisarufi vya (Kiarabu na Kiswahili), imetambulikana kuwa wanafunzi hupata shida zinazohusiana na abjadi, maendelezo, hijai, msamiati na maana ya sentensi.

Utafiti huu umependekeza kuwa bado Kuna haja ya kuendeleza elimu jumuifu ambapo mbinu changamano zinaweza kutumika. Hii ni kwa sababu mafunzo hayo

yote ya kidini na ya kimagharibi yana manufaa kwa maisha ya wanafunzi wakiwa shuleni na hata baada ya masomo shuleni.

1	...	...
2	...	...
3	...	...
4	...	...
5	...	...
6	...	...
7	...	...
8	...	...
9	...	...
10	...	...
11	...	...
12	...	...
13	...	...
14	...	...
15	...	...
16	...	...
17	...	...
18	...	...
19	...	...
20	...	...
21	...	...
22	...	...
23	...	...
24	...	...
25	...	...
26	...	...
27	...	...
28	...	...
29	...	...
30	...	...
31	...	...
32	...	...
33	...	...
34	...	...
35	...	...
36	...	...
37	...	...
38	...	...
39	...	...
40	...	...
41	...	...
42	...	...
43	...	...
44	...	...
45	...	...
46	...	...
47	...	...
48	...	...
49	...	...
50	...	...
51	...	...
52	...	...
53	...	...
54	...	...
55	...	...
56	...	...
57	...	...
58	...	...
59	...	...
60	...	...
61	...	...
62	...	...
63	...	...
64	...	...
65	...	...
66	...	...
67	...	...
68	...	...
69	...	...
70	...	...
71	...	...
72	...	...
73	...	...
74	...	...
75	...	...
76	...	...
77	...	...
78	...	...
79	...	...
80	...	...
81	...	...
82	...	...
83	...	...
84	...	...
85	...	...
86	...	...
87	...	...
88	...	...
89	...	...
90	...	...
91	...	...
92	...	...
93	...	...
94	...	...
95	...	...
96	...	...
97	...	...
98	...	...
99	...	...
100	...	...

## YALIYOMO

Usuli wa Mada.....	Ukurasa
Ungamo.....	i
Tabaruku.....	ii
Shukurani.....	iv
Ufafanuzi wa Istilahi.....	vi
Ikisiri.....	viii
Yaliyomo.....	ix

### **SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**

1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Suala la Utafiti.....	8
1.2 Maswali ya Utafiti.....	10
1.3 Malengo ya Utafiti.....	10
1.4 Nadharia Tete.....	11
1.5 Sababu za Kuchagua Mada.....	11
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	14
1.7.0 Misingi ya Kinadharia.....	15
1.7.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.....	15
1.7.2 Natija ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.....	15
1.7.3 Upungufu wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.....	16
1.7.4 Nadharia ya Lugha Kati.....	16
1.7.5 Mchango wa Nadharia ya Lugha Kati.....	17
1.7.6 Upungufu wa Nadharia ya Lugha Kati.....	17
1.7.7 Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi.....	18
1.7.8 Sababu za Kuchagua Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi.....	22
1.8.0 Udurusu wa Maandishi.....	23
1.9.0 Mbinu za Utafiti.....	28
1.9.1 Sampuli Iliyoshirikishwa.....	29

1.9.2	Ukusanyaji wa Data.....	29
1.9.3	Maktabani.....	29
1.9.4	Nyanjani.....	30
1.9.5	Uchanganuzi wa Data.....	34
1.9.6	Uwasilishaji wa Data.....	36
1.9.7	Hitimisho.....	36
<b>SURA YA PILI: ELIMU YA DUKSI</b>		<b>37</b>
2.0	Utangulizi.....	37
2.1.0	Kijielezi na Maana ya Duksi.....	37
2.1.1	Utaratibu wa Elimu ya Duksi.....	39
2.2.0	Nafasi na Dhima ya Elimu ya Duksi.....	42
2.2.1	Masomo katika Chuo cha Duksi.....	44
2.2.2	Somo la Lugha.....	45
2.2.3	Somo la Hati.....	45
2.2.4	Maendelezo ya Kiarabu.....	46
2.2.5	Somo la Kidini.....	48
2.2.6	Somo la Maadili.....	49
2.2.7	Somo la Hesabu.....	50
2.3.0	Mbinu za Kufunzia katika Chuo cha Duksi.....	50
2.4.0	Hitimisho.....	54
<b>SURA YA TATU : LUGHA YA KISWAHILI NA YA KIARABU</b>		<b>55</b>
3.0	Utangulizi.....	55
3.1.0	Lugha ya Pili, Kiswahili.....	56
3.1.2	Abjadi za Kiswahili.....	56
3.1.3	Fonimu za Kiswahili.....	59
3.1.4	Muundo wa Silabi.....	64
3.1.5	Mtindo wa Kuandika.....	67
3.1.6	Maendelezo na Hati.....	67
3.1.7	Mbinu za Kufunzia.....	69
3.2.0	Lugha ya Kiarabu.....	81
3.2.1	Abjadi za Lugha ya Kiarabu.....	82

3.2.2	Kipengele cha Maendelezo.....	84
3.2.3	Kipengele cha Msamiati.....	84
3.2.4	Kipengele cha Matamshi.....	88
3.2.5	Kipengele cha Utunzi wa Vifungu.....	89
3.2.6	Mbinu za Kufunzia Lugha ya Kiarabu.....	90
3.3.0	Ulinganifu kati ya Lugha Husika.....	91
3.4.0	Hitimisho.....	93

## **SURA YA NNE: ATHARI YA DUKSI KATIKA UFUNZAJI**

### **NA UJIIFUNZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI**

4.0	Utangulizi.....	95
4.1.0	Uchanganuzi wa Kazi za Darasani.....	96
4.1.1.	Vipengele vya Kisarufi.....	96
4.1.2	Kipengele cha Sauti.....	97
4.1.3	Kipengele cha Abjadi.....	97
4.1.4	Kipengele cha Maendelezo.....	98
4.1.5	Utunzi wa Sentensi.....	100
4.1.6.	Athari ya Elimu ya Duksi.....	102
4.1.7	Mbinu za Kufunzia.....	105
4.1.8	Athari Hasi ya Elimu ya Duksi.....	106
4.2.0	Fasiri ya Hojaji na Majibu ya Mahojiano.....	109
4.3.0	Hitimisho.....	113

## **SURA YA TANO: HITIMISHO**

5.0	Utangulizi.....	114
5.1.1	Muhtasari wa Utafiti.....	116
5.1.2	Mahitimisho ya Utafiti.....	119

5.1.3	Mapendekezo.....	126
	MAREJELEO.....	134
	KIAMBATISHO 1: Hojaji ya Walimu na Maafisa wa Elimu.....	137
	KIAMBATISHO 2: Hojaji ya Wanafunzi.....	139
	KIAMBATISHO 3: Maswali ya Mahojiano.....	140
	KIAMBATISHO 4: Zoezi la Imla la Wanafunzi.....	141
	KIAMBATISHO 5: Picha za Darasa la Duksi.....	142

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Duksi ni elimu ya kidini. Ni elimu ya kimsingi na kongwe miongoni mwa wanajamii wa dini ya Kiislamu wanaoishi katika mkoa wa Kaskazini Mashariki. Baadhi ya jamii husika ni kama Wasamburu, Waborana, Wasomali, Warendille na Waghala. Kinyume na hayo, katika mikoa mingine nchini mafunzo yayo hayo hushughulikiwa lakini kwa jina la kijumla la *madrassa*.

Elimu hii huwa inatolewa kwa utaratibu maalum na wa kipekee. Mafunzo juu ya abjadi za Kiarabu hutiliwa mkazo ili watoto wapate uwezo wa kujua, kutambua, kukariri na baadaye kumudu usomaji wa Korani kama inavyostahiki. Kila mtoto anapaswa kuanza kujifunza mara tu anapopata uwezo wa kuongea. Masomo hayo huendeshwa kwa lugha ya Kiarabu huku ufafanuzi ukifanywa kwa lugha ya kwanza. Maandishi pamoja na hati inayotumiwa ni ile ya asilia, ya Kiarabu. Kwa muda mrefu Korani haikuruhusiwa kutafsiriwa kutoka kwa lugha asilia kutokana na hofu ya kupoteza maana asilia.

Elimu hii inathaminiwa na wanajamii kiasi cha kuwafanya kuwalazimisha watoto kusoma mafunzo yote yanayofunzwa. Wazazi, hutarajia watoto kushika na kufuata mambo yote wanayofunzwa. Ni lazima watoto wahitimu katika mafunzo ya Duksi kabla ya kujiunga na Madrassa. Elimu hiyo hutolewa na walimu wa kidini

wanaoitwa maalim au Sheikh. Ufunzaji na ujifunzaji unaweza kufanywa nyumbani au katika vituo maalum vinavyotunzwa na viongozi wa kidini ya Kiislamu (Kwa mfano msikitini). Watoto wanapokea mafunzo kutoka nyumbani wazazi wao huwalipa walimu kibinafsi. Wanajamii pia wanaweza kuyagharamia mafunzo hayo kwa kuwaajiri walimu kuwafunza watoto wakiwa katika kikundi kimoja.

Tukiilinganisha elimu ya Duksi na somo la Kiswahili, imebainika kuwa yote ni masomo yanayotolewa chini ya mifumo dhabiti. Kiswahili pia ni lugha ya kitaifa na kimataifa. Kutokana na maingiliano na lugha zingine, lugha hii imeathiri na pia ikaathiriwa na lugha zingine. Humu nchini, husomeshwa katika viwango mbalimbali kuanzia shule za chekechea hadi vyuo vikuu. Katika dunia ya kazi, watu wengi huitumia kwa mawasiliano. Hivyo basi kando na kuwaunganisha wanajamii, huweza pia kuwapa kitambulisho wanajamii husika popote pale.

Mfumo wa elimu ya Duksi hushughulikia masuala mengi katika maisha ya binadamu. Mafunzo hayo hushirikisha masomo juu ya imani ya kidini, Hesabu, lugha, afya, Historia, ukoo, utamaduni na maisha kwa jumla. Silabasi inayofuatwa na maalim hutilia mkazo kuikariri Korani, kuandika hati ya Kiarabu pamoja na kutoa matamshi sahihi ya Kiarabu. Mafunzo hayo hujumuisha marudio na mazoezi ya mara kwa mara (asubuhi, aduhuri, jioni na hata usiku).

Watoto wasipoyaelewa na kuyashika mafunzo wanapofunzwa, adhabu kali hutolewa. Wanaweza kupewa kazi zaidi kama ya kuandika au wafungiwe chumbani wasiweze kutoka humo ndani. Mwisho kabisa kiboko hutumiwa kwa watoto watukutu na watundu wanapokosa kutii makanyo. Watoto wafikishapo umri wa kujiunga na shule ya msingi ilhali hawajayamudu mafunzo ya Duksi, hulazimishwa kulirudia hilo darasa na kuendelea na masomo yote sawia. Kwa hivyo watoto hujikuta wana kazi nyingi kutoka mifumo yote miwili ya elimu. Hali hiyo huwalazimisha watoto kuanza masomo mapema au kumaliza usiku, kwani ratiba hutolewa ili kila siku watoto waamkapo waanzie au wamalizie kwa darasa la Duksi. Watoto wanaoshindwa kutimiza hayo masharti, huchapwa viboko na hata kufungiwa kwa nyumba wasipate nafasi ya kutoka nje wala kucheza na wenzao. Kama tulivyotaja hapo mwanzoni, tumechunguza jinsi mafunzo haya yanavyoingiliana na kuathiriana na mafunzo ya Kiswahili ambalo ni somo la lazima katika mfumo wa 8.4.4 nchini Kenya.

Kwa mujibu wa Macaro (2005), ujifunzaji wa lugha ya pili ni mifanyiko inayomwezesha mtu kupata fahamu, maarifa na ujuzi juu ya vipengele vya kisarufi. Mtu anapojifunza lugha, hujifunza kipengele kimoja kimoja kila wakati wala si kujifunza vipengele vyote vya lugha vinavyoingiliana na kuathiriana kwa wakati mmoja. Kutokana na habari hiyo maswali muhimu ambayo tulijiuliza tulipoangalia ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili ni kama yafuatayo:

- Ni mbinu au mifanyiko ipi ambayo inaweza kutumika wakati wanafunzi wanajifunza lugha?
- Je, ni njia zipi mwafaka zinazoweza kutumiwa ili kuendeleza mifanyiko hiyo?

Maswali hayo yametokana na nadharia tete kuwa wanafunzi wakifunzwa lugha mbili tofauti wakiwa bado wana umri mdogo pana uwezekano wa kutatizika kwani mifumo hiyo miwili huwa inaathiriana.

Aidha kutokana na utafiti imebainika kuwa mambo hayo yote ya ujifunzaji lugha yana uwezo wa kuwawezeshwa wanafunzi kuyaendesha maisha na shughuli zao za kila siku kwa urahisi kwani ujifunzaji wa lugha ya pili huweza kumbadilisha mtu. Masomo huweza kumpa mtu tajriba pamoja na utambulisho mpya wa kihisia, kiutamaduni na kiisimu. Ijapokuwa elimu hiyo inaweza kuendeshwa kutoka mahali popote pale, kazi hii ya utafiti imejikita katika elimu inayotolewa shuleni ambapo stadi zote nne (4) za lugha yaani kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika hutiliwa mkazo.

Ingawa mafunzo ya elimu ya Duksi yanaendeshwa katika miji mingine kama Lamu, Nairobi, Mombasa na Mumias, istilahi tofauti hutumika kama vile chuo. Mji wa Garissa umelengwa kwa sababu ya kuwepo kwa lugha mseto pamoja na tamaduni

changamano. Vile vile miji mingi hujumuisha mafunzo hayo yote ya kidini kwa jina la Madrassa. Mjini Garissa huenda bado mambo mengi yamehifadhiwa kutokana na kukaribiana kwake sana na kitovu cha mafunzo hayo ya Duksi yaani nchi jirani ya Somali. Katika jamii husika ya mji wa Garissa kuna lugha nyingi za kiasili kama Kisamburu, Kirendille, Kiborana na Kisomali.

Kama ambavyo tumeshataja, mtoto anapozaliwa kwa mfano katika jamii ya Kisomali, hutumia lugha ya kwanza kama Kisomali lakini anapojiunga na mafunzo ya elimu ya Duksi anakuta lugha ngeni (Kiarabu) ambayo anapaswa kuijua. Lugha ya kwanza ndiyo inayotumiwa kwa kutoa maelezo na ufafanuzi ilhali habari zote zimeandikwa kwa lugha ya Kiarabu. Kufikia hapo, ilidhihirika kuwa mwanafunzi kama huyo anaweza kujikuta ana takriban lugha nne (4) au zaidi za kutumia anapojiunga na shule ya msingi. Lugha hizo zinaweza kuwa Kisomali, Kiarabu, Kiswahili na Kiingereza. Hali hii humchanganyisha mtoto.

Ijapokuwa kila mtu anahitaji lugha kwa mawasiliano na utendakazi katika asasi za kijamii, kupata umilisi huo, inamlazimu mtu ajifunze mfumo na sheria za lugha husika ili aweze kujimudu katika lugha. Katika harakati za kujifunza lugha ngeni aghalabu wanafunzi hujikuta wamezitoa kauli na pia kutunga sentensi zisizo sahihi. Utafiti huu basi umekusudia kuangazia kiini cha ugumu wa kujifunza sarufi ya Kiswahili katika mazingira yaliyosheheni mafunzo ya elimu ya Duksi.

Lado (1957), anasema kuwa kauli mbovu zinazoweza kutolewa wakati wa kujifunza lugha ngeni huenda zikadhihirisha ugumu wanaoupata wanafunzi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ugumu na matatizo hayo yanaweza kuhusishwa na kutoafikiana kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili hususan katika mbinu za kufunzia na vipengele vya sarufi kama vile abjadi, msamiati, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno katika sentensi. Huenda matatizo hayo ya kuhamisha na kupanua dhana hizo katika lugha ya pili au ya tatu, yakahusishwa na athari ya lugha ya kwanza.

Utafiti huu umeonyesha usemi wa Weinreich (1953) kuwa ugumu wa ujifunzaji wa lugha ya pili unatokana na tofauti inayopatikana kati ya lugha ya kwanza na lugha ya pili. Anasema kuwa jinsi tofauti hizo zinavyozidi kuwa nyingi, ndipo miundo na taratibu zinavyozidi kupanua tatizo la ujifunzaji na uwezo wa kuelewa lugha hiyo.

Mtafiti amelishughulikia suala la athari ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi ya lugha ya Kiswahili mbali na masuala mengine kama vile mbinu za kufunzia. Ameangazia na kulinganisha utaratibu wa elimu ya Duksi na utaratibu wa elimu ya msingi, yaani ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili. Uchunguzi umefanywa juu ya mbinu zinazotumiwa kwa kufunza vipengele vya kisarufi kama inavyobainishwa. Sampuli changamano imetumiwa ambapo wanafunzi, walimu,

wazazi, maalim na maafisa wa elimu wameshirikishwa. Pia tathmini imefanywa kupitia kwa kazi za imla hususan kubainisha sehemu za mwili, kutunga sentensi na kufanya zoezi la kukamilisha vifungu (kwa kujaza mapengo). Matokeo ya uchanganuzi yamepimwa na kukaguliwa dhidi ya hali ya ujifunzaji katika shule zilizoteuliwa kutoka mji wa Garissa pamoja na viunga vyake. Shule za msingi ambazo zimehusishwa zilikuwa Young Muslim, Korakora, Sankuri na Garissa.

Vilevile imedhihirika wazi kuwa jamii hiyo husika huzingatia mno mafunzo ya kidini. Kunayo mipango mahsusi ya kuhakikisha watoto wanapata masomo kwa utaratibu maalum. Msingi huwekwa kwa kuanza na elimu ya Duksi na baadaye mafunzo ya madrassa hali ambayo imemwezesha mtafiti kupata habari tosha na yakini. Utafiti awali ulionyesha pia kuwa eneo hilo ni *bikra*. Kitaaluma ni tafiti chache zimewahi kulishirikisha eneo hilo.

Kwa hivyo uchanganuzi huu umenuia kuonyesha namna ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili huathiriwa na elimu ya Duksi. Utafiti huu umelenga kudhihirisha baadhi ya matatizo changamano yanayoweza kuhusishwa moja kwa moja na lugha ya kwanza ijapokuwa kuna sababu na masuala mengine ndani na nje ya Isimu yanayoweza kutinga ujifunzaji wa lugha ya pili. Tumejikita katika ujifunzaji kwani ni muhimu kuelewa namna wanafunzi hufunzwa na wanavyojifunza kando na kutambua walimu wanavyofunza kusudi yaweze kusaidia kutoa maelekezo na mashauri juu ya namna

ya kuteua mbinu na nyenzo za kufunzia. Hivyo basi kubainisha jinsi ya kuandaa ufunzaji unaoafiki hali, maslahi na mahitaji ya wanafunzi husika.

Utafiti huu umeshirikisha sampuli ya miji midogo ya mashambani wala si maeneo yaliyo katika miji mikubwa. Haya yote yalikuwa muhimu kwa sababu utafiti huu umedhamiria kupambanua masuala ambayo yanaweza kutatinga ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Mtafiti amenuia kutoa mchango katika Taaluma pana ya Isimu hususan Isimu Tumikizi na Taaluma finyu ya ufunzaji na ujifunzaji (kuangazia mbinu za kufunzia lugha) ili kuboresha na kuimarisha shughuli hiyo.

### **1.1 Suala la Utafiti**

Athari ya elimu ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili ndicho kiini cha utafiti huu. Hii ni kwa sababu kuna haja ya kuangazia vipengele vya kisarufi ambavyo vinachukuliwa kuwa vinaathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Utafiti wa awali (mahojiano ya ana kwa ana na mwanajamii Swaleh Hussein Osman kutoka mjini Garissa), ulionyesha kuwa kulikuwa na haja ya uchunguzi kufanywa ili kubainisha athari ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Udurusu wetu kufikia hapo ulionyesha kuwa hakuna utafiti ambao tayari umefanywa kwa misingi ya kisayansi na ripoti kuandikwa kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa lugha

ya Kiswahili katika mji wa Garissa. Utafiti huu basi umekusudia kufanya hivyo. Aidha umenuia kupambanua taratibu mbili za elimu; elimu ya Duksi na elimu ya 8-4-4 inayotoa masomo kama lugha ya Kiswahili, Hesabu na Kiingereza kati ya mengineyo.

Musau (1993), alitafiti juu ya kipengele cha fonolojia na kuelezea athari za lugha ya kwanza kwa ujifunzaji wa Kiswahili. Akilenga kiwango cha fonolojia. Aliwashirikisha wakufunzi wa vyuo vya shule za msingi. Walakini, kazi hii imejikita katika vipengele vya kisarufi. Aidha kazi ya Musau (1993) haikushughulikia Duksi ijapokuwa baadhi ya data ilikuwa ya Kisomali. Vile vile masuala yanayoweza kutatiza ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili yameshughulikiwa kuhakikisha ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili unaboreshwa na kustawishwa. Katika kufanya hivyo utafiti unadhamiria kutoa mchango katika taaluma ya Isimu jamii.

Kazi za Mudhune (1994) na Onyango (1990) pia zimeshughulikia athari za lugha ya kwanza na Kiswahili kama lugha ya pili. Pengo ni kwamba hazikulenga Duksi wala lugha ya Kiarabu. Hivyo basi pakawa na haja ya kuufanya utafiti huu.

Nchini Kenya, Kiswahili ni somo la lazima. Ufunzaji na ujifunzaji wake huathiriwa na lugha zingine pamoja na elimu ya kidini. Kutokana na hali hizo, imebainika kuwa kuna haja ya kuchunguza mambo yanayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

## 1.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umenuia kujibu maswali yafuatayo:

- i. Duksi ni elimu ya aina gani?
- ii. Je, ufunzaji na ujifunzaji wa elimu ya Duksi unatofautiana vipi na ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili?
- iii. Ni mbinu zipi zinazotumiwa kwa kuendesha mafunzo ya elimu ya Duksi?
- iv. Vipengele vya kisarufi vya elimu ya Duksi abjadi, mtindo wa kuandika na mpangilio wa maneno katika sentensi vinaathiri vipi ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili?
- v. Ni mikakati ipi ambayo inaweza kutumiwa katika kuboresha na kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili?

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu umelenga kufikia mambo yafuatayo:

- i. Kubainisha maana na utaratibu wa elimu ya Duksi
- ii. Kulinganisha na kulinganua taratibu za kisarufi(abjadi, mtindo wa kuandika, msamiati na mpangilio wa maneno

katika sentensi)

- iii. Kupambanua mbinu zinazotumiwa kwa kuendesha mafunzo ya elimu ya Duksi
- iv. Kuchunguza athari ya vipengele vya kisarufi: abjadi, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno katika sentensi wakati wa kujifunza lugha ya Kiswahili
- v. Kuangazia na kupambanua mikakati inayolenga kuimarisha na kufanikisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

#### **1.4 Nadharia Tete**

- i. Utaratibu na mbinu za kuendesha elimu ya Duksi inayotolewa kwa lugha ya Kiarabu ni tofauti na zile za elimu ya shule ya msingi hususan utaratibu wa lugha ya Kiswahili hivyo kuathiriana.
- ii. Vipengele vya Elimu ya Duksi huathiri ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili yaani abjadi, maendelezo, msamiati, mpangilio wa maneno katika sentensi na mtindo wa kuandika.

#### **1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Kwanza, ujifunzaji wa lugha ni suala nyeti katika maisha ya binadamu. Inampasa kila mtu kujifunza lugha vyema ili aweze kujiimarisha na kujimudu katika nyanja zote za

maisha (uchumi, siasa, elimu na utamaduni). Katika ujifunzaji wa lugha vipengele vya kisarufi ni muhimu. Kutokana na vipengele hivyo, mtu anaweza kushiriki katika mawasiliano na kuelewa habari za watu wengine barabara.

Udurusu wetu umeonyesha kuwa wanaisimu wengi wameshatafiti na kuandika mengi juu ya lugha za kigeni. Hakuna utafiti ambao umefanywa na maandishi kuandikwa kuhusu wanafunzi wanaopata mafunzo ya Duksi kisha mafunzo ya lugha ya Kiswahili kufuatia. Vile vile hakuna utafiti ambao umefanywa na ripoti kuandikwa juu ya mfumo wa elimu au ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika jamii hiyo ya eneo la Garissa.

Kutokana na matokeo ya utafiti awali imebainika kuwa, Mji wa Garissa ni mji wa jamii funge ukilinganishwa na miji mingine nchini. Akielezea, Hussein anadai kuwa wanajamii walioenda nje ya mji wameathiriwa kiasi cha hata kustahili kutengwa na wenzao ambao wamezaliwa na kuishi katika mazingira yayo hayo bila kusafiri nje tangu kuzaliwa kwao. Athari ya kutoka nje haikuwa imeingilia sana lugha, utamaduni na imani ya wanajamii (wa mji wa Garissa na viunga vyake) hao kinyume na hali ilivyo katika miji mingine nchini. Wanajamii hao wameweza kuwa sampuli mwafaka ambayo imeitoa data wazi. Sababu nyingine ni kuwa mafunzo ya dini katika viwango vya Duksi na Madrassa bado yanatiliwa mkazo mno katika mji huo ikilinganishwa na miji mingine nchini Kenya.

Ripoti za matokeo ya mitihani ya kitaifa zimeonyesha matokeo mabaya katika mkoa wa Kaskazini Mashariki. Mtafiti amekusudia kuangazia kiini cha matokeo hayo mabaya. Mapendekezo ambayo yamefikwa yanaweza kutumiwa na wanaoandaa mitaala, wanasera kutoka Wizara ya Elimu. Walimu pia wanaweza kuyatumia maoni hayo wanapoteua mbinu na nyenzo za kufunzia lugha ya Kiswahili na masomo mengine kwa jumla. Utafiti huu umenuia kutoa mchango kwa taaluma ya ufunzaji na ujifunzaji wa masomo hususan ya lugha.

Nyingi ya tafiti hizo ambazo zimewahi kufanywa hazikuingilia masuala ya utendakazi kama vile Isimu matumizi bali zilizingatia tu Isimu ya kijumla, mchango ambao ni wa lugha za kijumla. Kwa sababu kazi hii imeshughulikia lugha za Kiafrika, imekusudia kutoa mchango kwa jumla katika Isimu ya Kiafrika pia.

Utafiti huu umelenga kuchangia kwa kuonyesha namna Duksi inavyoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Imefanya hivyo kwa kuangazia uwezekano wa kuendesha elimu jumuiifu ambayo ni ya kutegemeana, kujengeana na kukamilishana.

Macaro (2005), anasema kuwa utafiti juu ya ujifunzaji wa lugha uwe wa maabara au wa darasani, una uwezo wa kutoa mchango muhimu katika mafunzo ya lugha leo hii. Aidha utafiti huu unachukua mtazamo wa kitaaluma na wa kiisimu na matokeo yake yanaweza

kuhamishwa na kutumika katika miktadha ya masomo mengine mbalimbali. Mtafiti amedhamiria kuwanufaisha walimu, wanafunzi, wanaolinda na wanaounda sera, wanaoandaa mitaala na watafiti wengineo kwa jumla siku za usoni.

### **1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu umefanywa katika eneo la mji wa Garissa na tarafa ya kati. Ijapokuwa masuala mengi yakiwemo ya kisiasa, kitamaduni na kijiografia yanaweza kutatiza ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, mtafiti amejifunga katika utaratibu wa elimu ya Duksi inayoendeshwa kwa lugha ya Kiarabu na ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili. Katika eneo lengwa lugha ambayo inaweza kuwa Kisomali au Kiborana ndiyo inatumiwa kama lugha ya kufafanulia msamiati wa Kiarabu wakati wa mafunzo ya Duksi. Athari za lugha za kiasili katika ujifunzaji na ufunzaji wa Kiswahili hazikuangaziwa.

Utafiti huu haukushughulikia moja kwa moja masuala ya kidini wala utamaduni bali vipengele vya kisarufi yaani abjadi, msamiati, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno katika sentensi. Ijapokuwa upambanuzi umetolewa juu ya mbinu za kuendesha elimu ya Duksi (inavyoendeshwa kwa lugha ya Kiarabu na Kisomali), maana, dhima na athari ya elimu hiyo imeangaziwa. Mtafiti ameshughulikia kiwango cha sintaksia: vipengele vya kisarufi kama vilivyobainishwa hapo awali. Ili kubainisha uwiano na tofauti kati ya lugha hizi mbili, shughuli ya kulinganisha na kulinganua

imefanywa. Mbinu za kuendesha mafunzo zimeshughulikiwa katika viwango vilivyotajwa. Vipengele hivyo vimechaguliwa kwa sababu sarufi ndio uti wa mgongo wa lugha yoyote ile.

### **1.7.0 Misingi ya Kinadharia**

Katika uwanja wa ujifunzaji wa lugha ya pili kunazo nadharia nyingi kwa mfano nadharia ya Uchanganuzi Makosa, Ubadilishano, Uhamishaji lugha, Lugha Kati na Uchanganuzi Linganishi (Ellis na wenzake, 2005). Nadharia hizo zote zinaweza kutumika kuelezea kazi za ujifunzaji na ufunzaji wa lugha. Tumepitia kila nadharia huku tukiangazia mihimili yake. Tumetoa sababu ya kuchagua nadharia moja ya Uchanganuzi Linganishi na kuziacha nyinginezo.

#### **1.7.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa**

Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ni mojawapo ya nadharia kongwe katika uchanganuzi wa lugha ya pili. Nadharia hii iliasisiwa na Corder (1981) na ina utaratibu ufuatao:

- Kutambulisha makosa
- Kuelezea na kufafanua makosa ambayo yanaweza kutokea katika matamshi au katika kufasiri ingawa ni vigumu kubainisha kiisimu kiini cha makosa hayo
- Kuchanganua makosa ambayo mwanafunzi anaweza kufanya anapojifunza lugha ngeni.

### **1.7.2 Natija ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa**

Nadharia hii ina uwezo wa kudhihirisha vipengele ambavyo wanafunzi wanaelewa na hata pale wanapokosa kuelewa, mambo yafuatayo yanaweza kujitokeza:

- Kubainisha namna mtu hujifunza lugha yoyote ile
- Kuweka wazi makosa, hali inayoweza kuwasaidia wakati wa kufanya marekebisho. Wanaojifunza lugha wanaweza kugundua sheria za lugha lengwa.

### **1.7.3 Upungufu wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa**

Hata hivyo nadharia hii imeripotiwa kuwa na upungufu ufuatao:

- Taylor (1988), akinukuliwa na Ellis na mwenzake (2005) anasema, makosa anayoyafanya mwanafunzi hayapimiki
- Nadharia hii inajikita katika makosa anayoyafanya mtu anapojifunza lugha. Hivyo basi haiafiki mahitaji ya kulinganisha lugha mbili
- Haitoi picha kamili ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Inashughulikia tu makosa anayoyafanya mwanafunzi anapojifunza lugha huku ikipuuza anayoyaelewa vyema
- Nadharia hii hutilia mkazo mifanyiko pekee. Haiielezei kwa nini anayejifunza lugha huenda akakwepa maumbo mengine wakati anapojifunza lugha tofauti Sposky (1989).

### **1.7.4 Nadharia ya Lugha Kati**

Nadharia hii ni mojawapo ya nadharia zinazoweza kutumika kwa kulinganisha lugha mbili. Nadharia hii iliasisiwa na Selinker (1972).

Nadharia hii ina maoni kuwa kurejelea sarufi ubongoni ni hatua muhimu mwanafunzi anapojifunza lugha. Hali hiyo ya kufahamu na kuyashika yanafunzwa hujengwa kwa hatua dhabiti katika mifanyiko ya ujifunzaji huo. Nadharia hii haina sheria bali kunayo masuala ya kiisimu anayojifunza mwanafunzi. Mengi ya mambo anayoyajua na kutumia mwanafunzi huwa yanahamishwa kutoka mfumo wa lugha ya kwanza. Habari hizo hazina umbo na muundo dhabiti na huenda zikaathiriwa na lugha ya kwanza.

#### **1.7.5 Mchango wa Nadharia ya Lugha Kati**

Umuhimu wa nadharia hii ni kuwa inatuelezea jinsi mtu hujifunza lugha. Inafafanua mapito katika kujifunza lugha. Inasisitiza kuwa anayejifunza lugha ya pili hujikuta ameongezea dhana (kwa sababu ya kutaka kuijumuisha na kuirahisisha dhana). Kwa hivyo lugha kati ni lugha ya mpito inayobadilikabadilika kutegemea wakati.

#### **1.7.6 Upungufu wa Nadharia ya Lugha Kati**

Nadharia ya Lugha Kati ina upungufu ufuatao:

- Wanaisimu wana maoni tofauti juu ya Lugha Kati kwani Ellis na mwenzake (2005), wakimnukuu Gregg (1990), wanaongea juu ya mitazamo miwili tofauti: Lugha Kati ni zao linaloakisi kukua kwa ubongo na papo hapo kwa upande mwingine ni suala la Kiisimu
- Nadharia hii haiafiki mahitaji ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Inaelezea tu kipengele

cha umilisi wa lugha wala haina uwezo wa kulinganisha na kulinganua lugha mbili. Haishughulikii utendakazi kwa hivyo hatukuitumia nadharia ya lugha kati katika utafiti huu.

### 1.7.7 Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi

Mtafiti ameteua nadharia ya Uchanganuzi Linganishi kwa sababu ina uwezo wa kushughulikia ulinganifu wa lugha mbili kama ilivyoangaziwa. Nadharia hii iliasisiwa mwanzoni na Fries (1945) kisha baadaye ikapambanuliwa na Lado (1957). Spolsky (1989), anasema nadharia ya Uchanganuzi Linganishi iliibuliwa na kuongezewa vipengele vya Sarufi Jumulifu. Inapotumika huonyesha zaidi uwiano na tofauti kati ya lugha mbili.

Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ina mihimili ifuatayo:

- Kwa mujibu wa Lado (1957), katika ujifunzaji wa lugha kuna ugumu na viziwi.
- Kiini au sababu kuu ya ugumu na kutokea kwa makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili inatokana na uhamishaji wa dhana kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili
- Kulingana na Weinreich (1953), upo uwezekano wa kukisia na kutabiri ugumu na makosa wakati wa kujifunza lugha ya pili kutokana na tofauti zinazopatikana kati ya lugha mbili husika
- Ili kurahisisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili, tofauti kati ya lugha ya

kwanza na lugha ya pili hubainishwa ili ishughulikiwe ipasavyo wakati wa kujifunza kwa kutiliwa mkazo.

Imebainika kuwa mihimili hiyo inaweza kutumika katika utafiti huu. Mtafiti ameteua nadharia hii kwa sababu kuna hali ya kulinganisha na kulinganua taratibu za elimu ya Duksi zinazohusu lugha ya Kiarabu na vipengele vya kisarufi: abjadi, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno katika sentensi na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Mihimili ambayo imeongoza utafiti huu ni kama ilivyoelezwa hapa chini:

- Kutoa taratibu za lugha mbili zitakazolinganishwa ili uwiano na tofauti ibainishwe
- Kutenga tofauti zikishabainishwa, kwani itakuwa rahisi kutambua vipengele ambavyo huenda vikasababisha ugumu katika ujifunzaji wa lugha ya pili
- Spolsky (1989), anasema mwalimu na mwanafunzi wakibaini uwiano na tofauti kati ya taratibu mbili za lugha husika itakuwa rahisi kugundua na kubainisha vipengele ambavyo vinastahili kutiliwa mkazo ili kurahisisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili

Nadharia hii imechukuliwa kuwa makisio yanaweza kutolewa pamoja na maelezo juu ya muundo ambao unaweza kusababisha ugumu katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Ellis

(1985), anatoa utaratibu wa nadharia ya Uchanganuzi Linganishi na ni kama ufuatavyo:

- Kutoa maelezo juu ya lugha ya kwanza na lugha ya pili ambapo kwa muktadha wa kazi hii ni lugha ya Kiarabu na Kiswahili
- Kufafanua vipengele vya kisarufi vitakavyoteuliwa na kushirikishwa katika uchunguzi yaani abjadi, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno katika sentensi
- Kudhihirisha mpangilio wa maneno katika sentensi kwa mfano nomino, vitenzi na vivumishi. Kulinganisha na kulinganua uwiano na tofauti kati ya lugha mbili husika
- Kukisia na kutabiri vipengele vinavyoweza kusababisha matumizi ya sarufi mbaya.

Kama ambavyo tumeelezea hapo juu, maelezo ya tafsili yametolewa kuhusu taratibu hizo za ujifunzaji. Maelezo yameshirikisha vipengele vya kisarufi: abjadi, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno katika sentensi pamoja na mbinu za kufunzia lugha. Palipo na tofauti ndipo pamechukuliwa kuwa kiini kinachosababisha ugumu katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Hivyo basi walimu wamehimizwa kupazingatia palipo na tofauti wanapofunza.

Kutokana na maelezo ya utaratibu wa nadharia ya Uchanganuzi Linganishi imebainika kuwa hii nadharia ni mwafaka kwa utafiti huu. Nadharia hii imeundwa kwa lengo la

kuchunguza ugumu ambao wanafunzi walio na lugha yao ya kwanza hupata wanapojifunza lugha ya pili. Haya yameafikiana na madhumuni ya utafiti huu kwani kuna lugha mbili zinazolinganishwa (Kiarabu na Kiswahili).

Hata hivyo nadharia hii ya Uchanganuzi Linganishi imelaumiwa kwa kuwa na mtazamo finyu kuhusu ujifunzaji wa lugha. Kwa mujibu wa Weinrech (1953), kuna madai kuwa nadharia hii huaangazia njia moja tu ya kujifunza lugha ambayo ni uhamishaji wa dhana hasi. Msemaji anapoitumia lugha ya pili, hujikuta ameyatumia maneno anayoyaelewa na kuyazoea katika lugha yake ya kwanza. Nadharia hii hutilia maanani hatua na mapito apitiayo mwanafunzi anapoanza kujifunza lugha hadi anapojua kiasi cha kuupata umilisi.

Ellis (1985), anashikilia kuwa suala la kutabiri makosa yasiyokuwepo, limepingwa kwani utafiti wa kisayansi umeonyesha kuwa wanafunzi hujaribu kukwepa kutumia maneno magumu wanapojifunza. Anasema kuwa makosa ya wanafunzi kati ya thuluthi moja na nusu hutokana na athari ya lugha zao za kwanza.

Hata hivyo imebainika kuwa lengo kuu la Uchanganuzi Linganishi ni kuangalia nafasi ya lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa lugha ya pili wala sio kutabiri makosa yasiyohusishwa na mwanafunzi. Isitoshe hata nadharia hiyo ya kuchanganua makosa pia inao upungufu kama vile kutotoa picha kamili ya ujifunzaji wa lugha ya pili. Inayo mazoea ya kujikita tu kwa makosa badala ya kuzingatia uwezo alio nao mwanafunzi

katika utendakazi. Vile vile, upungufu mwingine ni kuwa nadharia hiyo haina uwezo wa kutabiri makosa ambayo anaweza kuyafanya mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili.

#### **1.7.8 Sababu za Kuchagua Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi**

Nadharia hii imeteuliwa kwa sababu zifuatazo:

- Nadharia hii ina uwezo wa kuelezea kiini cha wanafunzi kufanya makosa wanapojifunza lugha ya pili
- Nadharia hii ina uwezo wa kuonyesha uwiano na tofauti kati ya lugha mbili
- Kutokana na utaratibu wa kulinganisha na kulinganua, vipengele vinaweza kutatiza ujifunzaji wa lugha lengwa vinaweza kubainika. Habari hiyo inaweza kumfaidi mwalimu na mwanafunzi wakati wa kufunza na kujifunza lugha.

Kwa jumla nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ina manufaa ya moja kwa moja darasani. Kramer (1975), anaelezea kuwa mwanafunzi anaweza kuelewa uwiano na tofauti iliyoko kati ya lugha yake ya kwanza, pili na ya tatu. Mwalimu anaweza kuwaonyesha wanafunzi uwiano huu kama njia ya kuwapa moyo kando na kuwawekea msingi dhabiti. Mwalimu anaweza kulianzisha somo kwa kutanguliza kuwafunza penye uwiano ili kurahisisha ujifunzaji huku akiendelea kuongeza mambo mapya taratibu. Kwa sababu hii, mtafiti ameonelea kuwa ni bora kutumia nadharia hii katika utafiti. Utaratibu huu umeweza kubainisha pale ambapo panaweza kuwa na ugumu mwanafunzi anapojifunza lugha yoyote ile.

### 1.8.0 Udurusu wa Maandishi

Kunazo durusu na tafiti nyingi ambazo zimeshughulikia suala la ujifunzaji wa lugha ya pili. Scotton (1969), aliangazia matatizo yanayotokea kati ya Wabaganda na Waluhya wanapojifunza Kiswahili Sanifu. Lengo hasa lilikuwa kubainisha jamii iliyokuwa na matatizo mengi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huo ulijikita katika vipengele viwili vya lugha; fonolojia na sintaksia. Utafiti huo ulionyesha kuwa Wabaganda walipata ugumu zaidi katika kujifunza Kiswahili kuliko Waluhya. Makosa mengi yalikuwa ya kisarufi kama vile matumizi mabaya ya vbadala na viwakilishi. Utafiti huu umechangia kazi hii kwa kuangazia vipengele vya kisarufi: fonolojia na sintakia.

Whiteley (1974), anasema kuwa ijapokuwa kulikuwa na vishawishi vingi vya kutaka Kiingereza kifunzwe na kitumike takriban katika nyanja zote za maisha, uchunguzi wake kuhusu matumizi ya lugha mbali mbali nchini, ulidhihirisha kuwa Kiswahili hutumika kwa wingi kuliko lugha zingine za kiasili nchini Kenya hususan kwa shughuli za mawasiliano, biashara, siasa, kidini na hata katika asasi zingine za kijamii. Kutokana na utafiti huu, imebainika kuwa utafiti juu ya ujifunzaji uliwekewa misingi zamani. Pia imetambulika kuwa lugha ya Kiswahili ina dhima kuu katika jamii. Kutokana na utambuzi huo, wanafunzi wanaweza kupata motisha na ari ya kutaka kusoma hasa baada ya kung'amua umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika jamii na maisha yao ya usoni.

Wasomi wengine ambao wameshughulikia ujifunzaji wa lugha ya pili ni kama, Wanyoike (1978) na Mbaabu ((1985). Wao wanaafikiana kuwa watu wanaojifunza lugha ya pili hupata shida kutokana na athari ya lugha ya kwanza. Wanyoike (1978), anapendekeza utafiti wa kina ufanywe na watu walio na umilisi wa lugha ya Kiswahili. Akisisitiza anasema, matokeo ya utafiti yanaweza kutumiwa na wanaoandaa mitaala katika maandalizi itakayolenga na kuafiki mahitaji ya wanafunzi. Hali hii inaweza kurahisisha na kuboresha ufunzaji na ujifunzaji.

Mbaabu (1985), alitafiti juu ya takriban vipengele vyote vya sarufi na lugha ya Kiswahili. Alianza kwa kuangazia mitazamo ya historia na ya kiutamaduni kuhusu lugha na hali ya lugha katika eneo la Afrika Mashariki. Pia kwa ufupi kazi hiyo ilianguzia athari katika viwango vya fonolojia, sarufi na semantiki. Baadhi ya lugha zilizohusishwa ni kama Kikamba, Kikalenjini, Kikisii, Kibukusu, Kiluo, Kimeru na Kiluhya. Utafiti huo ilionekana kuwa utafiti mpana kwani ulilenga lugha nyingi.

Kazi hiyo inatofautiana na hii ambayo inajikita kwa taratibu za elimu ya Duksi na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili shuleni. Pili, utafiti huu umezingatia kulinganisha na kulinganua vipengele vya kisarufi za lugha hizo mbili tofauti. Tatu, sampuli ya kazi hii ni changamano. Imehusisha wanafunzi, walimu, maafisa wa elimu na wazazi. Utafiti huo basi, umemwezesha mtafiti kutambua palipo na pengo la kujazwa.

Ogolla (1990), alifanya utafiti juu ya lugha ya Kiswahili hususan mielekeo ya wasomi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Kazi hiyo ilionyesha kuwa mielekeo ni zao la jamii na husababishwa na utamaduni wa jamii ambamo lugha mbali mbali huzungumzwa. Hayo yote yalichunguzwa chini ya misingi ya Kisaikolojia. Utafiti huo umetoa mwangaza zaidi katika suala la utafiti.

Besha (1991), alifanya utafiti juu ya matatizo ya watu wazima katika jamii ya Wamasai wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Alionyesha ugumu wanaoupata Wamasai wanapojifunza lugha. Utafiti huo ulishughulikia matatizo ya kimuundo kati ya lugha ya kwanza na ya pili ambayo ni Kiswahili. Wamasai wana shida ya kuelewa ukubalifu wa sarufi iliyo mojawapo ya sifa kuu ya lugha ya Kiswahili. Ijapokuwa kazi hiyo ilijihusisha na sampuli ya watu wazima, matokeo yake yameangazia mielekeo yao juu ya lugha kwa ujumla wake.

Tafiti nyingi zimeshughulikia jamii za Kibantu na Kinailotiki lakini utafiti huu utaangazia jamii ya Kikushitiki. Vile vile utafiti mwingi umejikita katika fonolojia. Kazi hii imezingatia vipengele vya kisarufi kama ilivyoelezwa hapo juu. Kufikia hapo imebainika kuwa bado kuna pengo la kujazwa hasa katika ujifunzaji na ufunzaji wa lugha katika eneo hilo ambalo halijashughulikiwa sana.

Kama tulivyosema hapo mbeleni, Musau (1993) alifanya utafiti juu ya ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya pili, kipengele cha fonolojia. Alishirikisha wanafunzi waliokuwa wanajifunza lugha ya pili (Kiswahili). Wanafunzi hao walitoka katika jamii saba (7) ambazo hutumia lugha tofauti: Kikalenjini, Kikamba, Kibukusu, Kisomali, Kimasai na Kiluo. Utafiti wake ulizingatia matamshi yaani namna ya kutamka na kuelewa fonolojia ya Kiswahili. Lengo lake kuu lilikuwa kubainisha masuala yanayochangia muundo wa fonolojia ya mwanafunzi wa Kiswahili. Ilibainika kuwa mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili, yeye huhamisha baadhi ya istilahi kutoka lugha yake ya kwanza. Ugumu hutokea anapokumbana na mambo mageni katika lugha ya pili. Hata hivyo mwanafunzi hujikakamua akajiundia lugha anayoibadilishabadilisha kila anapojifunza dhana zingine kutoka kwa lugha ya pili. Kazi hiyo inaingiana na utafiti huu kwani kuna hali ya kushughulikia ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya pili.

Katika ujifunzaji wa lugha ya pili na hali ya ufutaji wa tabia na uhamishaji wa dhana kuu hutokea huku ujifunzaji ukiendelea Lado (1957). Hali hii inatokana na uhamishaji wa dhana hizo. Athari hiyo ndiyo hutatiza ujifunzaji wa lugha ya pili. Kupitia kwa nadharia ya Uchanganuzi Linganishi, vipengele vya kisarufi ambavyo vina athari inayotatiza ujifunzaji vinaweza kushughulikiwa kwa mapana. Vipengele hivyo vinaweza kupewa kipaumbele baada ya kubainishwa wakati wa kuandaa mitaala. Mtafiti amekusudia kuwa kutokana na utafiti huu anaweza kuyatambua masuala mengine ambayo yanaweza kutatiza ujifunzaji wa lugha mbali na hivyo basi kujaza pengo.

Mudhune (1994), anadhibitisha kuwa kuna tofauti kati ya Kiluo na Kiswahili kisarufi na tofauti hizi hutatiza ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huo ulizingatia nadharia ya Uchanganuzi Linganishi huku akiangazia viwango vya lugha. Alihusisha wanafunzi wa darasa la sita kutoka shule za msingi wilaya ya Siaya. Alijikita katika vivumishi, tarakimu, vimilikishi na viwakilishi. Lengo lake lilikuwa kubainisha makosa ya kisarufi ambayo yanahusishwa na lugha ya kwanza ijapokuwa huenda makosa hayo yakasababishwa na mambo mengine.

Utafiti huo uliangazia pia kiini cha matatizo katika lugha. Kazi hii inaingiana moja kwa moja na utafiti huu kwani suala la ujifunzaji limeshughulikiwa kwa kina. Akimnukuu Lado (1957), anasema aghalabu wanaojifunza lugha ya pili hutunga sentensi zenye makosa kulingana na sheria za lugha hiyo ya pili. Makosa hayo ya sarufi yanadhihirisha ugumu wanaoupata wanafunzi katika kuelewa dhana ngeni katika lugha ya pili. Naye Weinreich (1953), anasema kuwa ugumu unaweza kukadiriwa kwa kulinganisha na kulinganua lugha husika. Katika kulinganisha, sehemu zenye tofauti hubainishwa ili hatua mwafaka zipate kuchukuliwa hivyo kupunguza ugumu wa kujifunza na hata ikiwezekana kuondoa athari hiyo kama asemavyo Fries (1945).

Mathooko (2004), alilenga lugha za Kiafrika (Kitharaka na Kikamba). Mtafiti aliangalia namna (wenyeji wa mkoa wa Mashariki) wamekuwa wakiingiliana na kuathiriana kwa

miaka mingi. Alitaka kutambua athari katika viwango vya fonolojia na kisemantiki pamoja na athari za muundo wa kijamii. Utafiti wake ulikuwa wa kiisimu jamii.

Kufikia hapo imebainika kuwa vipengele vya kisarufi vingi havijashughulikiwa; abjadi, matamshi, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno kando na mbinu za kufunzia.

#### 1.9.0 Mbinu za Utafiti

Katika kuishughulikia kazi hii, mbinu kuu mbili (2) za uchunguzi zilihusishwa nazo ni: utafiti wa maktabani na wa nyanjani. Mbinu hizo zilichaguliwa kusudi kumwezesha mtafiti kuikusanya data yakini na tosha. Mtafiti aliweza kusoma vitabu, majuzuu, tasnifu, majarida na machapisho mengi. Hali hiyo ilimwezesha mtafiti kupata uelewa, ufafanuzi na maelezo zaidi juu ya eneo, wanajamii na mada ya utafiti.

Utafiti zaidi ulifanywa nyanjani ambapo eneo la Kaskazini Mashariki lilihusishwa. Mtafiti alihudhuria madarasa ya Duksi kando na kuwahoji ana kwa ana walimu, maalim, wazazi, wanafunzi, maafisa wa elimu na wazee wa kijiji. Kulikuwa na vipindi mbalimbali: vya kusikiliza, kuangalia, kuandika, kuuliza na kujibu maswali, kuchukua picha na kutathmini. Hatua hizo kwa pamoja zilimwezesha mtafiti kuipata data ya kina na wakilishi kwani kulikuwa na miktadha tofauti tofauti kama vile chini ya miti, ndani ya jengo, mjini, shambani, shuleni na chuoni.

### 1.9.1 Sampuli Iliyoshirikishwa

Mji wa Garissa na viunga vyake ndilo eneo lililotoa sampuli. Sampuli changamano ilishirikisha wanafunzi, maalim, walimu, wazazi, wazee na maafisa wa elimu. Shule nne (4) za msingi zilihusishwa.

### 1.9.2 Ukusanyaji wa Data

Katika kukusanya Data, mbinu kuu mbili (2) zilihusishwa yaani utafiti ulifanywa maktabani na nyanjani:

### 1.9.3 Maktabani

Utafiti wa maktabani ulijumuisha:

- i. Kuzuru na kusoma mitaala, silabasi, tasnifu, makala, majarida, magazeti na vitabu vilivyoandikwa na wataalamu mbalimbali kando na maelekezo ya kisera
- ii. Kutembelea vituo vya kuhifadhi habari kama Chuo Kikuu cha Kenyatta, Taasisi ya Elimu, Chuo Kikuu cha Nairobi na Afisi Kuu ya Wizara ya Elimu.

Haya yametusaidia kupata ufahamu na kupambanua zaidi juu ya mada ya utafiti, ufunzaji na ujifunzaji wa lugha elimu ya Duksi, sarufi ya Kiswahili, historia ya mkoa husika pamoja na wakazi wake. Vile vile kutokana na maandishi ya udurusu, mtafiti amepata mwangaza zaidi juu ya nadharia ya Uchanganuzi Linganishi na nadharia zingine zilizoelezea juu ya uwanja huu. Mtafiti aliweza kusoma na kupata maelezo juu ya

historia, mihimili mbali na uzito wa nadharia zinazohusu ujifunzaji wa lugha ya pili. Mtafiti alishughulikia vipengele vya lugha ya Kiswahili kama abjadi, sauti, silabi, fonimu, maneno, kauli na Isimu kwa mapana yake. Habari hizo zote zimekuwa mchango katika utafiti huu. Kwa jumla mtafiti mwishowe aliweza kung'amua kazi ambazo tayari zilikuwa zimeshashughulikiwa na kutambua pale palipokuwa na pengo la kujazwa.

#### 1.9.4 Nyanjani

Uchunguzi wa nyanjani umefanywa katika mkoa wa Kaskazini Mashariki yaani mji wa Garissa na viunga vyake. Mbinu ya mahojiano, hojaji, kuhudhuria mafunzo halisi kando na majibizano kati ya mtafiti na watafitiwa zilihusishwa. Hivyo basi sampuli changamano ilitumika. Walioshirikishwa walikuwa washika dau kama vile: maafisa wa elimu, maalim, wazazi, walimu na wanafunzi wa shule za msingi. Shule mbili (2) za mjini zilizohusishwa, shule ya msingi ya Young Muslim na ya Garissa. Kwa sababu ya kutaka kudhihirisha athari ya mashambani, shule mbili (2) kutoka tarafa ya kati, Korakora na Sañkuri zilishirikishwa. Shule nne (4) ziliteuliwa kwa shughuli ya kulinganishwa. Lengo lilikuwa kurahisisha na kufanikisha ukusanyaji wa data tosha na yakini.

Data imekusanywa kupitia kwa sampuli iliyoteuliwa (mbinu kusudio ilitumiwa). Mbinu kusudio imetumiwa ili kufikia shule ambazo zilikuwa zinaafiki mahitaji ya mtafiti. Walimu wanne (4) kutoka katika kila shule walihojiwa. Vile vile wanafunzi ishirini na nne (24) walijaza hojaji. Wanafunzi sita kutoka kila shule walihojiwa. Kulingana na

Milroy (1987), idadi hiyo iliteuliwa kulingana na sheria za kuchunguza lugha hususan katika uchunguzi wa lugha. Aidha wazazi wawili (2) kutoka kila shule na pia maafisa wa elimu wawili (2) walihojiwa. Idadi hiyo imetosheleza mahitaji ya utafiti kwani idadi kubwa sana huzidisha matatizo wakati wa utafiti badala ya kurahisisha utafiti. Maalim wawili (2) walihojiwa katika shule ya Young Muslim.

Makundi haya manne yaliteuliwa kwa sababu wao ndio wanaohusika na elimu kwa njia ya moja kwa moja. Wanafunzi ndio wanaojifunza lugha ya pili. Wazazi ndio wanaothamini na kufadhili aina zote mbili za elimu (Duksi na elimu ya shule za msingi). Maalim ndio wanaowafunza wanafunzi elimu ya Duksi. Walimu ndio waelekezi na maafisa wa elimu ndio walinda sera za elimu katika wilaya na mkoa husika. Wanafunzi wa darasa la tano walilengwa kwa sababu ya umri na kiwango cha elimu hali ambayo iliwawezesha kutoa mchango na maoni yao. Wameweza kujibu maswali na pia kuandika habari wakati walipohitajika kujaza hojaji.

Kulingana na sera ya elimu, lugha ya pili au ya tatu hutiliwa maanani kuanzia darasa la tatu. Baada ya wanafunzi kusoma mwaka mzima tathmini iliweza kufanywa. Vile vile wanafunzi waliweza kuelezea ugumu au matatizo kwani walikuwa wamekwisha kukumbana na hali hiyo ya kubadilisha kutoka elimu ya Duksi na kuanza kujifunza lugha ya Kiswahili shuleni au kusoma Duksi kabla ya kuanza elimu ya shule ya msingi. Kiwango cha juu zaidi (madarasa ya 6-8) hakikulengwa kwa sababu muda unapopita

huenda akili zao zikazoea taratibu zote na kusahau ugumu walioupata wakati wa kubadilisha kutoka elimu ya Duksi hadi ujifunzaji wa elimu ya sarufi ya Kiswahili.

Mtafiti aliweza kuhudhuria vipindi vya lugha darasani ili aone na kusikia jinsi wanafunzi hao walivyoshirikishwa katika somo na mchango wao, katika kusoma na kukariri maneno na kauli. Hatimaye wanafunzi waliyatungia maneno husika sentensi. Mtafiti basi aliweza kupata fursa ya kunakili habari muhimu kulingana na yale yaliyojiri kuhusu abjadi, matamshi, mtindo wa kuandika, maendelezo na athari ya Duksi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Kando na kuhudhuria somo, mtafiti alisaidiwa na walimu wa darasa la tano (5) shuleni kuteua wanafunzi kumi walioshiriki katika mahojiano. Mbinu bahatishi imetumika katika uteuzi wa kikundi hicho. Rejesta ya darasa la tano ilitumika. Milroy (1987), anasema sheria za kuchunguza lugha haziruhusu idadi kubwa sana ya washirikishwa. Wengi wa wanafunzi waliweza kufurahia kushirikishwa. Walijisikia huru kutoa habari ambayo hawangeweza kutoa mbele ya darasa kuhusu abjadi, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno katika elimu ya Duksi. Isitoshe mbinu bahatishi ilitumiwa kuhakikisha jinsia zote zinahusishwa kama inavyostahiki. Mtafiti anaamini kuwa waliweza kutoa habari nyingi ambazo zimechanganuliwa ili kufikia uamuzi wenye mashiko.

Kama yalivyokuwa matarajio yake mtafiti alichagua matumizi ya hojaji kama mbinu ya utafiti. Hojaji pia zilitumiwa. Hojaji ambazo zilitumiwa zilikuwa na maswali juu ya elimu ya Duksi, vipengele vya kisarafu kama abjadi, mtindo wa kuandika, maendelezo na mpangilio wa maneno katika sentensi. Hojaji zilijazwa na wanafunzi kumi waliochaguliwa kupitia mbinu bahatishi. Kwa mujibu wa Milroy (1987), sampuli iliteuliwa kwa kuzingatia lugha, umri na jinsia. Ili kufuatilia hatua vilivyo kama mbinu za kijamii zinavyotaka. Hali hiyo ilimwezesha mtafiti kupata habari za kina. Wanafunzi wameyatoa maoni yao kulingana na tajriba zao juu ya elimu ya Duksi. Pia waliweza kuandika abjadi za Kiarabu, majina ya sehemu za mwili na kisha wakayatungia sentensi maneno hayo. Ilibainika kuwa athari ya Duksi iliweza kudhihirika kupitia kwa majibu ya wanafunzi.

Mtafiti aliwahoji walimu wanane (8); wawili kutoka kila shule, aliwahasisha walimu wanaofunza lugha ya Kiswahili, darasa la tano. Mahojiano hayo yalihusu ufafanuzi wa utaratibu wa elimu ya Duksi, uwiano na tofauti kati ya taratibu mbili za elimu, mikakati ambayo imeshafanywa tayari na inayoweza kufanywa siku za usoni ili kuboresha na kuimarisha ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya Kiswahili mbali na kubainisha masuala yanayoweza kutatiza ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Walimu pia walijaza hojaji. Waliandika maana ya Duksi. Waliweza kuweka bayana tofauti kati ya mafunzo ya Duksi na ya Kiswahili kwa misingi ya tajriba zao. Fauka ya

hayo masuala mengine ambayo yanaweza kuathiri ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili yalipambanuliwa.

Maafisa wa elimu wawili wilayani, waliteuliwa ili wachangie kama maafisa wanaolinda sera katika kiwango cha wilaya na mkoa. Waliangazia kama walivyotarajiwa hali ilivyo katika eneo husika kando na kufafanua mikakati ambayo inaweza kuimarisha na kuboresha ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya Kiswahili katika eneo lilohusishwa. Walielezea kiini cha matokeo mabaya katika mitihani ya Kitaifa. Wazazi pia walihusishwa. Walihojiwa kuhusu maana, historia na utaratibu wa mafunzo ya elimu ya Duksi. Mahojiano hayo yalihusu maoni yao juu ya elimu jumuiifu, elimu ambayo imekusudiwa kumwandaa mtoto kwa masomo ya baadaye. Kwa jumla kila kundi limeteuliwa kimaksudi ili kufanikisha uchunguzi wa kina na kisha kuyajumuisha maoni.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

- **Nyanjani**

Data imekusanywa na kujumuishwa kutoka kwa makundi matano ambayo ni ya walimu, maalim, wazazi, wanafunzi na maafisa wa elimu. Katika kufanya hivyo, utaratibu wa kuchunguza na kuchanganua umefuatwa kwa makini. Hojaji za wanafunzi zimechanganuliwa ili kuonyesha jinsi wanafunzi wanavyofasiri elimu ya Duksi (ina umuhimu gani kwao?). Tathmini ya athari ya Duksi katika matamshi na maendeleo ilifanywa kupitia uchanganuzi wa majibu katika mahojiano na hojaji juu ya maana,

historia na utaratibu wa elimu ya Duksi. Mielekeo kuhusu elimu ya Duksi kwa jumla ilipambanuliwa kulingana na majibu ya wanafunzi na yale mtafiti aliweza kukusanya kutokana na kuhudhuria masomo kadhaa (matamshi, maendelezo, mtindo wa kuandika na mbinu za kufunzia lugha). Alifaulu kupata fursa ya kusikia na hata kushuhudia yaliyojiri.

Kutokana na mahojiano kati ya mtafiti na walimu, mielekeo ya walimu juu ya elimu ya Duksi imebainika. Fasiri ya walimu kuhusu maana na dhima ya elimu ya Duksi ilianguziwa. Kupitia kwa upambanuzi wa habari ambayo imekusanywa (kwa kutumia mbinu ya mahojiano na hojaji) matatizo yanayoweza kukinza ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya Kiswahili yamejadiliwa kwa kina.

Maafisa wa elimu waliweza kutoa habari kuhusu kijielezi, historia, umuhimu na utaratibu wa Duksi kupitia kwa hojaji na mahojiano. Mikakati ya kurahisisha na kuimarisha ujifunzaji na ufunzaji wa lugha ya Kiswahili ilijadiliwa. Kupitia kwa mahojiano, wazazi pia waliweza kutoa habari kuhusu abjadi, mtindo wa kuandika na historia ya elimu ya Duksi. Hatimaye waliwasilisha mapendekezo yanayoweza kusaidia katika kustawisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

#### **1.9.6 Uwasilishaji wa Data**

Uwasilishaji wa data yote iliyokusanywa imejumuishwa njia ya maelezo, michoro, picha, majedwali na vielelezo. Maelezo yametumiwa kwa kutanguliza na kutamatisha kila sura.

Majedwali yamedhihirisha tofauti kati ya lugha husika. Picha zimedhihirisha hali halisi hususan palipo na maalim na watoto wanaopokea mafunzo ya Duksi chuoni. Matatizo yaliyotambuliwa kuwa vikwazo katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili yameelezwa kwa njia ya nathari. Vile vile mapendekezo juu ya namna ya kukabiliana na matatizo hayo yakafafanuliwa ili kuweza kuiboresha mikakati na mbinu mwafaka zinazoweza kustawisha na kuimarisha hali ya ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na masomo mengine kwa jumla.

#### **1.9.7 Hitimisho**

Sura hii ikiwa sura tangulizi, imetoa maelezo ya kimsingi kuhusu mada ya utafiti kwa ujumla. Imeangazia na kupambanua dhamira na swala la utafiti, maswali yanayoongoza utafiti, nadharia tete pamoja na mbinu za utafiti. Ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data umeelezwa. Nadharia ya Uchanganuzi Linganishi ndiyo iliyoongoza shughuli ya utafiti ili kubainisha athari ya elimu ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

## **SURA YA PILI**

### **ELIMU YA DUKSI**

#### **2.0 Utangulizi**

Katika sura hii tumeshughulikia elimu ya Dukxi. Tumeelezea maana ya neno Dukxi ambapo tumebainisha mahusiko ya elimu ya Dukxi kando na kueleza asili yake. Aidha utaratibu wa elimu hii umeangaziwa. Lugha ya kufunzia pamoja na vipengele vya kisarufi vimefafanuliwa. Ili kubainisha elimu ya Dukxi, tumeangalia vijenzi vifuatavyo:

- Kijielezi na maana ya Dukxi
- Mafunzo katika chuo cha Dukxi
- Utaratibu wa elimu ya Dukxi
- Nafasi na dhima ya elimu ya Dukxi

#### **2.1.0 Kijielezi na Maana ya Dukxi**

Neno Dukxi limefasiriwa kwa njia mbili:

- Elimu ya Dukxi inapatikana katika eneo la Kaskazini Mashariki miongoni mwa maeneo mengine kama vile Pwani (Mombasa na Malindi). Jamii zinazoishi katika sehemu hizo ni jamii hamaji kama vile Wasamburu, Wasomali, Waborana, Warendille, Wagalla na Wamalakote. Ni muhimu kutambua kuwa wanajamii hawa hushinda wakihamahama kwa sababu ya kutafuta maji na lishe la mifugo. Hata wanapohama, wazazi huhakikisha kuwa maalim wanaendelea kuwapa watoto mafunzo ya Dukxi. Hali hiyo imetokana

na nafasi ya kipekee ambayo wameyapa mafunzo ya Duksi. Katika lugha ya Kisomali, neno Duksi lina maana ya chuo cha mafunzo ya kimsingi ya kidini ya Kiislamu. Kwa mujibu wa wanajamii wanaoitumia Korani wamelipa neno Duksi fasiri mbili:

- Elimu ya lazima katika jamii husika. Mtoto anapozaliwa huanza kufunzwa. Muradi tu aanze kujua kuongea, wao huanza kumfunza. Mafunzo hayo hutolewa pekee kabla ya watoto kujiunga na shule za msingi, yaani lazima wahitimu katika mafunzo ya Duksi. Elimu ya aina hii huitwa *Tahfidh*. Mafunzo hayo yamekusudiwa kutumiwa katika maisha ya kila siku na kuhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye. Pia watoto hufunzwa 'Hifadhi'. Katika hifadhi, wanafunzi hupewa uhuru wa kujifunza elimu ya kitaifa kando na elimu ya kidini. Wanaweza kuanza na elimu ya Duksi asubuhi kisha wakaenda kwa shule ya msingi. Hivyo basi mafunzo yote huendeshwa sambamba.

Kama ambavyo tumeshaona, Duksi ni neno la Kisomali lenye maana mbili. Neno hilo zamani lilitumiwa kumaanisha kivuli ambacho kingeweza kuwa cha mti au jengo. Kivuli hicho kilikuwa kinatumiwa kwa kufunzia watoto elimu ya dini ya Kiislamu na ndiposa hayo mafunzo ya Duksi yakaishilia kuitwa Duksi. Kwa hivyo leo hii, neno hilo linatumiwa kumaanisha masomo ya kimsingi ya kidini ya Kiislamu.

### 2.1.1 Utaratibu wa Elimu ya Duksi

Elimu ya Duksi hutolewa mahali popote, wakati wowote na mtu yeyote muradi awe amejifunza na kuishika dini kiasi cha kuweza kuikariri Korani inavyostahiki. Mahali hapo panaweza kuwa chini ya mti, katika veranda, darasani au nyumbani. Anayeendesha mafunzo ya Duksi huitwa maalim au Sheikh. Aghalabu walimu wa Duksi huwa wanaume. Hata hivyo wanawake pia wanaruhusiwa kuyaendesha mafunzo ya Duksi. Wanawake huwafunza watoto na hata wavulana wa umri chini ya miaka kumi na nne (14) mbali na wanawake wenzao. Vile vile vijana wanaonyesha umahiri katika kuishika na kuikariri Korani mapema hupewa nafasi ya kuwafunza watoto na vijana wenzao. Vijana hao huitwa *Kabiir* na wanaheshimiwa sana katika jamii husika kuliko wazee ambao hawajui Korani.

Mafunzo ya Duksi ni ya lazima katika jamii ya Kiislamu. Mtoto anapoanza kuongea anapaswa kujiunga na chuo cha mafunzo ili aweze kuwekewa msingi dhabiti wa maisha. Mtu ambaye hajakata mafunzo hayo hudharauliwa sana na wanajamii walioyapata mafunzo hayo. Asilimia kubwa ya wanajamii hujikakamua na wakahitimu. Wengi wao humwona mtu ambaye hajahitimu kuwa kafiri kwani wanaamini kuwa mwacha mila ni mtumwa. Huwa anaonekana na hata huchukuliwa kama kiumbe duni; mtu asiyeaminika. Kutokana na imani ya wanajamii, kila mtu hujibidiisha kuyapata hayo mafunzo na baadaye huhakikisha wanawe pia wanayapata masomo yayo hayo.

Kwa hivyo mafunzo ya Duksi hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mafunzo haya hupewa nafasi ya kikati katika jamii husika. Kila mwanajamii anastahili kuyagharamia mafunzo hayo. Walimu huajiriwa kuyaendesha mafunzo hayo kwa viwango mbalimbali. Familia au mzazi anaweza kumlipa maalim ili mtoto wake aweze kufunzwa pekee. Wazazi wanaweza kuwalipa maalim ili watoto wafunzwe katika kikundi. Familia au wazazi wengine wanaweza pia kuchagua nyumba ambayo mafunzo yanaweza kuendeshwa huku wao wakimlipa maalim kama kundi. Katika kiwango cha jamii, wazee hujitolea kuyagharamia mafunzo. Watoto wengi hukusanywa kati ya arobaini na mia wakafunzwa kwa pamoja kutoka msikitini.

Jamii husika ya Kiislamu katika mkoa wa Kaskazini Mashariki, imeweka mikakati maalum kuhakikisha kuwa kila mtu anaweze kuipata elimu hii kwa namna moja au nyingine. Kutokana na mipango mbalimbali inayolenga kuwawezesha kuwa takribani kila mtu kuyapata mafunzo hayo ya Duksi, asilimia ndogo sana huenda ikakosa kuipata elimu hiyo ujanani. Wanaokosa kujipatia elimu hiyo wakiwa na umri mdogo, wako na uhuru wa kujiunga na chuo cha Duksi baadaye kusudi wajifunze na kuelewa namna ya kuinukuu Korani wanaposwali na kuomba. Kwa hivyo si ajabu kuwaona watu wazima wakihudhuria darasa la Duksi kusudi wajifunze wasiyoyajua na kujikumbusha waliyoyasahau.

Kukiurejelea mji wa Garissa, tarafa ya kati kwa mfano, jamii zinazoishi pale ni kama vile Wasomali, Waborana, Wagalla, Wamalakote na asilimia ndogo ni mseto wa Waluhya, Wakikuyu, Wakamba, Wajaluo na wengineo. Tunapongea juu ya wanajamii wa dini ya Kiislamu, wote waliosilimu hujumuishwa wakajifunza Duksi. Kenneth (1991), anashadidia maoni hayo kwa kusema:

“Mafunzo ya Kiislam yamefaulu kuwabadilisha watu kutoka asili mbalimbali na kuwafanya kuwa kundi moja. Hivyo basi jamii isiyobadilika kwani daima waumini huyashikilia mafunzo yao”.

Kuhusu gharama ya masomo ya kimsingi ya kidini, kuna viwango mbalimbali vya malipo kutegemea mpango ambao umewekwa na kutumika. Kawaida malipo hutolewa Alhamisi. Katika eneo husika, kuna Duksi katika kiwango cha nyumba, familia na jamii.

Baada ya Duksi, wanafunzi wanaweza kujiunga na kiwango cha madrassa kisha baadaye shule ya upili na hatimaye vyuo vya kati au vikuu kama vinavyopatikana Pumwani, Thika na Pwani. Nchini Kenya takribani kila eneo lenye Waislamu lina elimu ya kimsingi (Duksi) ijapokuwa kwa majina tofauti tofauti kama vile chuo na madrassa. Vile vile baada ya shule ya upili, wanafunzi wanaweza kuyaendeleza mafunzo yao ya kidini nje ya nchi kwa mfano huko Saudi Arabia ambapo kuna vyuo vingi vya kidini ya Kiislamu.

Kwa hivyo elimu ya Duksi ni elimu ya kimsingi inayotangulia madrassa. Watoto wanapohitimu kutoka kiwango cha chini, wanaweza kujiunga na kiwango cha juu ambacho ni madrassa. Uhusiano uliopo kati ya madrassa na Duksi ni kuwa vyuo vyote vinavyoshughulikia ufunzaji na ujifunzaji wa masuala ya kidini kutegemea umri na eneo. Kama hali ilivyo katika madrassa, katika Duksi huwatarisha watoto kwa mafunzo ya juu na ya kina katika kuwawekea watoto msingi wa kidini, walimu wa Duksi huongozwa na silabasi kufunza juu ya mambo ambayo baadaye hufunzwa kwa kina katika kiwango cha madrassa.

Madrassa ni chuo cha kiwango cha juu kinachoendesha masomo mbalimbali kando na somo la kidini. Mfumo huu wa madrassa huzingatia lugha ya Kiarabu kwani ndiyo lugha ya kufunzia. Kwa upande mwingine Duksi ni elimu ya kidini ya kimsingi lakini mafunzo yanaweza kupambanuliwa kwa lugha zinazopatikana katika eneo husika. Kwa hivyo Madrassa ni aina ya shule ya kiwango cha juu inayotoa masomo tofauti tofauti. Shuleni humo, wanafunzi huimarishwa zaidi kwa masomo ya juu kulingana na umri, uwezo na bidii. Chuoni kuna ratiba ya masomo mengi inayoakisi viwango vya wanafunzi. Maudhui ya mafunzo hayo yanahusu dini na maisha kwa jumla hususan namna ya kuishi na kuweza kuukariri msahafu wakati wa kuswali.

## **2.2.0 Nafasi na Dhima ya Elimu ya Duksi**

Lengo la mafunzo hayo ni kutaka kuwawekea watoto msingi dhabiti wa kidini hususan

katika kukariri Korani. Tangu utotoni mwao watoto husaidiwa kutambua namna ya kuhusiana na Muumba wao. Njia ya pekee inayotumiwa kuwafanya watoto wakumbuke wanayofunzwa ni kukariri kwa sauti kubwa mara kwa mara. Watoto hupewa maandalizi juu ya maisha ya kila siku na hata baada ya uhai yaani siku ya mwisho duniani.

Elimu ya Duksi ni ya kimsingi katika maisha kwani wanajamii husika wanaamini kuwa kujua Mungu na mambo ya dini lazima yapewe kipaumbele. Inachukuliwa kuwa hakuna kitu kingine maishani kilicho cha muhimu kuliko kujua dini na ndiposa wanajamii wakashikilia kuwa “maisha ni dini na dini ni maisha”. Wanaiheshimu na kuienzi imani yao. Mafunzo hayo huwakumbusha juu ya matendo na mambo waliyoyatenda mitume na manabii (walikuwa ishirini na tano) kuanzia mtume wa kwanza Adamu hadi Mtume wa mwisho Mohammed. Mafunzo juu ya Mtume Mohammed huitwa Sunnah. Kwa mujibu wa AL Muntakhab, sura Tun nur, 56. Waumini wanaamriwa kushika sala, kutoa Zaka na kutii Mtume ili wapate kurehemewa.

Tukimnukuu mmoja wa wafuasi, Bahola anasema;

“Elimu ya Duksi ndiyo inayoendesha chembe chembe za damu mwilini, bila dini hakuna maisha.”

Kulingana na wanajamii, Duksi ni kweli tupu. Mambo ya ahera kama yalivyoelezewa kwa maoni ya manabii kama Musa, Issa, Yusuf, Yunus, Suleimani, Yakub, Idrisi, Nuh na Yahya hupambanuliwa. Watoto hufunzwa juu ya hao mitume kwani mitume ishirini na tano (25) waliaminiwa kuwa vielelezo bora. Waliishi na kutenda yote kulingana na

mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Kutokana na mafunzo ya hadithi, inatarajiwa kuwa watoto wanaweza kupata kujua jinsi Mungu anavyowataka waishi (kulingana na mafunzo ya *sira*). Kuna aina za hadithi kama *salih* (zilizosimuliwa vizuri) na *Hasan* (masimulizi ya *wastan*). Hivyo basi watoto wanaweza kuishi kistaarabu kama inavyotakikana wakiwa wenye nidhamu na tabia nzuri. Ili kuyafikia hayo malengo makuu, elimu ya Duksi imetoa silabasi na mtaala maalum wa kufuatwa na maalim wanapoanza hadi kuhitimu kwa wanafunzi.

### 2.2.1 Masoma katika Chuo cha Duksi

Katika chuo cha Duksi kuna masoma anuwai. Maalimu huwa wanaongozwa na ratiba ya kazi inayoonyesha jinsi mafunzo yanavyofuatana. Mafunzo hupangwa kuanzia mepesi na kumalizikia yanapoonekana mazito. Masomo ambayo yametengewa muda maalum katika ratiba ni kama yafuatayo:

- (a). Lugha
- (b). Hati
- (c). Matamshi
- (d). Maadili
- (e). Hesabu
- (f). Dini/utamaduni.
- (g). Kuomba na kuswali

Kila mojawapo ya masomo hayo yameshughulikiwa katika sehemu ifuatayo:

### **2.2.2 Somo la Lugha**

Kwa mujibu wa Ahmed (1993), Kiarabu ni lugha ambayo asili yake ni bara la Asia, kuanzia kaskazini mwa Syria na kuendelea hadi mashariki mwa AL Furat. Ni lugha inayotumiwa sana na jamii ya Kisemitiki. Lugha hii ndiyo ya kufunzia somo la lugha pamoja na masomo mengine katika Duksi. Katika jamii husika inaaminika kuwa lugha inayotambuliwa na hata itakayotumiwa siku ya kiamani Kiarabu. Hivyo basi, kila mtoto anatakiwa kuijua. Watoto wanapoanza kusoma, hufunzwa lugha ya Kiarabu kwa njia ya kukariri. Hufunzwa pia namna ya kutoa matamshi sahihi. Kukosea katika kutamka kunaweza kupotosha maana asilia. Watoto hufunzwa vile vile namna ya kuandika herufi za lugha ya Kiarabu. Hatimaye, watoto hufunzwa kuisoma na kuikariri Korani, kuomba na kuswali.

### **2.2.3 Somo la Hati**

Kama vile masomo mengine hutiliwa mkazo, somo la lugha hushirikisha kipengele cha hati. Tangu siku ya kwanza maalim huwaonyesha watoto umuhimu wa kuandika vizuri. Maalim huwaelekeza kama vielelezo bara. Hujitahidi kuandika kwa njia inayopendeza na kusomeka kwa urahisi. Pia wakati maalum hutengewa kipindi cha kuandika. Watoto huonyeshwa jinsi ya kuandika hati nzuri.

Maandishi yanaweza kuandikwa kwa njia mbili yaani kuandika herufi moja moja au

herufi zishikane.

Maendelezo yafuatayo yametoka kulia yakaelekea kushoto.

Tawihud-

Al-Ikhlās

Ayatil-Kursi

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ  
الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي  
أَمَّا اللَّهُ فِي مَنَاصِفِ  
وَأَيَّكَانِ أَبُودُ  
وَأَيَّكَانِ أَيْتَالِ  
مُوسْتَايِمِ  
الْأَسْتِرَالِيهِ  
الْيِيهِيمِ وَيِرِيلِ  
مَأَكْتُوبِي سِيرَاتَالِ  
لَادِهِينَا  
وَلَدَالِ لِينِ

#### 2.2.4 Maendelezo ya Kiarabu

Neno kitabu linaweza kuendelezwa kwa njia mbili tofauti nazo ni :

B T K AU

ب ت ك

ب ر ك

Kutokana na kielelezo hicho imebainika kuwa katika kuyaendeleza maneno ya Kiarabu, maandishi hutoka mkono wa kulia yakieleleka mkono wa kushoto. Hati hiyo inayotumiwa

inaitwa hati ya Kiarabu. Hati hiyo hutofautiana na hati ya Kirumi ambayo huanzia kwa mkono wa kushoto na kuendelea hadi mkono wa kulia. Maneno mengi ya Kiarabu hayamaliziki kwa irabu. Aidha lugha hii haina irabu e na o. Irabu hizo hutofautishwa kwa kuongezewa alama juu yake au chini yake. Alama hizo zinajulikana kama: *dhumma*, *fatha*, *kazra* na *sakna* kama ilivyoonyeshwa hapo nyuma. Alama hizo huwasaidia watoto kusoma herufi kama maneno. Bila hizo alama wanafunzi hawawezi kusoma maneno. Badala ya kusoma maneno wao huenda wakasoma herufi zikiwa zimejisimamia moja moja.

Baadhi ya mifano ni kama ifuatayo:

Athari ya Duksi	Kiswahili Sanifu
Kitaab	Kitabu
Kheri	Heri
Shariah	Sheria
Imlaa	Imla
Hisab	Hesabu
Sheitan	Shetani
Inshaa	Insha
Dastur	Desturi
Athar	Athari
Kiyama	Kiama

### 1.1 Kielelezo cha Athari ya Duksi.

Mifano iliyotolewa hapo juu imeonyesha makosa ya kisarafu. Kuna hali ya kuzidisha na

kupunguza herufi. Makosa hayo ya hijai yanaweza kutokea mwanzoni, katikati na hata mwishoni mwa maneno.

Kando na hayo maneno ambayo yametoholewa, kuna kule kubadilishabadilisha irabu mara watumie ‘a’ au ‘i’.

Hali hiyo imejidhihirisha katika mifano ifuatayo:

Maendelezo ya Kiarabu	Maendelezo ya Kiswahili Sanifu
Thalathin	Thelathini
Arubain	Arobaini
Ishirin	Ishirini
Hifdh	Hifadhi
Mukhutasar	Muhtasari
Ma’na	Maana
Quran	Koran
Ilhal	Ilhali
Maalim	Mwalimu
Kudur	Kudura

### 1.2 Kielelezo cha Mandelezo.

#### 2.2.5 Somo la Kidini

Katika mafunzo ya kidini, mambo mengi ya kiislamu huangaziwa. Kulingana na maoni ya AL Muntakhab sura ya 112- surat AL –Ikkhalas, watoto huwa wanafunzwa juu ya Mwenyezi Mungu ili waishi wakijua jinsi Muumba alivyo na nguvu, uwezo, mamlaka na

utukufu wa kipekee. Huonyeshwa kuwa hakuna kiumbe kingine chenye kuweza kulinganishwa na Allah. Maelezo hutolewa kwa kina ili watoto waelewe miujiza ambayo amefanya kuanzia kuumba dunia, mbingu na vyote vilivyomo. Majina tisini na tisa ya Mungu (*tawhid*) hufafanuliwa kwa mfano Rabana, Mola, Maulana na Allah. Majina hayo huonyesha sifa, uwezo ukuu na utukufu wake Mwenyezi Mungu

Watoto pia hufunzwa juu ya uhai, mauti na peponi. Kisha wakaelekezwa jinsi ya kuomba na kuepuka dhambi ili waweze kufika Ahera. Watoto hufunzwa Korani na kuelekezwa juu ya kuishi maisha ya Kiislamu yanayotilia maanani maadili. Huonyeshwa namna ya kuishi kama waislamu, kukaa kwa amani na upendo katika jamii na wengine. Mambo ya kusali, unadhifu na kuyahifadhi mazingira. Vile vile wanafunzwa juu ya wajibu na nidhamu ili waweze kuyaendesha maisha kwa njia ya kujitegemea, kujistahi na kujiheshimu. Tayebee aliyefasiri Korani, ametupa kielelezo mwafaka cha kutilia mkazo mafunzo hayo ya kidini. Picha zifuatazo zimeonyesha bayana hatua na maudhui katika *udhu*.

#### **2.2.6 Somo la Maadili**

Maadili Pia ni mada ambayo hushughulikiwa kwa marefu yake ili watoto waweze kujifunza kuwa na hulka njema (*akhlaq*). Baadhi ya tabia nzuri ni kama kusema ukweli, kutenda mema na ya haki. Uongo na haramu hulaaniwa sana. Watoto huonyeshwa jinsi ya kuabudu na kutangamana na wenzao inavyostahiki. Sheria na mambo ya mirathi

(*fiqhi*) hupambanuliwa kusudi kila mja apate kujua hukumu kulingana na imani ya jamii husika. Aisha (2000), analishadidia suala la maadili. Maoni yake ni kuwa matendo mema yanampendeza Muumba pamoja na binadamu.

### **2.2.7 Somo la Hesabu**

Somo la Hesabu huwa linatilia mkazo kukariri nambari kisha baadaye kuziandika. Mada zinazoshughulikiwa ni kama kuongeza, kuondoa, Aljebra na maumbo. Inaaminiwa kuwa mtu hawezi kuishi bila Hesabu kwani kila shughuli ya binadamu huhusisha kiasi fulani cha Hesabu. Wanajamii wanachukulia kuwa mazoezi ya Hesabu huwa yanasaidia ubongo wa mtoto kukua. Kule kufikiri mara kwa mara kunaaminiwa kuwa husaidia katika kupanua akili.

### **2.3.0 Mbinu za Kufunzia katika Chuo cha Duksi**

Mbinu ni njia anayoitumia maalim au Sheikh katika kuwasilisha habari ipasavyo. Njia huenda ikaathiri namna habari ilivyo. Jinsi inavyowasilishwa huenda ikaathiri mapokezi. Njia inayotumiwa inaweza kufanya hadhira ivutiwe na ipokee habari vizuri au ipokee lakini lengo likose kufikiwa. Kwa hivyo kwa jumla njia ni chombo ambacho kinaweza kusaidia au kuharibu habari kiasi cha kutofikia malengo na madhumuni lengwa kama ilivyokusudiwa. Katika kuwasilisha habari mbinu au njia maalum hutumiwa. Ule uratibu wa kupitisha habari ndio unaitwa njia au mbinu. Mbinu inaweza kuathiri ujumbe kiasi cha kutoeleweka au kueleweka vibaya iwapo njia mwafaka haikuteuliwa.

Katika ufunzaji wa elimu ya Duksi, maalim au sheikh hufuata ratiba ya kazi yake kulingana na uwezo wa mwanafunzi huku akizingatia silabasi na mtaala. Maalim hufunza wanafunzi wengi kutoka darasa au mahali pamoja lakini kila mmoja huwa anashughulikiwa kulingana na uwezo, maendeleo na mahitaji ya kiusomi. Darasa linaweza kuwa na watoto kama arobaini (40). Aghalabu maalim wawili huendesha darasa moja. Kila mmoja hudhibiti pembe au mstari wake. Maalim anayekaa nyuma ya darasa hupewa jukumu la kuchunguza namna wanafunzi wanavyoshiriki katika somo. Yeye huchunguza namna watoto wanavyoongea yaani vile midomo inavyotamka sauti. Sifa kuu inayobainisha darasa la Duksi kwa umbali ni kukariri kwa sauti. Wanafunzi huhimizwa kuimba, kuongea, kukariri na hata kujibu maswali kwa kutoa sauti kubwa.

Hatua ya kwanza huwa kujitolea kwa mwalimu. Yeye hujiona ni mfuasi anayeendeleza kazi aliyopewa na Mungu tena kazi yenye thawabu kubwa. Inaaminiwa kuwa baraka huhesabiwa na kuongezeka kutoka mtoto aliyefunzwa wa kwanza. Huwa anatoa huduma kwa moyo wa kujitolea kwani huamini anashiriki utukufu kwa kumfanyia Muumba wake kazi hiyo ya kuelekeza. Maalim au sheikh husalia mwalimu popote pale. Wanajamii huwaheshimu mno maalim. Kunapotokea sherehe kama harusi, maalim huandaliwa mlo maalum na kupewa mapema chakula bora kama nyama laini hususan maini. Wao hujitolea muhanga kuifanya kazi hiyo wakati wowote, asubuhi, aduhuri, jioni na hata usiku. Wao hulenga kutilia mkazo msingi wa dini. Huelezea asili ya Korani kuwa Mtume

Mohammed. Wao huandaa watoto ili wawe watu wanaomjua Mungu na dini yao kiasi cha kuwawezesha kuingia peponi (ahera). Huko Ahera wanaamini watatumia lugha ya Kiarabu wakati wa kujibu maswali. Hivyo basi hufunzwa juu ya maisha ya sasa na baada ya kifo au siku ya kiama.

Wanafunzi hufunzwa kujitegemea kuanzia pale wanapoanza kujifunza. Kila mtoto anapaswa ajitengenezee wino na kalamu yake. Wanafunzi huelekezwa kutengeneza wino kutokana na makaa yaliyosagwa kutoka kwa mti maalum kwa jina *Marimari* kisha yakachanganywa na maji au maziwapamoja na gundi. Kalamu huchongwa kutoka kwa kipande cha mti. Kila wanapomaliza kukariri, wanafunzi wenyewe hujitafutia maji ya kuosha ubao halafu wakaweka vifaa vyote vikiwa safi.

Ijapokuwa Wizara ya Elimu imepiga marufuku matumizi ya viboko shuleni, katika jamii husika viboko bado vinatumika. Watoto huchapwa vibaya kiasi cha kupata alama nyeusi miilini. Kuna viboko ambavyo huwa havivunjiki hata vikitumika. Inaaminika kuwa watoto wasipochapwa huenda wakaharibika na kupotoka. Kiboko kinaaminika kwa kuwadhibiti watoto kando na kuwatia adabu kusudi wawe na nidhamu. Wanapochapwa wengi huogopa wakawacha mabaya, utundu na utukutu; wakatulia na kuwa makini huku wakionyesha jitihada ya kushika yote wanayofunzwa.

Aghalabu darasani au chuoni huwa walimu wawili wanaoendesha mafunzo hayo ya

Duksi. Walimu hao huwafunza watoto kwa utaratibu maalum huku wakisisitiza ukariri wala si maana. Mwalimu mmoja anaweza kuendesha somo la kuandika kisha mwingine akafunza namna ya kukariri. Iwapo mwalimu mmoja hayupo, masomo huweza kuendelea kwani watoto huwa wameshawazoea walimu wote wawili.

Maalim hulenga kuwapa watoto maarifa na ujuzi fulani mbali na kujenga mielekeo inayotakikana katika jamii. Masuala mbalimbali hushughulikiwa kama vile usawa, imani, adabu na jinsi ya kuishi katika jamii. Katika msikiti kwa mfano, Maalim na wanafunzi wote huwa wanakaa chini kwa sababu wametambua na kuamini kuwa watu wote ni viumbe sawa mbele ya Mungu.

Maalim huongozwa na mpangilio mahsusi wa mada katika Silabasi. Mafunzo yote hupangwa ili kumwelekeza maalim wakati wa kufunza. Hali hiyo ya kumwelekeza maalim humwezesha kuwasomesha watoto taratibu, hatua kwa hatua. Madhumuni ya mwalimu huwa kuwapa wanafunzi msingi bora wa maisha. Kila mara walimu hukuambia kuwaandaa watoto kwa maisha ya sasa na ya baadaye. Pia huwawekea msingi dhabiti kwa masomo yao ya baadaye.

Kuhusu mafunzo juu ya Korani, mbinu mbalimbali hutumiwa kama maswali, majibu, kukariri, kutamka, utambuzi, masimulizi, uimbaji, kuandika na shughuli nyinginezo. Stadi zote nne (4) za lugha ambazo ni Kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika huangaliwa katika viwango mbalimbali. Kwa vile inafuata kuwa ili mtu aweze kuandika

lazima aanze kwa stadi nyepesi ya kusikiliza kisha kuongea na baadaye kusoma na kuandika. Maalim hufanya hivyo kwa kuzingatia masuala yafuatayo:

- Uteuzi na kukanusha matukio
- Ubingwa wa kusimulia hadithi kama za *Mtume Issa* na wasomi wa kale (kama vile, *Nabawi* na *Qudsi*) na masimulizi mengine juu ya wasomi wa Kiislamu (*al-Ghazali, Sunna, Hassan al-Banna*)
- Kueleza sifa za Mohammed na wasomi wa kale
- Matumizi ya vitu halisi ambavyo vinaweza kuonekana au kushikika.

#### 2.4.0 Hitimisho

Kwa muhtasari, katika sura hii ya pili, tumeshughulikia elimu ya Duksi. Maelezo yametolewa juu ya asili na maana ya neno Duksi. Ufafanuzi umetolewa kuhusu walimu ambao huwa wanashirikiana katika kuyaendesha mafunzo tofauti tofauti. Masuala yanayoshughulikiwa katika Duksi kama vile kukariri Korani na kuwa mwadilifu yameangaziwa. Katika kutamatisha, mbinu za kufunzia katika chuo cha Duksi zimebainishwa ipasavyo. Kwa jumla imedhihirika kuwa mafunzo hayo ya Duksi yamekuwapo na yataendelea kuwepo kwani ni mafunzo ya kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Elimu ya Duksi ni mfumo maalum ambao una silabasi ya kufuatwa. Shughuli inayotiliwa mkazo ni kukariri wala si maana na matumizi. Asilimia kubwa ya wanajamii wanaithamini na kuenzi. Mafunzo hayo yamepewa nafasi ya kikati katika jamii husika.

## SURA YA TATU LUGHA YA KISWAHILI NA YA KIARABU

### 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumeshughulikia elimu ya Duksi. Tumeangazia maana, utaratibu, lugha na mbinu za kufunzia kando na dhima ya elimu ya Duksi. Tumeweza kukubainisha kuwa neno Duksi linaweza kutumiwa kumaanisha mahali panapotumiwa kwa kuendeleza mafunzo ya kidini au kurejelea mafunzo ya kidini ya kimsingi. Chuo hicho kinaweza, kuwa katika jengo, veranda au kivuli cha miti. Habari zote za kufunzwa huwa ziko kwa lugha ya Kiarabu. Mara kwa mara Maalim huchanganya ndimi kutegemea mazingira. Katika eneo husika, lugha ya Kisomali na Kiswahili hutumiwa katika kufafanua dhana. Ijapokuwa imedhihirika kwa kiasi kuwa kuna uwiano kati ya vipengele vya lugha ya Kiarabu na Kiswahili, bado kuna haja ya kuchunguza tofauti hususan katika msamiati, maendelezo, mtindo wa kuandika, mpangilio wa maneno na mbinu za kufunzia.

Kwa hivyo sura hii imekusudia kudhihirisha vipengele vya sarufi ya Kiswahili na ya Kiarabu kwa madhumuni ya kuvilinganisha na kuvilinganua. Shughuli hiyo imelenga kubainisha uwiano na tofauti kati ya lugha husika. Mtafiti amevishughulikia vipengele vya lugha zote mbili katika viwango vya abjadi, fonimu, mtindo wa kuandika, maendelezo, msamiati na mbinu za kufunzia lugha ya Kiswahili na ya Kiarabu.

### **3.1.0 Lugha ya Pili, Kiswahili**

Kulingana na sera ya Wizara ya Elimu, Kiswahili ni somo la lazima katika shule za msingi na za upili. Vile vile mjini, lugha ya Kiswahili imechukuliwa kuwa lugha ya kwanza kwani watu wa jamii tofauti huishi pamoja huku watoto wao wakitumia Kiswahili kama lugha yao ya Kwanza. Kwa upande mwingine, eneo la mashambani lugha za kiasili ndizo hutumika kutoka shule za chekechea hadi darasa la tatu.

Kihalisia, jamii ambayo imechunguzwa ina ulumbi hivi kwamba kuna matumizi ya lugha nne. Hata hivyo imechukuliwa kuwa lugha ya pili ni Kiswahili nazo lugha zile zingine ni Kisomali, Kiarabu na Kiingereza. Lugha ya Kiswahili imechukuliwa kuwa lugha ya pili kwani kiisimu, lugha yoyote ambayo mtu hujifunza baada ya lugha yake ya kwanza huchukuliwa kuwa lugha ya pili. Kwa mujibu wa ripoti ya Mackay (1981), mfumo wa 8-4-4 ulianzishwa 1985, lugha ya Kiswahili ikafanywa somo la lazima kuanzia shule za Chekechea na kuendelea hadi vyuo vikuu.

### **3.1.2 Abjadi za Kiswahili**

Abjadi ni herufi za lugha ambazo huwa Irabu na konsonanti. Irabu pia hujulikana kama vokali. Lugha yoyote ile huwa na idadi maalum ya abjadi. Kwa mfano lugha ya Kiingereza ina abjadi ishirini na nne (24) ilhali lugha ya Kiswahili ina abjadi thelathini (30): vokali tano (5) na konsonanti ishirini na tano (25).

Mbaabu (1996), amezidhihirisha vokali hizo kama : a , e , i , o , u ilhali konsonanti nazo ni:b, c , d , f , g , h , j , k , l , m , n , p , r , s , t , v , w , y na z.

Katika kufundisha abjadi hizi pia huendelezwa katika hali ya ukubwa:

A B C D E F G H I J K L M N O P R S T U V W Y Z. Jedwali lifuatalo

limeonyesha tofauti kati ya maendelezo ya herufi ndogo na herufi kubwa:

Herufi kubwa	Herufi ndogo
A	a
B	b
C	c
D	d
E	e
F	f
G	g
H	h
I	i
J	j
K	k
L	l
M	m
N	n
O	o
P	p
R	r
S	s
T	t
U	u
V	v
W	w
Y	y
Z	z

### 1.3 Kielelezo cha Abjadi.

Vile vile abjadi huungana kuunda sauti ambatani au changamano zinazotamkwa kama abjadi moja nazo ni:

*Ch, dh, gh, nd, ny, ng, ng', nz, nj, mb, nch, njw, sh, sw, shw, kw, na th.*

Sauti hizo zikiunganishwa na irabu au konsonanti zinaunda maneno na vifungu virefu.

Baadhi ya mifano ni kama yafuatayo:

Sauti Ambatani	Mifano ya maneno
Ch	Chukua
Dh	Dhania
Gh	Ghadhabu
Nd	Tenda
Ny	Nyanya
Ng	Ngoja
Nz	Zinzia
Nj	Njia
Mb	Kimbia
Nch	Nchi
Njw	Mgonjwa
Sh	Shuka
Shw	Oshwa
Kw	Kwake
Th	Thawabu

#### 1.4 Kielelezo cha Sauti.

Sauti hizi hujitokeza mbele, katikati na hata mwishoni mwa maneno. Sauti hizo si fonimu halisi. Ni fonimu mbili zilizoshikanishwa na huathiriana. Kwa mfano konsonanti /m/ na/b/zote hutamkwa katika mazingira sawa (mdomoni). Vivyo hivyo, /n/ ambayo ni fonimu ya nasali ya ufizi huambatana na /d/ zote hutamkwa katika mazingira hayo ya

ufizi. Ndio maana nasali /n/ haiwezi kutangulia /b/ ambayo ni konsonanti ya midomoni. /Mw/hueleweka katika mkabala wa /m/ na /w/. Kwa hivyo ingawa sauti hizo zinatenda kazi kama fonimu, si fonimu halisi bali ni fonimu changamano.

### 3.1.3 Fonimu za Kiswahili

Kama lugha zingine zilivyo, lugha ya Kiswahili ina fonimu zake. Kwa mujibu wa Mgullu (1999), sifa za fonimu ni kama zifuatazo :

- Kila fonimu inazo sifa zake za kifonetiki zinazoweza kuelezwa ili kuifafanua fonimu hiyo
- Kila fonimu inazo sifa za kifonolojia ambazo huonyesha uamilifu wa fonimu hiyo katika lugha fulani. Watu wanaotumia lugha fulani huzielewa sifa zote za fonimu za lugha yao ikiwa ni sehemu ya umilisi wao wa lugha hiyo
- Kila fonimu hushiriki katika kulenga na kutofautisha maana katika maneno
- Fonimu moja peke yake haina maana yaani si kiashiria cha kiashiriwa chochote
- Fonimu ikibadilishwa katika neno, hilo neno linabadilika na maana kutoweka.
- Fonimu ikiongezwa katika neno lolote, maana ya neno hilo inabadilika au inapotea.
- Fonimu ikipunguzwa katika neno, maana ya neno hilo inabadilika au inapotea
- Mpangilio wa fonimu katika neno ukipanguliwa, maana ya neno hilo inabadilika au inapotea.

Kila lugha ina fonimu zake hivyo basi fonimu za lugha tofauti hazifanani katika uamilifu wao. Pia kuna alofoni. Hii ni sauti ambayo ni kipande kidogo kabisa kisichohusishwa na lugha yoyote. Hartman (1972), ameeleza alofoni kuwa ni sauti mojawapo miongoni mwa sauti kadhaa zinazowakilisha fonimu moja. Alofoni hutokea katika mazingira mahsusni.

Kulingana na Mgullu (1999), fasiri hizi zinaonyesha kwamba alofoni za fonimu moja huwa ni mambo mbalimbali au matamshi tofauti ya fonimu moja. Ingawa matamshi haya huwa yana tofauti ndogo au chache za kifonetiki lakini hayaleti tofauti yoyote katika maana za maneno. Aidha, ingawa sauti hizi ni tofauti lakini tofauti hiyo/hizo ni ndogo au chache sana. Mifano ifuatayo inaweza kudhihirisha tofauti hiyo:

/ e / konomikisi

/ i / konomikisi

/ ba / yolojia

/ bi / ayolojia

/ ji / ografia

/ jo / grafia

/ de / reva

/ d / reva

/ o / fisa

/ a / fisa

Kutokana na mifano hii, imebainika kuwa maneno mengi ni ya kuazimwa au ya kutoholewa. Aghalabu alofoni hutumiwa katika muktadha au mazingira ya kifonetiki yaliyo tofauti. Tofauti hizi huwa ni tofauti za kimazingira au kimuktadha tu. Hata hivyo wakati wa kutumia sauti hizi katika maneno sauti huweza kuathiriana na kupata sifa

mpya za kifonetiki. Haya huitwa mabadiliko ya kifonolojia.

Habwe na Karanja (2004), wanasema kwamba harakati zinazosababisha hali hii huitwa mifanyiko ya kifonolojia ambayo husababisha mabadiliko ya kifonolojia.

Baadhi ya fonimu hizo ni kama zifuatazo :

Fonimu	Mifano ya maneno
F	Faa
V	Vaa
S	Saa
Z	Zaa
P	Paa
B	Baa
K	Kaa
G	Gaa

### 1.5 Kielelezo cha Fonimu.

Kutokana na fonimu hizo, imebainika kuwa tukibadili fonimu ya kwanza tu, tunaishia kupata maneno tisa (9) ambayo ingawa ni ya Kiswahili yana maana tofauti kabisa.

- Faa - Kutosheleza / ridhisha
- Vaa - Kutia mavazi mwili au kwa chochote
- Saa - Kifaa cha kuonyesha wakati au muda
- Zaa - Kuleta kiumbe kipya katika dunia au kuendeleza uzazi
- Paa - Kwenda juu au kukwea
- Aina ya mnyama
- Sehemu ya juu ya jengo

Baa - Mahali pa starehe – kunywea pombe

Janga/tatizo/shida

Gaa - Kujishughulisha pwani

Kaa - Kuishi

Kuketi

Sehemu ya ukuni

Aina ya mnyama

Kwa hali kama hii tunaweza kusema kuwa foni ni ; (f) , (v) , (s) , (z) , (p) , (g) na (k).

Nazo fonimu ni /f/, /v/, /s/,/z/, /p/, /b/, /g/ na /k/ katika lugha ya Kiswahili kwa sababu ni bainifu, yaani zinao ule uwezo wa kutofautisha maana katika **maneno**.

Kwa jumla lugha ya Kiswahili ina:

- Fonimu za irabu
- Fonimu za nusu irabu
- Fonimu za konsonanti

Lugha ya Kiswahili inazo irabu tano tu kama ambavyo ilivyobainishwa hapo juu:

(a), (e), (i), (o) na (u) .

Herufi za Irabu hutamkwa kutegemea mambo yafuatayo:

- Mahali ulimi ulipo kinywani
- Mwinuko wa ulimi
- Jinsi mdomo unavyokaa

Wakati irabu inapotamkwa, ulimi unaweza kuwa umeinuliwa juu au upo katikati au upo chini kinywani. Midomo inaweza kuwa imeviringwa au imetandazwa irabu inapotamkwa kama ilivyootelezwa. Mahali pa kutamkia fonimu za Irabu zinaweza kuwa :

- Irabu za mbele ni /i/ na /e/
- Irabu za nyuma ni /u/ na /o/
- Irabu za kati ni /a/
- Irabu za juu ni /i/na/u /
- Irabu za nusu chini ni / e/ na /o/
- Irabu ya chini ni / a /
- Irabu za midomo mviringo ni / u / na / o / na
- Irabu za midomo mtandazo ni / i / na / e /.

Fonimu za nusu irabu katika Kiswahili ni mbili tu yaani /w/ na /j/. Mbaabu (1992), anaelezea kuwa herufi zinaitwa nusu irabu kwa sababu matamshi ya fonimu hizi yanakaribiana sana na matamshi ya irabu. Kwa mfano ukitumia /a/, /y/ na /w/ tofauti iliyoko ni ndogo sana.

### 3.1.4 Muundo wa Silabi

Kamusi ya TUKI (1984), inatoa kijielezi cha silabi kuwa tamko katika mfumo wa sauti ambalo huwa ni irabu au konsonanti na irabu.

Massamba na wenzake (2004), wanasema silabi ni kipashio cha fonolojia kinachohusu matamshi ambacho kwacho sauti za lugha hutamkwa kwa mara moja kama fungu moja linalojitegemea kimatamshi. Fungu hilo linaweza kuwa na sauti moja pekee, sauti mbili au hata zaidi kutegemea muundo wa lugha inayohusika.

Karanja na Habwe (2004), wanaeleza kuwa silabi ni kipashio cha utamkaji ambacho kwa kawaida ni kikubwa kuliko fonimu lakini kidogo kuliko neno. Kufikia hapo imebainika kuwa kila lugha ina utaratibu wake wa utamkaji na hilo tamko ndilo huitwa silabi. Alama \$\$ huwakilisha mipaka ya silabi. Tofauti hizi hutokana na wakaa (muda unaotumika katika utamkaji wa sauti ya lugha). Wakati mwingine, muda wa utamkaji wa silabi huathiriwa na mkazo unaofungamana nao. Wakaa huweza kutofautisha lugha za Kiromansi kama Kireno, Kiispaniola, Kiitaliano na kundi za lugha za Kijerumani.

Kulingana na Kihore na wenzake (2003), lugha ya Kiswahili ina silabi aina mbili; silabi huru na silabi funge. Silabi huru pia huitwa silabi wazi. Silabi huru inapatikana katika maneno asilia ya Kiswahili na huishia kwa irabu. Kwa mfano neno 'imba'. Silabi funge maneno yake huishia kwa konsonanti nayo ni ya kuazimwa kwa mfano neno rais. Katika silabi huru matamshi huendelea, hayakatiki ghafla kama hali ilivyo katika silabi funge.

Silabi yoyote ile huwa na sehemu tatu kama inavyoaminika na wanafonolojia wengi. Mgullu (1999), anataja sehemu ya kwanza, chanzo, ambayo huwa mwanzoni mwa silabi. Sehemu ya pili ni kilele au kiini cha silabi. Huwa katikati mwa silabi na ndiyo husikika

kwa nguvu. Lugha nyingi kama ilivyo Kiswahili huwa na irabu kama kiini cha silabi. Sehemu ya tatu ni mwisho wa silabi ambayo huwa mwishoni mwa silabi.

Lugha ya Kiswahili tofauti na lugha zingine haionyeshi kuwa na sehemu hizi moja kwa moja. Msingi wa muundo wa silabi za Kiswahili ni muundo wa silabi za Kibantu. Irabu zote tano hujitokeza kama silabi pekee au zikiambatana na konsonanti. Baadhi ya mifano ni kama ifuatayo :

<b>Silabi</b>	-	<b>Maneno</b>
\$a\$na\$a\$ndi\$ka\$	-	anaandika
\$e\$le\$ke\$a\$	-	elekea
\$o\$a\$a\$	-	oa
\$u\$a\$a\$	-	ua
\$kwe\$nda\$	-	kwenda
\$ng'o\$mbe\$	-	ng'ombe
\$nya\$nya\$	-	nyanya

Silabi zina umuhimu wake. Silabi ndiyo hubeba sifa mbalimbali za kiarudhi (sifa za kimuziki). Maneno ya lugha yoyote iwayo hutamkwa kwa kufuata utaratibu wa silabi. Nyimbo pia hutungwa na kuimbwa kufuatia utaratibu wa silabi. Silabi ni muhimu katika utunzi wa mashairi kwa sababu yanahitajika kuwa na urari wa vina na mizani ili yaimbikwe au yatongolewe. Mapigo mahsusi ya sauti yanazidisha mahadhi na mdundo. Silabi pia hurahisisha matamshi mbali na kuyaongoza matamshi hayo. Kando na hayo,

silabi huongoza maandishi kwani maandishi hutegemea matamshi ambayo hutegemea silabi zinazosikika. Matamshi yakiwa mabaya yanapotosha maana kwani maendelezo huathiriwa.

Kiimbo na mkazo ni sehemu muhimu vile vile katika mapigo ya sauti lugha. Hii ni kwa kuwa kupitia kwazo tunaweza kutofautisha maana mbalimbali ya maneno na hata sentensi. Lugha nyingi za Kiafrika kikiwemo Kiswahili kina kiimbo. Kiimbo ni utaratibu maalum wa kupanda na kushaka kwa mawimbi ya sauti. Dhana ya viimbo huambatana na dhana ya vidato au pichi yaani ruwaza kupanda juu, kuwa katikati au kwenda chini wakati wa usemaji. Kiimbo husaidia katika kubainisha lengo la tamko lililokusudiwa na mzungumzaji wa lugha husika. Inaweza kuwa amri, maelezo, swali, mshangao au nidaa kulingana na namna kiimbo kinavyobadilikabadilika. Basi kiimbo huweka wazi ujumbe kwa kuondoa utata ili maana lengwa ieleweke.

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (2004), maelezo kwa mfano hutofautiana kimaana mathalani kunaweza kuwa na maelezo ya kusimulia ya moja kwa moja, maelezo ya kuigiza, ya kuogofya na kushangaza, viimbo hivi hutofautiana kwa kiasi fulani.

### **3.1.5 Mtindo wa Kuandika**

Katika lugha ya Kiswahili, mtindo wa kuandika ni hati ya Kirumi inayotoka kushoto kuelekea kulia. Kuna abjadi, sauti, maneno, virai, aya na sentensi katika uandishi wa

kinadhari. Haya yote huungana yakajenga maandishi mengi ya kuunda makala, majarida, miswada, matini na vitabu. Vitabu vinaweza kuwa Hadithi fupi, Riwaya, Tamthlia au Diwani.

Katika ushairi kwa mfano, kuna pia silabi au mapigo yanayoungana na kuunda neno kisha maneno yakaunda kipande (ukwapi, utao na mwandamizi). Vipande hivyo vikiungana, vinaunda mishororo nayo mishororo inajenga ubeti. Beti zaidi ya mbili zinaweza kutengeneza shairi, wimbo au utenzi. Maandishi haya ya kishairi huwa ya kiufundi. Yanaweza kuimbwa kutongolewa, kukaririwa au kuandikwa. Mashairi yakiandikwa, yanaweza kutoa kitabu ambacho huitwa Diwani kwa mfano *Sauti ya Dhiki* kilichoandikwa na Abdlatif Abdalla kati ya vingine vingi.

### 3.1.6 Maendelezo na Hati

Uandishi wowote ule uwe wa kisanii au wa kawaida, huwa na utaratibu maalum. Kuna mfuatano wa konsonanti na irabu. Hata maneno ya kuazimwa yameswahilishwa.

Yameendelezwa kama maneno asilia ya Kiswahili kwa mfano:

*Dakitari, afisa, afisi, televisheni, eropleni na mengine mengi.*

Kutokana na mifano iliyotolewa hapo juu, imedhihirika kuwa kila baada ya konsonanti herufi ya irabu inafuatia. Ili habari yoyote iweze kusomeka katika lugha ya kawaida au ya kishairi, lazima sheria za kisarufi na kiarudhi zifuatwe. Alama za kuakifisha hutumiwa

inavyostahiki. La sivyo maana huenda ikapotoka. Kwa upande wa ushairi, kulingana na Amri Abedi, bila kufuata sheria za kutunga mashairi, mshairi atapotoka na kutunga mashairi guni ambayo hayawezi kuimbika.

Katika lugha ya kawaida inabidi mwandishi atambue na kuelewa mahali pa kutumia alama za uakifishaji kama :


*Kiulizi (?), nidaa (!), nukta (.), kikomo (,), dukuduku (.....),  
kistari (-) na zingine nyingi.*

Aya zinastahili kuwa za wastani, si ndefu sana wala si fupi sana. Kila aya inastahili kuelezea wazo moja. Inafaa kuwa na sentensi fupi fupi. Sentensi zinastahili kuanza kwa herufi kubwa na kutamatishwa kwa nukta. Kila sentensi inastahili kueleweka moja kwa moja bila kuzua utata.

Maandishi hayo yakiwa ya kawaida tu, mwandishi anaweza kupamba lugha kwa kutumia tamathali za lugha kama semi, nahau, methali, misemo, msamiati usio wa kawaida, tashbihi na mafumbo kwa lengo la kufanya lugha yake ivutie. Maandishi hayo yanaweza kutumika katika barua za kirafiki, visa na hata masimulizi.

Maandishi ya kirasmi kama barua rasmi, hotuba na kumbukumbu huwa na utaratibu maalum wa kufuatwa. Kila mojawapo wa kazi hizi ina umbo lake la kipekee. Mambo ya kuzingatiwa hapa ni mpangilio wa mawazo katika aya, utangulizi na tamati. Matumizi ya

herufi kubwa na ndogo, vitone na vistari hufaa kuangaliwa kwa makini. Kando na hayo kuna lugha rasmi inayozingatia sarufi wala hakuna kupiga chuku. Mambo halisi huwasilishwa namna yalivyo katika sentensi. Yanafuata utaratibu maalum ambapo kuna kuwa na mfuatano. Hutanguliza kinachotenda (nomino) kisha, kitenzi na mwisho kitendewa. Mfano wa sentensi ya Kiswahili ni kama ifuatayo:



Sentensi hiyo ikibadilishwa bila kuzingatia sheria za lugha husika, mpangilio mpya hautasomeka wala haitakuwa na maana kisarufi kwa mfano; Sana, analia mdogo mtoto.

Katika lugha ya Kiswahili hati inayotumika ni ya Kirumi. Maandishi hutoka kushoto na kuelekea kulia jinsi ambavyo haya yanavyoendelezwa.

### 3.1.7 Mbinu za kufunzia

Tunapoongea juu ya mbinu za kufunzia tunalenga utaratibu wa kuendeleza au kutoa mafunzo. Kunazo mbinu mbalimbali za kuendesha masomo. Mbinu hizo hutegemea umri wa mwanafunzi na kiwango cha elimu kwani huenda zikatofautiana kutoka kiwango kimoja hadi kingine. Huenda mbinu zinazotumiwa nyumbani zikatofautiana na zile zitakazotumiwa katika shule za msingi, upili na hata za chuo kikuu.

Kwa sababu ya kazi hii, tumejikita kwa mbinu za kufunzia lugha katika shule za msingi. Stadi zote nne (4) za lugha hushughulikiwa kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Kufikia hapo ni muhimu kuelewa malengo ya kitaifa ya elimu ya shule za msingi kwani ni kutokana nayo ndipo tunapata mwelekeo wa mada za kushughulikiwa. Baadhi ya malengo yaliyo na uhusiano wa moja kwa moja na somo la Kiswahili ni kama yalivyoorodheshwa kwa silabasi ya shule za msingi (2002):32

- Kukuza na kuendeleza umoja na uzalendo nchini ili wananchi waweze kuishi pamoja kwa amani
- Kuwaandaa vijana kwa majukumu ya baadaye
- Kuwawezesha wananchi kupata akili, maarifa na mielekeo ili aweze kushiriki katika ujenzi wa taifa (kiuchumi, kisiasa na kijamii)
- Kutambua na kukuza vipawa vya kila mtu ili kuwaendeleza watu binafsi
- Kukuza maadili ili watoto wakue na kuwa wacha Mungu, wenye nidhamu na wa kutegemewa
- Kukuza na kuendeleza hali ya utangamano na ujamaa
- Kuweza kuheshimu na kulinda tamaduni changamano nchini
- Kujenga hali ya kupendana, kujali na kukaa na majirani kwa amani ulimwenguni.
- Kuhakikisha mielekeo bora juu ya afya na kulinda mazingira.

Ili mwanafunzi ayafikie malengo hayo, lazima awekewe msingi imara mapema shuleni. Malengo hayo yamefasiriwa kiasi cha kuweza kuwasilishwa kwa wanafunzi kupitia kwa masomo na mada mbalimbali shuleni. Tukiangalia somo la Kiswahili, kupitia kwalo

wanafunzi wanaweza kupata uwezo wa kusoma na kuandika, kuhesabu, kubuni na kuwasiliana. Wanaweza kufurahia kusoma na kujenga hamu ya kutaka kuendelea kusoma. Kutokana na michezo na nyimbo zinazotumiwa humo shuleni, tamaduni changamano hushughulikiwa. Vipawa vya wanafunzi vinaweza kutambuliwa na kukuzwa mapema shuleni. Pia wanafunzi wanaanza kuelewa haja ya kukaa kwa amani na wenzao shuleni. Kupitia kwa nyimbo, masimulizi na mashairi, wanaweza kujifunza maadili na nidhamu

Katika kuyafikia malengo hayo, Wizara ya Elimu na Taasisi ya Elimu, imetoa mitaala na Silabasi ya kuwaongoza na kuwaelekeza walimu wanapofunza shuleni.

Kwa maoni ya Macaro (2005), pengo kati ya utafiti, sera na hali halisi katika maisha linaendelea kuwa changamoto linalostahili kushughulikiwa. Anasema kuwa kuna haja ya kuendelea kufanya utafiti ili kuimarisha ufunzaji ambao utarahisisha ujifunzaji na hata kuinua viwango vya elimu. Yanayostahili kushughulikiwa ni maandalizi na namna ya kuwasilisha habari.

Chambilecho Silabasi ya Taasisi ya Elimu (2002), somo la Kiswahili limepewa vipindi vitano (5) kila wiki kuanzia darasa la kwanza hadi la tatu. Vipindi saba vimetolewa kwa darasa la nne hadi nane. Kwa jumla madarasa ya chini yana vipindi thelathini (30) ilhali madarasa ya juu (5-8) dakika thelathini na tano (35). Kutokana na malengo makuu ya

kitaifa ya elimu, malengo ya shule za msingi yalifasiriwa. Kila darasa lina malengo maalum. Malengo ndiyo hubeba shabaha maalum. Kwa mfano darasa la tano (5) lina malengo yafuatayo:

Mwanafunzi aweze kuendelea;

- Kutambua na kutumia maamkuzi kwa njia inayofaa
- Kutambua na kuzingatia matamshi bora
- Kutunga na kutamka sentensi za kiwango chake
- Kuiga na kuigiza
- Kujieleza kwa njia inayoeleweka
- Kutumia vyombo vya habari katika kujipatia burudani na mafunzo ya kumwezesha kuwasiliana vyema na
- Kutambua na kutumia misemo na methali.
- Malengo hayo kwa jumla yanaweza kumsaidia mwalimu kupata mada na yaliyomo yaani mambo yanayofunzwa ili mwanafunzi aweze kuyafikia malengo mapana ambayo yamebainishwa. Baadhi ya mambo yanayoshughulikiwa katika kiwango hicho ni:

- Maamkuzi
- Sauti
- Sentensi
- Masimulizi
- Michezo katika mazingira ya mwanafunzi

- Mawasiliano kupitia vyombo kama runinga, redio, mtandao na magazeti.

Mwelekezi anaweza kumsaidia mwanafunzi kufikia malengo haya iwapo yeye mwenyewe atakuwa ameandaliwa vya kutosha katika Chuo cha ukufunzi. Inampasa afahamu umuhimu wa kuwa na maandalizi mapema kabla kutekeleza jukumu lake la kufunza.

Baada ya kuhitimu mwalimu anatarajiwa kuelewa kuwa wajibu wake ni kumwelekeza mwanafunzi kiasi cha kumwezesha kujua na kupata akili, maarifa na ujuzi. Macaro (2003), anapendekeza kuwa katika ufunzaji na ujifunzaji ni muhimu mahitaji ya mwalimu pamoja na ya mwanafunzi yashughulikiwe vilivyo kwani kila mmoja ana mahitaji ya kipekee yanayoweza kuathiri ufunzaji na ujifunzaji.

Mwalimu anaweza kutumia silabasi katika matayarisho yake ya kufunza na hata katika kutunga mitihani. Silabasi ni nyenzo muhimu katika kutengeneza ratiba ya kazi, mpangilio wa somo na mitihani kando na mijarabu. Katika kufanya hivyo, inawezekana kila kipindi kutengewa mbinu maalum kulingana na mada ya siku.

Tukiteua mada ya maamkuzi kwa mfano, kuna mbinu nyingi za kuendeleza somo hili.

Mwalimu anaweza kuchagua chombo cha mawasiliano kama redio.

Wanafunzi wanaweza kusikiliza maongezi yanavyoendeshwa kisha baadaye wakaulizwa kufafanua mambo muhimu yaliyojitokeza. Vile vile wanaweza kubainisha aina za salamu. Mwalimu anaweza kuwachagua wanafunzi waigize darasani. Wanaweza kuigiza nafasi na majukumu tofauti tofauti kama:

*Mgonjwa na tabibu, mwalimu na mwanafunzi, mashoga wawili, mfanyi biashara na mteja, abiria na utingo kati ya mifano mingine mingi.*

Katika kuhitimisha mwalimu anaweza kutilia mkazo ufafanuzi wa istilahi za salamu au maamkuzi. Hoja muhimu zinastahili kuandikwa ubaoni kwa mpango mzuri ili wanafunzi wapate fursa ya kujifunza namna ya kupanga kazi kwa unadhifu. Wanafunzi wanaweza kujifunza hijai na hati nzuri inayosomeka kutokana na kazi ya mwalimu. Mwalimu anastahili kuwa kielelezo bora. Marudio na mazoezi ya mara kwa mara huwawezesha wanafunzi kushika hoja.

Soómo linapoendelea, mwalimu anastahili kujibidiisha kuwashirikisha wanafunzi. Pia kuwatambua kwa kuwaita majina yao na kisha wanapotoa majibu kuwe na utambuzi, himizo au pongezi. Wakati mwingine mshindi atunukiwe kama njia ya kuwachochea wengine pia waamke na kutia bidii. Wanafunzi wanapopewa nafasi ya kujieleza mara kwa mara, wanapata ujasiri wa kujieleza bila uoga.

Kuhusu stadi ya kusoma, mwalimu anaweza kuteua makala yaliyosheheni mafunzo kama ya maadili, uzalendo au tamathali za lugha. Taarifa hiyo inaweza kusomwa kwa sauti na

mwalimu au wanafunzi huku wanafunzi wakizikinakili hoja muhimu daftarini. Kukiwa na vitanza ndimi kwa mfano, wanafunzi wanaweza kupewa fursa ya kuvisoma kwa sauti. Mifano ni kama:

- *Wanawali wa Liwali wala wali wa Liwali.*
- *Mchuzi ana ujuzi wa kuchuuza mchuzi.*
- *Baba abeba papa ijapokuwa anampelekea babake*

Wanafunzi wanaweza kupewa kazi za ziada ili watafiti juu ya vitanza ndimi zaidi kutoka kwa wanajamii, runinga (kipindi cha kukanganyana), redio na magazeti (Taifa) kisha kazi hiyo iwasilishwe darasani. Mwalimu anapaswa kujaza palipo na pengo kando na kurekebisha makosa. Kazi kama hii inaweza kunoa vipawa kama vya ubunifu licha ya kuwachangamsha wanafunzi.

Zoezi la imla hutolewa moja kwa moja. Wanafunzi wanaweza kusomewa sentensi kisha wakazinakili daftarini. Baada ya mwalimu kusahihisha zoezi la kukanusha linaweza kuendelea ambapo majibu yakaandikwa daftarini kisha yasomwe kwa sauti na baadaye kuandikwa na kutamkwa inavyostahiki.

Katika kusoma, wanafunzi wanatakiwa kukua watoto kama asemavyo Mheshimiwa Rais Kibaki. Watoto wanaweza kupewe mazingira na uhuru wa kuwawezesha kuwa watoto. Michezo mbalimbli inaweza kutumiwa ili wanafunzi wasome huku wanafurahia ujana wao. Michezo maarufu kama ile ya “*cha baba cha mama na nyama, nyama, nyama*”

inaweza kutumiwa. Mviringo duara huundwa kwa kushikana mikono nao wimbo ukaanzishwa na mmoja wa watoto. Anapoimba na kuongea lengo huwa kujaribu kukanganya ili wengine wapotoke. Anayeshindwa kufuata inavyostahiki huchekelewa kisha akalazimishwa kuingia ndani na kushika usukani wa kuwaongoza wengine. Wasio makini kwa kutambua majina ya wanyama au vyakula vinavyoliwa huku wanarukaruka, pia hunaswa wakaingia ndani ya mviringo.

Kando na kufurahia michezo wanafunzi hujifunza msamiati wa wanyama na wa vyakula. Vile vile somo hilo linaweza kuendelezwa darasani kwa kuwauliza watungie sentensi majina ya wanyama au waandike mtungo juu ya wanyama au vyakula.

Vyombo vya mawasiliano kama redio vinaweza kutumiwa kwa kufunza juu ya vitendawili, hadithi, mijadala, nyimbo na tamathali nyinginezo za lugha. Baada ya kusikiliza kipindi, maswali yanaweza kutolewa na wanafunzi wakajibu. Hatimaye mwalimu anaweza kujumuisha somo kwa kutoa muhtasari. Kanda za kunasia sauti pia hutumiwa kwa kuelimisha wanafunzi juu ya masuala ibuka kama vile Ukimwi, katiba, madawa ya kulevya, haki za watoto, ajira, ajali, njaa na uchaguzi kati ya mengine mengi.

Fanani huweza kualikwa shuleni akasimulia kisa, akatongoa shairi, akawafunza juu ya mazingira, ujana au jambo lolote linalowaathiri. Mtaalam au mgeni mwalikwa anaweza kutoa hotuba juu ya mada yoyote darasani. Vikundi vya wasanii vinaweza kutumiwa

kutoa mafunzo maalum kwa mfano, Tausi, wingu la moto, vitimbi na vioja mahakamani kati ya vingine vingi.

Mada zingine kama za uandishi wa insha zinahitaji maelezo yenye utaratibu maalum. Mwalimu anaweza kuanza kwa kutoa funzo juu ya uakifishaji. Viakifishi vyote vinaweza kutajwa kwa majina kisha vikiambatanishwa na alama yazo. Kila alama inafaa ielezwe kwa kina huku matumizi yakionyeshwa papo hapo. Baadaye aina mbalimbali za insha zinaweza kubainishwa huku umbo lake likielezwa kwa kina. Wakati mwingine sentensi zinaweza kutolewa na wanafunzi kuhusu mada fulani halafu wakazitumia katika kuandika insha yao.

Pia kutaja vidokezo nao wanafunzi wavitumie kwa kukamilisha uandishi wa insha. Mbinu hii inaweza kuimarisha na kukuza kipawa cha ubunifu. Insha bora inaweza kusomwa darasani mbali na mshindi kutambuliwa na kupewa tuzo. Kando na hayo insha hiyo bora huweza kuangikwa kwa kibao cha matangazo ili wanafunzi wengine waone na kujisomea. Matarajio ni kuwa jambo hili huweza kuwachochea wengi kufanya juhudi.

Kusoma maktabani pia ni njia nzuri ya kukamilisha somo. Kila mwanafunzi anaweza hupewa kazi ya kutafiti maktabani kisha wayawasilishe matokeo darasani huku wengine wakichangia chini ya uongozi wa mwalimu. Mwalimu hutengeneza darasa lake likawa ukuta zungumzi iwapo jitihada zitafanywa kupamba ukuta kwa habari, maandishi,

michoro na picha zilizo na mawazo ya kiusomi. Mojawapo wa kazi hizi inaweza kuwa maendelezo ya abjadi kwa herufi ndogo na kubwa.

Kupitia mchoro, wanafunzi huweza kujifunza msamiati kama sehemu za mwili hasa mchoro ukiambatanishwa na majina yake. Majina ya pembe nne (4) za dunia yanaweza kuonyeshwa kwa mchoro wa dira na mengine mengi yanaweza kuonyesha pia majina ya vitu mbalimbali kama; rangi, nyota, ajira na tarakimu. Kielelezo cha duka na kona ya mazingira huwekwa katika pembe ya darasa ili kuwasaidia wanafunzi. Wakati wa somo au wakati wa mapumziko huwa na vitu anuwai kama makartasi, mikebe, majani, pipi, sukari, matunda na sabuni. Mimea aina aina kama maembe, miwa, ndizi, nyanya, machungwa, mahindi na mawele huweza kukusanywa.

Wanafunzi huhusishwa katika kuweka unadhifu katika eneo hilo. Mwalimu hujibidiisha kuhakikisha anawavutia na kuwanasa wanafunzi wake darasani anapofunza kupitia kwa matumizi ya nyenzo tofauti tofauti kila wakati. Kila somo likiwa na nyenzo maalum wanafunzi hufurahia somo na hata kuwa na hamu ya kutaka kusoma kila wakati. Mada kama ya mapambo huweza kufana sana wanafunzi wakipewa jukumu la kuleta mapambo kama njunga, ushanga, herini, pete, bangili, vipuli na mkufu. Wakati wa somo hupewa nafasi wakavaa na kujitokeza mbele ya darasa.

Mada inayohusu mahali mahsusi kama bunge, mahakama, zaraa na sokoni kati ya

kwengine kwingi. Hali hiyo huwavutia na hata kuwafanya wanafunzi kueleweka zaidi wanapopelekwa kushuhudia shughuli husika badala ya kuelezwa juu yake.

Mwalimu huweka rekodi ya kila mwanafunzi ili iwapo atakwama asaidiwe. Huwa rahisi kutambua na kufuatilia maendeleo na bidii ya kila mwanafunzi kama rekodi ya kazi ya mwanafunzi inatumiwa na kuhifadhiwa vema. Mwalimu anapofunza huweka malengo ya kutekelezwa. Kupitia mpango kama huu, hakuna wakati utapotea bure.

Maongezi kati ya mwelekezi na mwanafunzi huwa muhimu. Huwa yanamwangazia mwanafunzi kiasi cha kutanabahi lengo la kufikiwa shuleni mbali na kuteua uwanja wa kazi baadaye maishani.

Mwalimu kama jina lake linavyosema, hakika vitendo vyake hutoa mafunzo hata bila yeye kufungua kinywa chake. Kuanzia namna anavyojibeba, mavazi na lugha yake inaweza kuathiri ujifunzaji wa wanafunzi. Mwalimu huwa kielelezo bora wakati wowote. Mbinu ya kushughulikia kila mwanafunzi kama mtu binafsi badala ya kufunza darasa, humsaidia katika ujifunzaji kwani mtazamo huu humwezesha mwalimu kumwandalia kila mmoja kazi ya ziada kulingana na mahitaji yake binafsi.

Macaro (2005), anajumuisha maoni hayo kwa kusema kuwa hakuna njia ya kipekee ya kufunzia lugha. Kila njia ina umuhimu katika ujifunzaji wake. Anasisitiza kuwa kuna

haja ya kuwa na maandalizi, kufuatilia na kuchunguza mwanafunzi anapoongea na anapoandika. Kazi iliyokamilika kama ya maandishi huenda isionyeshe palipo na kiini cha tatizo la mwanafunzi. Kwa hivyo wanafunzi wanastahili kuelezwa zaidi kuwa wao wanajifunza lugha ngeni. Kwa hivyo wawe huru kutafuta ushauri wanapoendelea kujifunza lugha. Walimu wanahimizwa kuwapa moyo wakati huo badala ya kutumia maneno yanayoweza kuwavunja moyo. Wanafunzi wakielewa kuwa wanao uwezo wa kujifunza na kudhibiti lugha, hili litakuwa jambo la kuwainua. Njia bunifu na maarifa yatumike katika kuwasilisha matokeo ya wanafunzi.

Matumizi ya maongezi katika ujifunzaji wa lugha ni mbinu nzuri pia. Mbinu hii huruhusu utangamano kati ya mwalimu na mwanafunzi hali inayoweza kwenda moja kwa moja na tathmini. Vikundi vya wawili au zaidi huweza kutumiwa katika kuhusisha darasa zima kwa mijadala.

Macaro (2005), anapinga njia za kulazimisha wanafunzi. Anasema kuwa kuna hatari walimu na walinda sera kulazimisha wanafunzi kwa njia fulani za kufunzia darasani (kutoka na silabasi na sera zisizo misingi ya kisayansi). Anapendekeza kuwa mwalimu awe akijiuliza, “ni nini nimewacha nje ya ufunzaji wangu ambacho kinaweza kutatiza ujifunzaji wa mwanafunzi”. Hali hii ya kuakisi inaweza kusaidia kupata kuelewa maendeleo yake.

Carl James (1980), anasema mwalimu mzuri lazima ashughulikie mielekeo akiwa anatathmini. Akifuutiliza anafaa ajiulize kwa nini wanafunzi hufanya makosa fulani. Ni kutokana na msingi huu ndipo mwalimu huenda akaandaa kazi ya ziada na kuwasaidia wanafunzi wenye udhaifu. Hata mwanafunzi anastahili kuelewa kwa nini amekosea ili asije kuyarudia makosa hayo tena.

### 3.2.0 Lugha ya Kiarabu

Katika kulishughulikia somo la lugha, elimu ya Duksi hujifunga katika lugha ya kufunzia masomo bila kujishughulisha na lugha ya Kiarabu kama inavyotumiwa na wanajamii wa huko Yemen, Saudia, Iran na Iraq. Hayo yametokana na imani kuwa ni muhimu kupokeza habari na lugha asilia mapema iwezekanavyo kwa watoto. Kwa hivyo hati na lugha ya kuendeleza mafunzo imesalia katika Kiarabu. Ijapokuwa somo ni la lugha, kulingana na Tayebjee mtaalam aliyefasiri Korani, watoto hufunzwa Kiarabu cha Korani ili waweze kuijua, kuisoma na kuikariri Korani wanapomba na kuswali.

Kufikia wakati wa utafiti hakukuwa na tafsiri nyingi za maandishi ya Korani. Hali hiyo imetokana na imani kuwa maneno yanayopatikana katika Korani yanayounda sura mia moja na kumi na nne (114) ni habari aliyopewa Mtume Mohammed moja kwa moja na Mwenyezi Mungu. Jitihada ya kutafsiri imehofiwa kuwa inaweza kupotosha maana lengwa aliyoiikusudia Mungu. Kwa hivyo hati na lugha ya kufunzia imesalia kuwa

Kiarabu.

Kama ambavyo tumepitia vipengele vya lugha ya Kiswahili, katika nafasi hii tumeangazia vipengele vya lugha ya Kiarabu. Katika somo la lugha, vipengele mbalimbali vya sarufi hutiliwa mkazo. Viwango hivyo ambavyo vimeshughulikiwa ni kama vifuatavyo:

- Abjadi
- Matamshi
- Maendelezo
- Msamiati
- Maandishi
- Mbinu za kufunzia

Tutavipitia viwango hivi kimoja baada ya kingine.

### 3.2.1 Abjadi za Lugha ya Kiarabu

Kwa sababu ya kutaka kuwawekea watoto msingi dhabiti na kuwapa uwezo wa kujua, kuisoma na kuikariri Korani, utaratibu maalum hutumiwa. Watoto hufunzwa hatua kwa hatua. Maalim huanza kwa matamshi. Katika matamshi abjadi za lugha hushughulikiwa nazo ni irabu na konsonanti. Majedwali yafuatayo yanaonyesha abjadi za lugha ya Kiarabu na pia abjadi zile ambazo hazipo katika lugha ya Kiarabu:

IRABU ZA KIARABU اي اي يو او

Irabu hizo zinaweza kutumiwa pamoja na konsonanti katika kuunda maneno mbali mbali kama yalivyoonyeshwa hapa chini.

Baadhi ya sehemu za mwili katika lugha ya Kiarabu ni kama zifuatazo:

**HERUFI                      HERUFI MOJA MOJA                      HERUFI ZIKISHIKANA**  
**ZA KISWAHILI**

Mkono	ح ق ن د	ايدى
Paja	ك ن ه ه	الرك
Mguu	ل ه ز	الساق
Meno	ت ه ت ح	الأسنان
Mdomo	ش م س ر ح	الفم
Kidole	ف ز اي ان اي بحث	إصبع

Kwa jumla, abjadi zinazotumika sana katika lugha ya Kiarabu ni zaidi ya thelathini (30).

**3.2.2 Kipengele cha Maendelezo**

Maendelezo katika lugha ya Kiarabu yanaweza kuendelezwa kwa njia mbili (2). Herufi zinaweza kushikana au kusimama wima. Wakati maneno yanaendelezwa yanaweza kutokea kama vile neno kitabu lilivyoendelezwa hapa chini. Neno kitabu linaweza kuendelezwa kwa njia mbili tofauti nazo ni:

B T K

بتك

Au

ب رك

### 3.2.3 Kipengele cha Msamiati

Watoto hufunzwa juu ya msamiati mbalimbali kusudi waweze kuelewa maana na namna ya kuyatumia maneno inavyostahiki. Kulingana na silabasi ya elimu ya Duksi, msamiati anuwai umetengewa muda. Matumizi ya msamiati hutegemea wakati, umri, mahali mahusiano na lengo. Katika elimu ya Duksi, watoto hufunzwa juu ya msamiati wa majina ya Mungu (99), wakati wa kuomba, jinsi ya kuswali, maadili, mahusiano, mazingira na maisha kwa jumla.

Katika mada ya msamiati watoto hufunzwa namna ya kutamka ambapo sauti yenye mdundo na mahadhi husisitizwa kwani kila neno lina matamshi yake sahihi. Kukosa kutoa matashi sahihi hupotosha maana. Na kwa sababu hiyo, watoto hukariri maneno mara kwa mara ili waweze kuyajua na kuyatofautisha wanapoyatumia kwa maandishi na maongo. Watoto pia huonyeshwa na kuelekezwa kuyaandika maneno kama

inavyostahiki. Baadhi ya msamiati ni kama ufuatao:

Maendelezo ya msamiati (Kiarabu)	Maendelezo ya msamiati (Kiswahili)
Amm	Amu
Khamsa	Hamsa
Khamsin	Hamsini
Rafī:q	Rafiki
Ya:qu:t	Yakuti
Ra:ha	Raha
Rahn	Rehani
Shayta:ni	Shetani
Qabi:l	Kabili
Hamm	Hamu

### 1.6 Kielelezo cha Maendelezo.

Kutokana na mifano ya hapo juu, imebainika kuwa kuna matumizi ya sauti /q/, alama (:), kurefusha na kufupisha maneno. Wakati mwingine, picha kama zinazofuatia hutumiwa. Maelezo juu ya jinsi ya kushiriki katika maombi yamefafanuliwa katika picha ifuatayo;

## SALA KWA UFUPI

8. Osha mkono wa kulia hadi kifundoni mara tatu (angalia Picha 7).

9. Osha mkono wa kushoto hadi kifundoni mara tatu.

10. Paka maji baadhi ya kichwa, na bora kichwa chote (angalia Picha 8, 9 na 10).

11. Osha masikio yote mawili nje na ndani kwa wakati mmoja kwa kutumia vidole gumba (kwa nje) na vidole vya shahada (kwa ndani) mara tatu (angalia Picha 11).

12. Osha mguu wa kulia mpaka kifundoni mara tatu.

13. Osha mguu wa kushoto mpaka kifundoni mara tatu (angalia Picha 12).

*Angalia.*—Pachua vidole vya miguu kwa kupitisha kidole kidogo cha mkono wa kushoto katika hivyo vidole vya miguu.)

14. Fuatisha utaratibu huu, kuanzia namba (1) mpaka namba (13). Kama huwezi kufanya yote, yaliyo lazima kufanya ni namba (1), (7), (9), (10), (12), (13) na (14)

اذان

### Adhan

Ni mwito wa kuwaita watu kwenda kusali. Adhan husikika mara tano kila siku kwa Salah za Faradhi:

### Salah كَيْفِيَّةُ الصَّلَاةِ

Nia

Tia nia moyoni mwako kuwa unakusudia kusali Salah ya: (1) Alfajiri; au (2) Adhuhuri; au (3) Alasiri; au (4) Magharibi; au (5) 'Ishaa. Wala hulazimiki kutamka hiyo nia kwa maneno:

Takbyratul-Ihram

اللَّهُ أَكْبَرُ

(Hii inaitwa Takbiratul-Ihram) huku umeinua mikono yako na vidole gumba viwe usawa wa masikio kisha, ikunje mikono yako na iweke juu ya kifua, wa kulia juu ya wa kushoto. Macho yako yangalie pahala pa kusujudu (angalia Picha 1 na 2). Soma moja kati ya Du'a za Al-Istiftah au Du'a Thana.

Du'a Al-Istiftah (Du'a za kuanzia Salah)

Ta'awwudh

Kisha sema kwa siri:

أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ

## Udhu

كَيْفِيَّةُ الوُضُوءِ

UDHU ni kuosha viungo kwa ajili ya Salah.

Jinsi ya kutawadha

Tayarisha maji tahiri ya kutosha kutawadha kisha:

1. Tia nia moyoni kuwa unakusudia kutawadha;

2. Sema: بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِیْمِ

3. Piga mswaki.

4. Osha vitanga vya mikono, vyote viwili kwa wakati mmoja mara tatu, na safisha baina ya vidole kwa kupitisha vidole vya mkono mmoja baina ya vidole vya mkono mwingine (angalia Picha 1).

5. Sikutua kinywa kizima mara tatu (angalia Picha 2).



Picha 1

Picha 2

Picha 3



Picha 4

Picha 5

Picha 6



Picha 7

Picha 8

Picha 9



Picha 10

Picha 11

Picha 12

6. Vuta maji puani na kuyatoa mara tatu (angalia Picha 3 na 4).

7. Osha uso wote toka sikio hadi sikio na toka maoto ya nywele hadi chini ya kidevu mara tatu (angalia Picha 5 na 6).

Imebainika kuwa katika kuomba lazima mja ajiweke safi kimwili na kiroho. Tukiangalia picha za mtafiti Tayebjee, tunatambua kuwa ametufafanulia kwa njia ya michoro hatua za kupitiwa wakati wa kwenda mbele za Muumba. Amefanya hivyo kwa kubainisha msamiati wa viungo mbalimbali vya mwili. Mchoro uliotangulia umedhihirisha mawazo hayo mawili (2). Kabla ya maombi, hatua maalum hupitiwa kama njia ya maandalizi. Picha imeonyesha hatua hizo na maelezo juu ya maombi.

Ameфанunua taratibu namna ya kuosha viungo mbali mbali vya mwili kama njia ya kujitayarisha kwa shughuli ya *udhu*. Ameonyesha njia ya kujiweka safi hata ndani ya moyo kabla ya kuomba. Viungo vyote vinaoshwa kama ambavyo vimeonyeshwa kwa picha huku mwombaji akiwa ameanza na moyo wake (kuamini na kukusudia) kuwa anataka kuelekeza dua yake kwa Maulana. Majina yote ya kutajia Muumba hufafanuliwa kwa utaratibu ili watoto waweze kuyashika na kuzielewa sifa zake. Hali hiyo, huwawezesha kujua jinsi Mungu alivyo na nguvu, ukuu na uwezo mkubwa na wa mwisho kabisa. Katika msamiati wakati mwingine maneno hutumiwa kutoa maana tofauti na hali ya kawaida. Baadhi ya msamiati wa aina hiyo ni kama:

Msamiati wa Kiarabu	Maana/Matumizi
Sahil	Pwani
Kamis	Kamisi
Aql	Akili
Wasiya	Wosia
Att-taali:m	Elimu

#### 1.7 Kielelezo cha Msamiati.

Orodha hiyo imeonyesha kuwa nadra maneno ya Kiarabu yamalizike kwa irabu.

### 3.2.4 Kipengele cha Matamshi

Kando na maendelezo, kipengele cha matamshi hutiliwa mkazo pia. Matamshi katika lugha ya Kiarabu kama zilivyo lugha zingine hutofautisha maana. Matamshi yakivutwa au yakikatwa ghafla huenda yakatofautisha maana. Maalim huchukua muda kuwaelekeza watoto chuoni ili waweze kuelewe umuhimu wa kutoa matamshi sahihi. Watoto huwasikiliza walimu wakiyatoa matamshi inavyostahiki kisha wakaongozwa katika kuyatoa matamshi. Baadhi ya maneno hayo huweza kufupishwa au kurefushwa kama hali ilivyo katika mifano inayofuatia:

Maneno ya Kiarabu yaliyofupishwa	Kiswahili Sanifu
Adab	Adabu
Adha:b	Adhabu
Afdhal	Afadhali
Aghlab	Aghalabu
Aib	Aibu
Ajal	Ajali
Ala:m	Alama
Alfajr	Alfajiri
Aljabr	Algebra
Amin	Amini
Ama:n	Amani

1.8 Kielelezo cha Maneno yaliyofupishwa.

Kutokana na maendelezo hayo, imebainika kuwa abjadi huungana zikaunda maneno. Vile vile herufi zinaweza kuongezwa au kupungua maneno ya Kiarabu yanapoendelezwa. Uchunguzi nyanjani umeonyesha pia kuwa kuna hali ya kubadilisha sauti. Kwa sababu ya ukosefu wa sauti fulani katika lugha ya kwanza, mazoea humlazimu mtu kupanua dhana ili kuafiki maana husika. Matumizi ya /b/ badala ya /p/, /a/ au /i/ badala ya /e/ yanadhihirisha hali hiyo.

### 3.2.5 Kipengele cha Utunzi wa Vifungu

Maendelezo yafuatayo yametoka kulia yakaelekea kushoto.

Tawihud-

Al-Ikhlās

Ayatil-Kursi

- بيسمىلاهي الرحمن الرحيم الهامدولياهي  
الرحمن الرحيم بالاريديوم ربيع قليلا امين  
بالسيد المالكي في منتصف وايكان ابودو  
وايكا متوفر ابودو وايكانايستاهين يهدي ناس  
الاستراليه سيراتال مستايم سيراتال لادهينا  
الييهيم ويريل ماكتوبي ولد دال لين

- Mfano wa sentensi ni kama ufuatao:

Mtoto

mdogo

analia

sana

لودي

صغير البكاء

طفل

### 3.2.6 Mbinu za Kufunzia Lugha ya Kiarabu

Katika kuliendesha somo la lugha, maalim hutumia mbinu changamano. Ijapokuwa kunazo mbinu anuwai kama matumizi ya mafafanani, nyimbo (kaswida), maelezo, masimulizi, utendaji, majibu na maswali, kazi muradi pamoja na utazamaji katika mazingira halisi kama msikitini mbinu tegemezi ni ukariri. Watoto huhitajika kukariri sana bila kujali na kutilia mkazo maana na matumizi.

Inapowezekana maalim wawili hushirikiana katika kuliendesha darasani. Mmoja anaweza kufunza kipengele kimoja kama cha kusimulia huku mwingine akiwachunga watoto ili watulie darasani na kufuata wanayofunzwa. Baada ya kipindi tangulizi kama cha kusikiliza, maalim wanaweza kubadilishana majukumu. Kawaida huwa kuna utaratibu wa kuyaendesha mafunzo yote. Huwa kuna muda wa kusikiliza, kuongea, kuchora, kuandika abjadi, kusoma sauti na mwisho kuandika maneno na vifungu. Vile vile iwapo mmoja hajaweza kufika chuoni, watoto wanaweza kuendelea bila kukosa masomo. Maalim huwafunza watoto dhana mpya kabla ya kuwapa kazi ya mazoezi au kazi ya kutafitia.

Chuoni kuna adhabu mbalimbali. Kiboko na njia zingine za kuhakikisha adabu hutumika kulidhibiti darasa na hata kuwatia adabu watoto walio watundu. Tathmini hufanywa kama kigezo cha kumwezesha mtoto kujiunga na darasa la juu. Wanaoshindwa kuishika

na kuikariri Korani husalia kwa darasa moja mpaka wayajue wanayostahili kujua.

### 3.3.0 Ulinganifu Kati ya Lugha Husika

Kutokana na vipengele ambavyo vimeshughulikiwa hapo juu, imebainika kuwa lugha ya Kiswahili na Kiarabu zinaweza kulinganishwa kwani hali ya kufanana na kutofautiana imedhihirika.

Ahmed (1993), akielezea juu ya uhusiano kati ya Kiswahili na Kiarabu anasema;

“Uhusiano wa lugha ni wa kuingiliana na kuathiriana kwani lugha si viziwa. Kiswahili na Kiarabu zilifanya tangu karne ya kwanza baada ya kuja kwa Yesu.”

Uwiano na tofauti ambao umedhihiri ni kama ufuatavyo:

Kwanza, lugha zote zimeshughulikiwa kama masomo ya lazima yanayopewa kipaumbele katika mifumo husika ya elimu. Katika lugha zote mbili kuna vipengele vinavyofanana vinavyotiliwa mkazo kwa mfano abjadi, maendelezo, mtindo wa kuandika, msamiati na mpangilio wa maneno katika sentensi.

Katika kuvishughulikia vipengele hivyo vya lugha msisitizo upo juu ya stadi zote nne (4) kwani hali ya kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika zimeangaziwa kupitia kazi na mazoezi ya kukariri na kuandika. Kila mojawapo ya lugha ina umuhimu wake yaani ina hadhi na nafasi yake katika maisha ya wanajamii. Uchunguzi umeonyesha kuwa kunazo sauti za Kiarabu zinazopatikana katika Kiswahili na hata baadhi ya msamiati.

Vile vile walimu wanapoyaendesha masomo hayo hutumia silabasi inayowaongoza taratibu. Na kwa sababu kila somo lina lengo maalum, walimu hulenga kuwaongezea wanafunzi akili, maarifa na ujuzi ili wapate kuwa na umilisi.

Hata hivyo, bado kuna tofauti kati ya hizo lugha nazo ni kama zifuatazo:

Katika lugha ya Kiswahili, lugha inakua kila uchao na kupata msamiati mpya. Hali hiyo inakubaliwa kinyume na hali ilivyo katika lugha ya Kiarabu ambapo lengo ni kuhifadhi lugha na hati asilia kupitia msisitizo wa kukariri bila kujali kujua maana. Kwa upande wa abjadi imebainika kuwa lugha ya Kiarabu ina herufi nyingi kuliko lugha ya Kiswahili.

Katika maandishi lugha ya Kiswahili inatumia hati ya Kirumi (maandishi yanatoka kushoto na kuelekea kulia) ilhali kwa Kiarabu, hati asilia inadumishwa (maandiko yanaanza kulia na kuenda kushoto). Katika lugha ya Kiarabu maendelezo yanahusisha alama maalum ambapo maandishi yanaweza kushikana au kuwachana yanapoandikwa kama ilivyoonyeshwa hapo awali. Katika Kiswahili herufi ni aidha kubwa au ndogo.

Tukirejelea dhima ya lugha mbili, Kiswahili ni lugha ya kitaifa na hata kimataifa. Inatumiwa katika ulimwengu wa kazi, inawapa pia watu kitambulisho, kando na kuwaunganisha. Kwa upande mwingine Kiarabu ni lugha ya kupokeza dini. Kwa mujibu

wa Al Muntakhab Kiarabu ni lugha inayoaminiwa kuwa takatifu katika jamii husika. Inachukuliwa kuwa ndiyo lugha itakayotumiwa huko Ahera. Hivyo basi lengo la somo hilo ni kuwawezesha watoto kuijua na kuikariri Korani wanaposwali au wanapoomba. Kutokana na ukosefu wa sauti zingine za Kiswahili kama /c/, /e/, /f/, /g/, /p/ kwa lugha ya Kiarabu wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili baada ya kupitia Duksi hupata ugumu wa kuzitamka na kuzitambua sauti hizo ngeni. Wao husoma kwa maneno yaliyo na sauti /p/ wakitumia /b/ kama hali ilivyodhihirika katika mifano ifuatayo:

Maendelezo ya Kiarabu	Maendelezo ya Kiswahili sanifu
Besa zimebatikana	Pesa zimepatikana
Ninabakia nguo	Ninapakia nguo
Bika chakula	Pika chakula
Ilete samaki baba	Ilete samaki papa
Bebeta moto	Pepeta moto

### 1.9 Kielelezo cha Athari ya Kiarabu.

#### 3.4.0 Hitimisho

Katika sura hii, tumezishughulikia lugha mbili (2), ya Kiswahili na ya Kiarabu. Tumeangazia dhima na nafasi ya lugha zote mbili. Tumejadili vipengele vya lugha kama abjadi, msamiati, mtindo wa kuandika, maendelezo na mbinu za kufunzia lugha. Tumejikita katika athari ya elimu ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili ambapo imebainika kuwa lugha hizi huweza kuathiriana. Palipo na uwiano kama kwa msamiati, inakuwa rahisi kwa wanafunzi kujifunza na kuendelea. Lakini

palipo na ukinzano, wanafunzi hujikuta wamehamisha dhana walizozioea hadi lugha ngeni. Mfano mwafaka ni pale wanapoyaendeleza maneno kana kwamba ni ya Kiarabu. Wanafunzi huongeza, hupunguza na hata hubadilisha sauti wakati wanapozitumia herufi kama /q/ na b/ badala ya /k/ na /p/.

Khalid (1997), akiunga mkono maoni hayo anasema kuwa:

“Kuchanganya lugha kupitia mifumo miwili husababisha hali ya ujifunzaji kurudi chini kwani akili isipoegemea kitu kimoja wakati mmoja, yaliyosomwa husahaulika”

Akielezea, anatoa mfano wa wachezaji ala kuwa mtu huwa maarufu kwa kucheza ala moja wala si mbili. Isitoshe, anasema waandishi kawaida huvuma kwa jambo moja. Akimtaja Joseph Conrad mwandishi kutoka Uholanzi, anasema yeye alipoingia na kuishi katika mazingira yaliyosheheni Kiingereza, alifaulu kuandika kwa Kiingereza pekee.

Na katika sura inayofuatia tumeangazia uchanganuzi wa data ili kudhihirisha athari ya elimu ya Duksi.

## SURA YA NNE

### ATHARI YA DUKSI KATIKA UFUNZAJI NA

### UJIFUNZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI

#### 4.0 Utangulizi

Katika sura ambayo imetangulia tumeshughulikia lugha mbili, ya Kiswahili na ya Kiarabu. Kutokana na utafiti imedhihirika kuwa Kiswahili ni lugha ya Kitaifa na Kimataifa ilhali Kiarabu ni lugha ya kufunzia mafunzo ya kidini katika kiwango cha Duksi, madrassa na hata Chuo Kikuu. Kwa upande mwingine lugha ya Kiswahili imeenea sana na inatumika hata nje ya nchi yetu. Lugha ya Kiswahili inazo abjadi ambazo zinatofautiana na za lugha zingine kama Kiarabu na Kiingereza. Inazo konsonanti ishirini na tano (25) na irabu tano (5). Katika lugha hizi, sauti huwa zinaungana ili kuunda maneno. Baadhi ya sauti, herufi na maneno yaliyo katika lugha ya Kiswahili yanapatikana pia katika lugha ya Kiarabu. Vile vile imedhihirika kuwa silabi anuwai zinaweza kutumiwa katika kuunda maneno mengi.

Mtindo wa kuandika pia umeangaziwa. Imebainika kuwa mtindo wa Kirumi ndio hutumiwa. Maneno huendelezwa kutoka kushoto kuelekea kulia. Na katika kutamatisha, tumejadili mbinu za kufunzia lugha zote mbili, ya Kiswahili na ya Kiarabu.

Katika kuiendeleza kazi hii, tumetathmini kazi za darasani, majibu ya hojaji zilizojazwa na watafitiwa kando na kuchanganua majibu ambayo yametokana na mahojiano kati ya

mtafiti na walioshirikishwa (sampuli changamano imehusisha: wazazi, walimu, Sheikh, maafisa wa elimu na wanafunzi). Ili kulifikia lengo kuu, tumezingatia maoni, mielekeo na matarajio ya watafitiwa pamoja na tajriba za wanajamii.

#### **4.1.0 Uchanganuzi wa kazi za darasani**

##### **4.1.1 Vipengele vya Kisarufi**

Mtafiti aliweza kuhudhuria darasa mara nne wakati walimu walipokuwa wakiendesha mada za imla, uandishi wa sentensi na insha katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti ametafiti athari ya Duksi kupitia kuchunguza namna ufunzaji na ujifunzaji hufanywa. Vile vile katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, walimu walishughulikia usahihishaji na marekebisho. Imedhihirika kuwa katika baadhi ya madarasa, walimu walifaulu kuwasilisha ujumbe wao.

Wanafunzi pia waliweza kuwasiliana na walimu wao. Uchunguzi umeonyesha kuwa wanafunzi wanajimudu katika lugha kutokana na jinsi walivyojibizana (mbinu ya maswali na majibu ilitumiwa). Walimu na wanafunzi waliweza kutumia lugha ya Kiswahili kutoka mwanzo hadi mwisho wa kipindi. Kinyume na hali hiyo, katika shule zingine mbili, walimu pamoja na wanafunzi walichanganya ndimi kila walibadilishana maoni. Walitumia lugha ya Kiswahili na Kisomali katika kuuliza na kujibu maswali.

#### 4.1.2 Kipengele cha Sauti

Kupitia kwa maongezi, imebainika kuwa wanafunzi waliokuwa wamehitimu katika mafunzo ya Duksi waliongoza darasani. Walikuwa huru kuuliza na kujibu maswali. Ijapokuwa walikuwa na shida ya kutamka sauti /p/, walijibidiisha mara kwa mara kutoa matamshi sahihi. Ugumu huo huenda ulitokana na mazoea yao kwani sauti /p/ haipo katika lugha yao ya kwanza. Vile vile baaada ya kuwasikiliza wanafunzi wakiongea, ilidhihirika bayana kuwa wanafunzi wana ulimi mzito unaofanya matamshi yamalizike kwa sauti nzito kama vile sauti *h* katika neno *katah*.

#### 4.1.3 Kipengele cha Abjadi

Kutokana na utafiti, imebainika kuwa lugha zote mbili zina abjadi. Abjadi zingine zinafanana na zingine zinatofautiana. Abjadi zinazopatikana katika lugha hizi mbili ni kama zifuatazo :

*a, b, d, f, g, h, I, j, k, l, m, n, o, r, s, t, u, v, w na y.*

Uchunguzi umeonyesha pia kuwa abjadi zisizopatikana katika lugha ya Kiarabu (kama vile /e/ na /p/) ndizo huwatatiza wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Wanafunzi huzoea abjadi ambazo huzitumia katika lugha wanayoitumia kila siku kisha wanapojifunza lugha mpya wakajikuta wamezihamisha na kuzitumia abjadi hizo bila kukusudia.

Ingawa lugha hizo mbili zina uwiano katika vipengele vya kisarufi kama abjadi, sauti na

baadhi ya msamiati, bado kuna tofauti katika maendelezo. Utafiti wa nyanjani umeonyesha kuwa mazoezi ya mara kwa mara yanaweza kutatua shida hiyo ya matamshi na hata ya maendelezo. Hata hivyo, kukosa kuyarekebisha makosa hayo mapema huzidisha shida kiasi cha kupotosha maana na kukwamisha mawasiliano.

#### **4.1.4 Kipengele cha Maendelezo**

Kutokana na kazi za wanafunzi, imebainika namna wanavyozipanga kazi zao hususan mtindo wa kuandika, ati na hijai. Vipengele hivyo vyote vimeonyesha kuwa kuna athari inayoweza kuhusishwa na lugha ya kwanza. Wanafunzi wameonyesha kuwa na mazoea ya kuandika jinsi wanavyoandika katika darasa la Duksi. Kuna hali ya kubadilisha herufi au kuwacha irabu zinapokuwa mwishoni mwa maneno. Aghalabu humchukua mwalimu muda mrefu kuwaelezea wanafunzi ili waweze kuyaelewa na kuyatambua makosa yao katika kutamka na kuandika. Sababu ni kuwa wengi wao waliendelea kuyarudia makosa hata baada ya kukosolewa.

Kando na mtafiti kuyasoma baadhi ya hayo masuala daftarini, aliyasikia pia na hata kuyaona darasani walimu walipokuwa wanawafunza wanafunzi. Katika kuyaendeleza maneno wakati mwingine waliongeza herufi au walibadilisha irabu kinyume na maendelezo ya lugha ya Kiswahili.

Baadhi ya mifano ni kama ifuatayo:

<b>Maendelezo yasiyo sahihi</b>	<b>Maendelezo sahihi</b>
Wajih	Wajihi
Ma'na	Maana
Swahib	Sahibu
Khitab/Kitab	Kitabu
Hisab	Hesabu
Thamanin	Themanini

## 2.0 Kielelezo cha Maendelezo yasiyosahih*i*

Hali ambayo imejitokeza hapo juu inaweza kuhusishwa na lugha ya wanafunzi ya kwanza na ile ya Kiarabu. Katika mifano iliyotolewa hapo juu, kuna hali ya kupunguza irabu kwa mfano neno ma'na badala ya neno maana. Pia kuongezea konsonanti kumedhihiri kupitia kwa maneno kama mukhutasar, khitab na mengineyo. Kwa jumla sauti zinazotatiza ni irabu ya /a/, /e/, na /i/. Aghalabu zinabadilishwabadilishwa kama ilivyoonyeshwa hapo awali.

Ijapokuwa wanafunzi wa darasa la tano waliweza kuandika maneno waliyoyasikia maendelezo yaliwatatiza. Asilimia themanini (80%) ya wanafunzi walijikakamua kuendeleza maneno ya sehemu za mwili sahihi yaani mapua, masikio, kichwa, midomo, miguu, uso, paja na kipaji. Asilimia ndogo iliyosalia, ishirini (20%) ndiyo ilifaulu katika kuyaendeleza sahihi maneno paja, kipaji, pua na kwapa.

Wengi wao waliyaendeleza vibaya kama inavyoonyeshwa:

Maendelezo Sahihi	Maendelezo yasiyo sahihi
Kipaji	Kibaji
paja	Baja
poa	Boa
Pua	Bua
Pupa	Buba
Papa	Baba
Pete	Bete
Pepo	Bebo

### 2.1 Kielelezo cha Maendelezo.

Kutokana na mifano kazi ya wanafunzi asilimia sitini (60%) ilionyesha kuwa walitatizika na matumizi ya herufi /p/. Jambo hilo lilitokana na ukosefu wa herufi hiyo kuliwafanya wanafunzi kukosea. Walitumia /b/ bila kuona hilo kama kosa la maendelezo.

#### 4.1.5 Utunzi wa Sentensi

Wanafunzi waliweza kuzitunga sentensi wakiyatumia maneno waliyoyaandika katika kazi ya imla. Asilimia sabini (70%) walikuwa na uwezo wa kuunganisha maneno na kuzipata sentensi. Mpangilio wa maneno ulionyesha kuwa walielewa sheria za lugha yaani sarufi. Takriban kila mwanafunzi alianza sentensi kwa nomino kisha akafuatisha kitenzi na halafu akatamatisha kwa kivumishi. Ijapokuwa walianza na kutamatisha kwa aina mwafaka za maneno, wengi hawakukumbuka kuzitumia herufi kubwa wala nukta.

Bado kulikuwa na tatizo la uakifishaji. Wengi wao walitumia herufi ndogo mwanzoni mwa sentensi na hata walipotaja nomino huru hawakukumbuka matumizi ya herufi kubwa. Hali hiyo imejitokeza katika mifano ifuatayo:

Sentensi zisizo sahihi	Sentensi sahihi
<u>m</u> imi nitafurahi nikim <u>b</u> ata <u>s</u> ofia	Mimi nitafurahi nikimpata Sofia.
<u>j</u> uma mtoto wetu ame <u>b</u> oa kitindani	Juma mtoto wetu amepoa kitandani.
<u>S</u> hule ya <u>k</u> amu imefanya vizuri kwa mtihani	Shule yetu ya Kamu imefanya vizuri katika mtihani.

### 2.2 Kielelezo cha Sentensi.

Mifano iliyopigiwa kistari inaonyesha makosa ya hijai hususan matumizi yasiyosahihi ya /b/. Matumizi haya ya kubadilisha herufi yametokana na athari ya lugha ya Kiarabu ambayo haina herufi /p/. Badala ya kutumia herufi kubwa, herufi ndogo zimetumiwa. Hakuna alama ya kuonyesha tamati kwani sentensi hazina alama ya kuakifisha (kituo au nukta) mwishoni mwa sentensi.

Baada ya mwalimu kupitia sentensi kadhaa huku akizinakili ubaoni, wengi wa wanafunzi walianza kuonyesha kuwa walielewa na hata kuweza kuyatambua makosa yao. Mwalimu alichagua baadhi yao kwenda mbele ya darasa na kuziendeleza sentensi zao ubaoni. Kufikia mwisho wa masomo hayo darasani, ilibainika kuwa makosa hayo yanaweza kutatuliwa kwa kufanya mazoezi na marudio mara kwa mara. Hatua ya kuelekeza na kufuatilia kwa uangalifu inaweza kuwasaidia wanafunzi kutambua sarufi ya lugha husika.

#### 4.1.6 Athari ya Elimu ya Duksi.

Kutokana na uchunguzi uliofanywa, imedhihirika kuwa athari ya elimu ya Duksi inaweza kuelezwa kwa hali mbili. Kunazo athari nzuri na athari mbaya. Tukirejelea shughuli katika darasa la Duksi, ni wazi kuwa kuna athari chanya na athari hasi inayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi ya lugha ya Kiswahili katika mazingira yaliyosheheni mafunzo ya kidini.

Wanafunzi wanaopitia elimu ya Duksi kabla ya kujiunga kwanza na shule za malezi na hatimaye za msingi, wamedhihirisha ujasiri na uwezo wa kujieleza bila kuwa na uoga wowote. Hivyo basi, elimu ya Duksi imeonyesha kuwa na uwezo wa kuwawekea wanafunzi msingi bora. Wanafunzi wanapoingia shule za msingi huwa tayari wameshawazoea walimu kwani wao huwa wameshakutana na walimu. Hivyo basi badala ya wanafunzi kupoteza muda katika kujaribu kujifahamisha kwa mazingira mapya ya shule, wao hukaa kwa utulivu wakaanza kusoma moja kwa moja. Kwa sababu ya kupewa mafunzo juu ya maadili na nidhamu, wanafunzi huliona jambo la kutii na kufuata sheria kuwa jambo la kawaida.

Mwalimu anapoanza kuwafunza juu ya mada kama ya abjadi, kutamka na kuyaendeleza maneno, wanafunzi waliohitimu katika Duksi huwa hatua nyingi mbele ya wenzao kwani tayari huwa wamefunzwa mambo mengi. Huwa wamesoma jinsi ya kushika kalamu na

kuandika kwa kitabu. Kutokana na mafunzo ya Duksi wanafunzi huweza kushika baadhi ya maneno yanayopatikana katika lugha ya Kiswahili. Baadaye, wanafunzi wanapofunzwa katika shule za msingi hayo maneno huwa marudio kwao. Baadhi ya maneno hayo ni kama:

*Kalamu, mwalimu, darasa, Korani na mengine mengi.*

Hatua hiyo ya kujifunza elimu ya Duksi, huwarahisishia wanafunzi mpito wa kubadilisha na kuingia katika shule ya malezi na baadaye ya msingi. Wakati wa kushirikishwa katika mjadala au kujibu maswali, wanafunzi waliohitimu kwa chuo cha Duksi, huongoza. Wao huwa wamezoea kazi ya maswali. Wanafunzi hao huipata kazi ya shule za malezi na msingi kuwa nyepesi mno. Rekodi za wanafunzi waliohitimu katika Chuo cha Duksi cha Young Muslim zimeonyesha kuwa wanafunzi kama hao, wakati mwingine hurukishwa madarasa kusudi waweze kudhibitiwa kando na kutowapotezea wakati kusoma mambo ambayo tayari wanayaelewa ipasavyo.

Walimu wamegundua kuwa wanafunzi hao huwa na uwezo wa kuelewa mambo haraka wakilinganishwa na wanafunzi wengine ambao hawajayapokea mafunzo hayo. Wanafunzi watatu (3) kati ya sampuli ya wanafunzi walioteuliwa walikuwa wamehitimu na kufanywa maalim. Wanafunzi hao huwasaidia Sheikh katika kuwafunza vijana wenzao habari za kidini chini ya uongozi wa Sheikh. Basi imebainika kuwa wanafunzi hufaidika mno wanapoanza mafunzo kwa elimu ya Duksi. Vile vile hufunzwa juu ya wajibu kisha wakaanza kuwajibika ilivyotakikana.

Kutokana na shughuli na kazi hufanywa katika Chuo cha Duksi, wanafunzi huweza kuyapata mazoezi ya kufanyisha viungo kazi kama vile mikono, vidole, miguu na akili ili baadaye wanapoanza kushika kalamu na kitabu, waweze kufanya hivyo bila shida yoyote. Mazoezi hayo wanayapata kutokana na kazi za mikono kama za kufagia, kuosha darasa, kuandika, kufuta na kuosha mbao zao. Kujitengenezea wino pia ni shughuli mojawapo inayowawezesha kupata tajriba ya muhimu na ya kuwafaa mwanzo wanapojiunga na shule za malezi na baadaye za msingi.

Utaratibu wa kukaa na kusikiliza mafunzo kwa muda mrefu ni mazoea bora yanayowasaidia wanafunzi wanapoanza shule za malezi au za msingi. Wanafunzi huwa tayari wanaweza kustahimili muda mrefu wa mafunzo bila kupoteza umakinivu wao. Katika madarasa ya elimu ya Duksi wanafunzi hupata nafasi ya kutangamana na wenzao. Hivyo basi, wanapata fursa ya kujifunza namna ya kukaa na watoto wengine kwa amani. Tabia hiyo, huwa inawafaidi wanapojikuta katika mazingira mengine kwani tayari huwa wanaelewa jinsi ya kuishi na wenzao.

Kutokana na maelekezo bora ya Sheikh juu ya umuhimu wa matamshi sahihi (yenye kupanda na kurudi chini) wanafunzi huweza kutambua mapema umuhimu wa matamshi sahihi. Wao huanza kujizoesha kutoa matamshi bora mapema. Kwa hivyo wanapoenda kwa shule ya malezi au msingi, wao huweza kufuata kwa urahisi maelezo ya mwalimu

juu ya mdundo na mapigo ili kutoa sauti nzuri, nyororo na yenye mahadhi.

Katika darasa la Duksi wanafunzi hufunzwa juu ya kuweka Muumba wao mbele ya chochote kile. Watoto wanaposhika dini, aghalabu huishia kuwa watu wenye nidhamu na tabia nzuri. Na kwa sababu ya mwenendo mzuri, wanafunzi huzingatia kupata ushindi darasani. Huwa hawapotezi wakati kwa shughuli zisizo na maana. Huwa wanatambua namna ya kuyaendesha maisha kisha wakasoma kwa bidii. Kinyume na watoto wengi ambao hawana msingi wa kidini, huwa watovu wa nidhamu na hivyo basi muda wao huutumia kwa kuzembea au kutenda maovu.

#### **4.1.7 Mbinu za Kufunzia**

Mbinu za kufunzia katika Chuo cha Duksi ni anuwai. Maalim hutumia mbinu mseto au changamano. Kule kuchanganya mbinu huwafanya wanafunzi kila mara kuchangamkia mafunzo. Kupitia shughuli ya kukariri na mazoezi ya mara kwa mara, kumbukizi za wanafunzi hunolewa vya kutosha.

Wanafunzi hao wanapoingia shule ya malezi na hatimaye msingi, akili yao huwa imekua na kuzoea kushika mafunzo na ndiyo sababu wanafunzi wanaohitimu katika vyuo vya Duksi hudhihirisha umaarufu wa kipekee darasani.

Kwa sababu elimu ya Duksi ni ya lazima na hutolewa wakati wowote, wanafunzi

wanaohudhuria mafunzo ya Duksi hulazimishwa kujifunza na kujizoesha kufanya mambo haraka. Wanaoshindwa kutumia wakati wao vizuri, huadhibiwa. Kukosa kukamilisha kazi huwakosesha muda wa kupumzika na hata kucheza. Mazoea hayo ya kuwajibika, kujichunga na kujibidiisha huwafaidi sana wanafunzi wanapojiunga na shule za malezi pamoja na za msingi.

Maalim wanapowafunza wanafunzi chuoni, hutilia mkazo umuhimu wa kufanya kazi vizuri. Kwa mfano unadhifu hupewa kipaumbele. Watoto wanatakiwa kukua na kukaa katika mazingira safi. Kwa vile wanapaswa kufanya haya yote chuoni, wanapojiunga na shule ya msingi huwa tayari wamezoea kujitunza na kutunza vitu vyao kama inavyotakikana. Hivyo basi wao huyafurahia maisha ya shule za msingi.

Maalim huwaelekeza wanafunzi kwa kila hali. Kuhusu kuandika, huwaonyesha kwa kuwaandikia ubaoni. Ikimlazimu maalim humshika mwanafunzi mkono akautembeza huku akiandika. Kitendo hicho cha kumwongoza mwanafunzi ni muhimu katika madarasa ya chini. Mfano mwingine ni kuwa wakati wa kuimba, kukariri na kusoma, wanafunzi wote huhimizwa kutoa sauti kubwa. Kwa vile makelele hayo huwepo pia katika shule za malezi na za msingi, watoto huwa hawaonyeshi hali ya kushtuka wakati wa kujiunga na madarasa hayo. Wanafunzi hujihisi nyumbani wakaendelea kusoma bila ugumu unaotokana na kubadilisha mazingira.

#### 4.1.8 Athari Hasi ya Elimu ya Duksi

Tumegundua pia kuwa licha ya mchango wa Duksi kwa ufunzaji na ujifunzaji katika shule za malezi na msingi, kuna athari hasi. Athari hizi huwa ni za kijamii, kisaikolojia na kimasomo. Kulingana na Wizara ya Elimu, matumizi ya viboko kama njia ya kuadhibu imepigwa marufuku. Kinyume na sheria hiyo, chuoni, maalim huwachapa watoto wanapokosea. Wanajamii (wakiwemo maalim na wazazi) wanaamini kuwa watoto wasipochapwa hawawezi kuwa na nidhamu. Kiboko kimekusudiwa kuwadhibiti watoto darasani. Maalim huwachapa wanapokosa kushika wanayofunzwa kando na kukosa nidhamu.

Kwa sababu mafunzo ya Duksi hutolewa wakati wowote, wanafunzi huweza kuonyesha hali ya uchofu wafikapo shuleni baada ya kuhudhuria mafunzo ya Duksi. Wakati wa kuendesha mafunzo, maalim huwachapa watoto kusudi watulie darasani, wajifunze au wayakariri vilivyo wanayofunzwa. Hapo hofu ambayo imejitokeza ni kuwa watoto wanapozoea kiboko, inachukuliwa kuwa wanaweza kusumbuka sana wanapoingia daraja ile nyingine. Athari hizi ni za kisaikolojia.

Utafiti umeonyesha kuwa kuna wanafunzi ambao hujificha wakati wa darasa wakajitokeza baada ya shule kwa sababu wanaelewa hakuna kiboko kitakachotumika huko katika shule za elimu ya kimagharibi.

Hofu ya kuchapwa wakati wa mafunzo ya elimu ya Duksi, imedhihirika kwani hali hiyo huwafanya wanafunzi wasitulia darasani wakati masomo ya shule za malezi na msingi yanapoendeshwa. Wengine hata huamua kusinzia makusudi darasani ili wakati wa Duksi wawe macho na hivyo basi kukwepa viboko kali.

Kuhusu hali ya kuendesha masomo ya Duksi wakati wowote, uchunguzi umeonyesha kuwa muda mwingi hutumiwa kwa elimu ya Duksi kuliko elimu ya shule za malezi na msingi. Sababu ni kuwa mafunzo ya Duksi hutolewa asubuhi mapema, aduhuri, jioni na hata usiku. Mtoto anatarajiwa kuhudhuria mafunzo hayo zaidi ya mara mbili. Kule kubadilishabadilisha kutoka Duksi hadi shule za malezi au za msingi kumeonekana kuathiri ufunzaji na ujifunzaji wa lugha na masomo mengine yanayotolewa katika mfumo wa 8-4-4. Wanafunzi huwa wanachoka. Wanafunzi huwa hawana muda wa kucheza wala kupumzika. Kitambo wanafunzi wamalize kazi za darasani na za chuoni, huwa muda wa kulala, kupumzika na kucheza umedidimia. Hali hiyo huwafanya wanafunzi kukosa muda wa kuwawezesha kuimudu sarufi na lugha ya Kiswahili kwa jumla.

Asilimia thelathini na nne ya wanafunzi wanaopitia elimu ya Duksi, wameonyesha tamaa ya kutaka kuendelea na elimu hiyo lakini kwa mpangilio maalum. Wanaonelea kuwa ni vyema kama elimu ya Duksi inaweza kutangulia elimu ya malezi na msingi ili hali ya kuchanganya elimu mbili isikuwepo. Kila aina ya elimu inafaa ishughulikiwe kwa wakati mmoja na kwa utaratibu unaotilia maanani maslahi na mahitaji ya mwanafunzi binafsi.

Wanafunzi pamoja na walimu wameonyesha kufurahia ratiba ambayo inamruhusu *mwanafunzi kuwa mtoto*. Watoto waweze kulishughulikia jambo moja kwa wakati mmoja kisha wapate muda tosha wa kucheza na kufurahia maisha kama watoto. Mahojiano yamedhihirisha kuwa wanafunzi huwa hawana muda wa kutosha wa kucheza, kulala na kupumzika baada ya mafunzo yoyote yale. Athari hasi huathiri pia kisarafu, hijai na matamshi.

#### 4.2.0 Fasiri ya hojaji na majibu ya mahojiano.

Uchunguzi umeonyesha kuwa elimu ya Duksi ni mafunzo ya kimsingi ya dini ya Kiislamu. Neno Duksi limeelezwa kuwa mahali au chuo cha mafunzo ya kidini. Utafiti huo umedhihirisha kuwa elimu hiyo ni kongwe na imeshika mno katika jamii husika. Elimu hiyo imepewa nafasi ya kikati katika jamii. Mafunzo hayo hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hutolewa na yeyote yule ambaye ameshahitimu, wakati wowote na mahali popote.

Imebainika kuwa zamani za kale elimu hiyo ilikuwa ikitolewa kwa kivuli cha jengo au miti. Wakati huu madarasa maalum yamejengwa kwa shughuli hiyo. Kutokana na mahojiano ni bayana kuwa athari nzuri inakithiri athari hasi. Elimu ya Duksi imeonekana kuchangia pakubwa mafunzo ya elimu ya malezi na ya msingi. Hali halisi imeonyesha kuwa mafunzo ya Duksi na elimu ya shule za msingi yanajengana, yanaingiliana, yanategemeana na kukamilishana. Mafunzo yanayotolewa katika Duksi yanaweza

kurudiwa au kujengewa katika shule za malezi na msingi. Baadhi ya hayo mafunzo ni kama: *Matamshi, maendelezo, kusoma, kuandika na kukariri.*

Masuala ya kusoma kwa sauti, kukariri na kuandika kwa hati nzuri, hutiliwa mkazo kwanza katika chuo cha Duksi kisha baadaye yakaendelezwa katika shule za malezi pamoja na za msingi.

Kulingana na maoni ya walimu, wazazi, wanafunzi, Sheikh na maafisa wa elimu, kunayo masuala mengine mengi yanayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Baadhi ya masuala hayo ni:

- Hali ya mazingira na anga katika eneo husika hutatiza shughuli za ufunzaji na ujifunzaji. Joto huwa kali mchana kiasi cha kuwafanya wanafunzi wasiweze kutulia.
- Ukosefu wa vyakula, maji na majani hulazimisha wanajamii wengi kuishi maisha ya kuhamahama. Wanafunzi wanapohama wanapoteza muda wa kujifunza
- Wakati mwingine wanafunzi huwacha hata kusoma kwa muda. Shughuli ya kutafuta chakula na maji aghalabu huwapotezea muda wa kusoma.
- Lipo pia tatizo la kuteua lugha ya kutumia. Wanafunzi hujikuta wanazo lugha mne (4) za kutumia wanapoingia katika shule za msingi (Lugha ya mama, Kiarabu, Kiswahili na Kiingereza). Hali hii humkanganya mwanafunzi na kumtatiza wakati wa kujifunza.

Uchunguzi umeonyesha kuwa suala la mielekeo bado linaathiri shughuli ya ufunzaji na ujifunzaji. Wanajamii wengi hawaamini wala hawaoni umuhimu wa elimu ya kimagharibi. Bado wanashikilia kuwa haina haja watu kupotezea wakati, nguvu na pesa shuleni ilhali hakuna kazi baada ya kuhitimu.

Wanafunzi wamelaumu uhaba wa walimu waliofuzu kwa matokeo mabaya ya mitihani ya kitaifa. Ukosefu wa vifaa vya usomi kwa mfano madarasa, vitabu, madawati ni baadhi ya sababu zinazoathiri ufunzaji na ujifunzaji. Utafiti umeonyesha kuwa Wizara ya Elimu imelishughulikia tatizo hilo kupitia mpango wa elimu ya bure katika shule za msingi.

Walimu wanalaumu hali ya kutowajibika kwa Wizara ya Elimu. Kule kubadilisha mitaala bila kuandaa warsha tosha za kuwawezesha walimu kupata fasiri kamili ya yaliyomo katika silabasi. Walimu wamedhihirisha hali ya kuchanganyikiwa juu ya fasiri ya mada zilizoshughulikiwa katika silabasi. Maafisa wa elimu mkoani wamewaunga mkono walimu ingawa wanayo matumaini ya kutokea warsha maishani.

Uteuzi wa vitabu huwatatiza walimu. Maagizo na maelezo kuhusu shughuli hiyo yamkini huwa hayaeleweki. Baadhi ya walimu hujikuta na vitabu wasivyovielewa. Hivyo basi kuvifunza ikawa shida. Imedhihirika wakati wa mahojiano kwamba baadhi ya vitabu ambavyo huteuliwa huwa vigumu kwao. Huwa havieleweki kwa urahisi.

Matarajio ya walimu ni kuwa maishani, mwangaza zaidi utatolewa na vitabu viteuliwe kwa haki kulingana na kiwango cha wanafunzi.

Imedhihirika kutokana na utafiti kuwa kulikuwa na upungufu wa walimu wa kufunza lugha ya Kiswahili ipasavyo. Vile vile walimu hao huwa hawatulii katika shule moja. Tabia ya kuhamishwa kutoka shule moja hadi nyingine una madhara yake. Pia kubadilisha walimu huathiri mifanyiko ya ufunzaji na ujifunzaji. Utaratibu kama huo hauruhusu hali ya kufuatiliza wanafunzi kusudi wasaidiwe hadi wahitimu.

Baadhi ya wanafunzi wanaonekana kukosa ari na moyo wa kusoma. Maoni ya wengi wao yameonyesha hali ya kutothamini elimu ya kimagharibi. Kuna uwezakano kuwa uhaba wa walimu wa lugha ya kiswahili katika mkoa unachangia tatizo hilo. Walimu wengine wamedai kuwa hulazimishwa kufanya kazi katika eneo moja kwa muda mrefu. Walimu wanaojikuta kwa hali kama hiyo, huvunjika moyo wakaamua kukaa tu bila kufanya kazi yoyote. Walimu hao wanaonelea kuwa ni bora kupewa nafasi ya kuhama wanapoomba uhamisho.

Katika kutamatisha wanafunzi wameonyesha kuwa lugha ya Kiswahili imeendelea kuwa ngumu kila uchao. Msamiati mpya unazuka kila siku kiasi cha kufanya Kiswahili kiwe kigumu kuliko hata Kiingereza. Kwa sababu lugha inakua wanafunzi wanahimizwa kujikakamua zaidi. Mazoezi ya mara kwa mara yanaweza kuwafaa kando na kujiepusha

na matumizi ya Sheng'.

#### 4.3.0 Hitimisho

Katika sura hii tumechanganua data. Tumeangazia athari ya elimu ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Tumepambanua athari chanya na athari hasi.

## SURA YA TANO

### HITIMISHO

#### 5.0 Utangulizi

Utafiti huu umefanywa kwa madhumuni ya kudhihirisha athari ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi ya lugha ya Kiswahili. Data imechanganuliwa kutoka mji wa Garissa na viunga vyake. Mbinu ya usomaji wa maktaba na utazamaji na usikilizaji nyanjani ndizo zilitumika. Mahojiano yalifanywa ambapo wanafunzi, wazazi, maalim, maafisa wa elimu na Masheikh walishirikishwa. Hojaji pia zilitumika na sampuli ambayo imetajwa hapo juu kisha majibu yakachanganuliwa kusudi kubainisha mahusiko ya elimu ya Duksi na namna yanavyoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Wanafunzi arobaini (40), walimu kumi na watano (15), masheikh wanne (4), wazazi wanne (4), maafisa wa elimu wawili (2), walikamilisha hojaji. Hojaji hamsini na tano zimechanganuliwa lakini hizo zingine kumi hazikuweza kusomeka.

Hojaji hizo zimedhihirisha maana, umuhimu na mbinu za kufunzia elimu ya Duksi. Mahojiano kati ya mtafiti na sampuli ambayo ilishirikisha wazazi, wanafunzi, walimu, Sheikh na maafisa wa elimu kutoka mjini Garissa na viunga vyake hususan taarafa ya kati kudhihirika kuwa athari ya elimu ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi ya Kiswahili. Huko nyanjani, mtafiti alihudhuria mafunzo ya Duksi na ya lugha ya Kiswahili. Aliweza kukusanya data moja kwa moja kutokana na yaliyojiri darasani na chuoni katika shughuli za utenda kazi.

Data ya utafiti huu imefasiriwa kwa misingi ya nadharia ya Uchanganuzi Linganishi katika kuonyesha uhusiano kati ya vipengele vya lugha ya Kiswahili na ya Kiarabu kando na kuangazia mbinu za kufunzia. Hivyo basi, utafiti ulifaulu kutimiza malengo ambayo yalikuwa:

- i). Kubainisha maana na utaratibu wa elimu ya Duksi
- ii). Kulinganisha na kulinganua vipengele vya kisarafu (Kiswahili na Kiarabu)
- ii). Kupambanua mbinu za kufunzia lugha ya Kiswahili na ya Kiarabu
- v). Kuchunguza athari ya elimu ya Duksi katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili
- v). Kuangazia mikakati ambayo inaweza kuboresha na kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Ili kuyafikia malengo hayo, vipengele vifuatavyo vilishughulikiwa:

- Abjadi.
- Maendelezo.
- Mtindo wa kuandika.
- Msamiati.
- Mbinu za kufunzia.
- Mpangilio wa maneno katika sentensi.

### 5.1.1 Muhtasari wa Utafiti

Katika sehemu hii, ufafanuzi zaidi umefanywa kudhibitisha kuwa malengo yaliyotajwa yametimizwa. Utafiti ulifanywa mjini Garissa, ulihusisha sampuli mseto yaani walimu, wanafunzi, maafisa wa elimu, sheikh na wazazi. Shule nne (4) ambazo zilishirikishwa ni shule ya msingi Garissa, Korakora, Young Muslim na Sankuri.

Hojaji zilitumiwa na mahojiano yakafanywa katika kukusanya data. Kutokana na shughuli hizi utafiti umefanikiwa kuonyesha kuwa elimu ya Duksi ni mafunzo ya kimsingi ya dini ambayo ni ya lazima. Yamkini elimu hiyo kongwe inaendelea kupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Uchunguzi umeonyesha kuwa elimu hiyo imeenea sana na kuthaminiwa na wanajamii husika. Imebainika pia kuwa wakati wa mafunzo, msisitizo huwa kwa ukariri wala si kufafanua maana na matumizi ya maneno.

Katika chuo cha Duksi mafunzo mbalimbali hutolewa kama vile maadili, unadhifu, ulinzi na uhifadhi wa mazingira, jinsi ya kuishi na kuingiliana na watu mbali na masuala ya kidini. Mafunzo juu ya Korani huendeshwa. Msisitizo huwa juu ya ukuu na sifa za Muumba (majina tisini na tisa ya Mungu hupambanuliwa). Lengo kuu huwa kuwaonyesha watoto jinsi Mungu alivyo na uwezo wa kipekee. Watoto huelekezwa ili waweze kuishika na kuikariri Korani kwani wakati wa kuswali wanahitajika kunukuu aya. Mafunzo mengine yanahusu matendo mema, utamaduni, kutunza mazingira, usafi na lugha.

Katika somo la lugha, vipengele vya sarufi ya Kiarabu hufunzwa kwa makini. Maalim hushughulikia abjadi, maendelezo, matamshi sahihi na msamiati. Elimu hiyo hutolewa wakati wowote, mahali popote na maalim. Madhumuni ni kuwaandaa watoto kwa maisha yao ya sasa na ya baadaye. Kukariri Korani hupewa nafasi ya kipekee na ya kikati. Watoto hufunzwa namna ya kuishika na kuikariri Korani kwani hicho ndicho huwa kigezo cha kupimia uwezo wa wanafunzi. Kila mtu anayehitimu kwa elimu hiyo huheshimiwa sana katika jamii husika. Maalim hujitolea kuwafunza wanafunzi. Kwa sababu waamini huo ni wajibu kutoka kwa Mungu, maalim huifanya kazi hiyo kwa makini na moyo mkunjufu. Mwishowe maalim hutuzwa na wazazi kwa kazi nzuri hususan watoto wanapohitimu.

Lugha ambayo hutumiwa ni lugha ya Kiarabu. Maelezo yamkini hutolewa kwa lugha ya Kisomali na Kiarabu. Takriban watoto wote hulazimishwa kuhudhuria darasa la Duksi. Wanapokosa, maalim huwaadhibu kwa kuwafanyisha kazi kama kukariri na kuandika aya fulani wakati wenzake wanacheza kando na kufungiwa darasani. Wanafunzi pia huchapwa na maalim viboko kama njia ya kuwatia adabu na hekima.

Lugha hiyo ya Kiarabu ina uwiano na lugha ya Kiswahili hususan katika vipengele vya abjadi, sauti na msamiati. Hata hivyo lugha hizi zinatofautiana katika maendelezo. Aghalabu katika lugha ya Kiarabu maneno hayakamiliki kwa irabu. Maneno hubadilishwa au huongezewa sauti mwishoni mwa maneno kwani Kiarabu hakina sauti

zingine. Utafiti umeonyesha kuwa uhusiano kati ya elimu ya Duksi na elimu ya shule za msingi ni wa kujengana, kujengeana, kuingiliana kutegemeana na kukamilishana. Mafunzo ya Duksi huwekeka wanafunzi msingi dhabiti. Huangazia usomi, maisha ya sasa na ya baadaye.

Wanafunzi wanaotangulia kupata elimu ya Duksi hutokea kuwa washindi katika masomo ya baadaye yaani kwa shule za msingi. Mambo mengi ambayo huwa yapitiwa katika elimu ya Duksi kama msamiati hupanuliwa na kuendelezwa katika masomo ya baadaye.

Mbinu za kufunzia mafunzo ni nyingi. Maalim huwa anatumia mbinu changamano au mseto. Mafunzo hayo ya Duksi hutolewa taratibu na hatua kwa hatua. Maalim wawili huendesha mafunzo hayo kila wakati inapowezekana. Wanafunzi wanapoanza kusoma hakuna kuwabadishabadilisha walimu. Maalim hushikilia darasa kutoka mwanzo hadi mwisho wanafunzi wanapohitimu. Kule kufuatiliza huwafanya wanafunzi kuwa kila wakati makini wanapopewa mafunzo.

Kuimba, kukariri, kusoma na kuandika hufanywa wakati maalum ambao hutengwa. Wanafunzi huelekezwa na huzoeshwa kujifanyia mambo mengi kama kunadhifisha mazingira na vitu vyao binafsi. Mazoea hayo yote huwasaidia wanafunzi wanapojiunga na shule za msingi. Habari hizo huwa tayari wameshazipitia. Kutokana na muda unaotolewa mafunzo ya Duksi, lugha ya Kiswahili huathirika. Muda mwingi hutumika

kwa kufunza elimu ya Duksi. Kila uchao kabla au baada ya masomo watoto hawapati muda wa kutosha wa kufanya kazi za masomo katika shule za msingi kama lugha ya Kiswahili na masomo mengine.

### **5.1.2 Mahitimisho ya Utafiti**

Kutokana na utafiti, matokeo yamedhihirisha kuwa kuna athari chanya na athari hasi. Imebainika kuwa Duksi ni elimu kongwe na imeweka mizizi yake katika jamii husika. Wanajamii hao wanaithamini mno. Kwa sababu ya umuhimu wake katika jamii, hupokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kila muumini yuko tayari kuigharimia. Ama kwa hakika elimu hii hutolewa popote pale wakati wowote na mtu yeyote muradi awe ana uwezo wa kuikariri na kuelezea Korani kwa mapana inavyostahiki.

Mafunzo ya Duksi hayabagui umri wala wakati. Mtu yeyote anaweza kuhudhuria darasa la Duksi wakati wowote ule iwe usiku au mchana. Ufunzaji na ujifunzaji huanza kwa mada au mambo yanayoeleweka. Mwalimu huanzia kufunza mambo mepesi (rahisi na yanayoeleweka). Inakuwa rahisi kuendelea taratibu huku mambo mapya na magumu kiasi yanachopekwa hatua kwa hatua. Mwalimu huendelea hivyo kwa mpango maalum akafikia lengo huku akiyashughulikia mambo wasiyoyajua bila ugumu wowote. Katika darasa la elimu ya Duksi kunazo baadhi ya sauti na maneno yanayopatikana katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na hayo imebainika kuwa wanafunzi wanaohitimu katika Duksi kisha wanapojiunga na shule ya msingi, hufurahia somo la lugha ya Kiswahili. Kwa

wengi wao sauti na maneno ya Kiswahili huwa wanayaelewa kwa urahisi kwani huwa si mara ya kwanza kujifunza sauti hizo na maneno hayo. Wanafunzi kama hao huchangamkia masomo hayo na hivyo huweza basi kufanya vizuri katika mitihani ya kitaifa.

Kwa upande wa sarufi, utafiti umeonyesha kuwa makosa mengi ya kisarufi kama vile matamshi na maendelezo mabaya hutokana na athari ya lugha ya kwanza kwa mfano katika Kiarabu sauti /p/ na ndio sababu wengi wa wanafunzi wenye asili hiyo hutamka maneno yenye sauti /p/ vibaya, wao hutumia /b/ badala ya /p/. Vile vile kuna hali ya kuhamisha dhana.


Elimu ya Duksi inaenziwa na asilimia kubwa ya wanajamii. Elimu hii hutolewa takribani kila mahali katika eneo husika. Elimu hii huendeshwa na wanajamii wa umri wowote mahali popote kando na maalim au sheikh. Wanajamii wengi wameonyesha hali ya kuipelelea elimu ya Duksi zaidi kuliko shule ya msingi. Wanajamii huishughulikia sana elimu ya Duksi kuliko elimu ya shule za msingi. Hata wazazi wengine hutosheka tu na elimu ya Duksi. Watoto wao wanapohitimu katika Duksi hutosheka wasijishughulishe na elimu nyingine.

Ili watoto waweze kushika mafunzo haraka maalim huajiriwa kuendelea kuwafunza watoto wakati wa jioni na ikibidi hata usiku.

Kutokana na hadhi na nafasi ambayo elimu hii hupewa katika jamii, mafunzo huendeshwa wakati wowote bila kikomo. Vituo maalum ambavyo vimejengwa (jengo la kudumu) kwa gharama kubwa ili mafunzo hayo yaendeshwe kutoka kwa hilo jengo. Mfano mwafaka ni jengo lililo katika shule ya Young Muslim. Darasa hilo la Duksi limewagharimu wafadhili shilingi nusu milioni.

Katika elimu ya Duksi hakuna kukosa kuhudhuria masomo. Baada ya kuelewa na kuweza kukariri Korani wanafunzi huhitimu kwa kufanyiwa sherehe nao maalim hupewa zawadi kubwa kama ng'ombe. Mafunzo haya yanaweza kutolewa kabla au baada ya kuhudhuria masomo ya shule ya msingi. Maalim huruhusiwa kuchanganya ndimi kwa sababu ya athari ya mji, maingiliano ya wanajamii na elimu ya kimagharibi. Ingawa maalim anaweza kutumia lugha ya kwanza na Kiswahili kwa kufafanua dhana, lakini habari za kidini zimeandikwa kwa lugha ya Kiarabu. Waandishi wachache wanajaribu kutafsiri Korani.

Mbinu anuwai hutumiwa na maalim katika kuyaendesha maelezo, utendaji, miradi, hadithi, maigizo, nyimbo, maswali-majibu, mazoezi, marudio na kukariri. Maalim hutumia ubao na chaki huku wanafunzi wanatumia *kijiti* na *loh* ambapo kila mmoja akiwa na vifaa vyake. Wanafunzi hawaruhusiwi kutumia kalamu au kibao watu wawili (kila mtoto ana *loh*) kama ilivyoonyeshwa hapo chini:



Wanafunzi wakiwa wameshika loh mikononi

Wanafunzi wamedhihirisha uzoovu wa kusikiliza na kutenda kulingana na maagizo au masharti. Wanafunzi huwa wamezoeshwa kushirikishwa katika kila hatua ya ujifunzaji.

Mafunzo hayo yote hutolewa kwa mpangilio maalumu kulingana na silabasi na mtaala. Mafunzo hutolewa hatua kwa hatua kutegemea jinsi wanafunzi wanavyoelewa na kushika wanayofunzwa. Stadi zote nne hutiliwa mkazo kwa makini. Mwanzo, maalim hutanguliza maelezo huku wanafunzi wamesikiliza kisha akayarudia wakiyasema wanayoyasikia kwa sauti kubwa mara nyingi. Hatimaye, wanafunzi huyarudia wakashinda wakikariri. Mwishowe hupewa nafasi ya kusoma mmoja mmoja. Wanapoonyesha kuwa wamejua, hupiga hatua wakaanza kuandika.

Kando na Korani, wanafunzi hufunzwa maadili. Tabia nzuri na nidhamu husisitizwa. Wanafunzi ambao wanashindwa kushika na kufuata wanayofunzwa hupigwa vibaya na maalim. Wanafunzi hulazimishwa kurudia mafunzo ya Duksi. Hali hii ya kulazimishwa kuyarudia mafunzo ya Duksi hutisha watoto kiasi cha kuwafanya wajikakamue mpaka wafuzu. Hata wakichapwa, huvumilia wasitamani kutoroka.

Wanaohitimu, wanaweza kuwa maalim hata wakiwa na umri mdogo. Kwa hivyo vijana wengi hupenda sana elimu hiyo kwani kuna uhakika wa kupata kazi muradi mtu amefuzu ipasavyo. Wanajamii wengi huipuzilia mbali elimu ya kimagharibi. Inaaminiwa kuwa elimu ya Duksi ilitokana na Mwenyezi Mungu aliyemdokezea Mtume Mohammed kwa

njia ya maono. Hivyo basi wanaamini ni ya kweli na haki tupu.

Wanajamii wengi wanashikilia kuwa mafunzo hayo huwaandaa watu kwa maisha ya leo na hatima kule ahera. Imekusudia kuwafunza watu pia juu ya siku ya mwisho (siku ya kiama huko ahera). Inachukuliwa kuwa Kiarabu ndiyo lugha ambayo inatumika huko peponi.

Wanafunzi hudokezewa vile vile juu ya mila na desturi zao ili wasije wakawa waacha mila kwani wanajamii waliamini kuwa *mwacha mila ni mtumwa*. Wanajamii hao wanaamini kuwa mtoto mdogo akifunzwa juu ya Korani ni vizuri kwani huwa hajajifunza mabaya wala maovu yoyote. Vile vile umri mdogo huaminika kuwa na uwezo mkubwa wa kushika mambo mengi. Kuna madai kuwa mtoto mwenye umri wa miaka kati ya tatu na tano (3-5), akifunzwa jambo hawezi kusahau.

Katika jamii husika shule za bweni hazithaminiwi kwa sababu wazazi wanahofia watoto kutengwa na walimu wa kidini licha ya familia. Pia kuna wasiwasi kuwa athari ya nje inaweza kuwafanya watoto wasahau dini yao. Kwa hivyo wanajamii wengi wanapendelea shule za kuhamahama ambapo walimu huwafunza wanafunzi elimu zote mbili, ya kidini na ya kimagharibi. Haya yote yametokana na fasiri mbovu ya elimu ya kimagharibi.

Kwa jumla athari ya elimu ya Duksi ambayo imedhihirika ni kuwa kupitia kwa mbinu za kufunza, ni kuwa wanaofuzu katika elimu ya Duksi, huweza kupata maandalizi na matayarisho bora kabla ya kujiunga na shule za msingi. Walimu wa shule za msingi na malezi wamekiri kuwa elimu ya Duksi huwawezesha wanafunzi kuupata msingi thabiti wanapowekewa. Wanashikilia kuwa kiwango na uwezo wa wanafunzi wanaohitimu katika Duksi kilikuwa juu zaidi walipolinganishwa na wale ambao walitoka tu nyumbani na kuingia shuleni. Wanafunzi hao huwa tayari wanaelewa mambo ya ujifunzaji kama jinsi ya kushika kalamu, kuandika, kutamka kando na kutangamana na wenzao darasani. Wao huongoza kwa nidhamu na hata katika mitihani.

Kwa upande wa kujifunza na kujitegemea, wanafunzi waliohitimu kutoka chuo huwa safi na hata huweza kulinda vitu vyao kama vitabu na kalamu kwa sababu huwa tayari wameshafunzwa katika 'vyuo vya Duksi'. Katika darasa la Duksi hakuna kupoteza wakati. Kila muda huwa umetengewa kwa kazi maalum (Kwa mfano asubuhi ni kusoma, mchana kukariri na jioni kuandika). Katika kukariri kuna hatua tatu:

- Kujifunza matamshi ili maneno yatamkwe ipasavyo
- Kukumbuka ili yapokezwe kwa kuwaelezea wengine
- Kuelewa na kushika ili waweze kunukuu na kukariri aya katika Korani wanaposwali.

Elimu ya Duksi imekusudiwa kumtayarisha mtoto/mtu kwa maisha yake hapa duniani na baadaye huko ahera. Mafunzo haya ya kidini huchukuliwa kuwa ya kimsingi maishani.

Kuna asilimia kubwa ya wanajamii wanaoiamini na kuithamini kiasi cha kusema kuwa;

*“Dini ni maisha kwani bila dini hakuna maisha”.*

### 5.1.3 Mapendekezo

Imebainika kutokana na utafiti ambao umefanywa kuwa elimu ya Duksi imekuwepo na itaendelea kuwepo kwa sababu ya umuhimu wake katika jamii husika. Hivyo basi uchunguzi zaidi juu ya elimu hii, unaweza kufanywa ili kuangazia kwa kina hali halisi.

Ni muhimu kutanabahi kuwa utafiti huu ulishughulikia elimu ya kidini ya kimsingi ilhali kuna mafunzo ya juu katika viwango vingine kama madrassa, shule za upili, vyuo vya kati na hata vyuo vikuu.

Vile vile maoni mbalimbali juu ya jinsi ya kuimarisha na kuboresha ufunzaji na ujifunzaji wa sarufi ya lugha ya Kiswahili yalidhihirika. Maoni ya baadhi ya walimu ni kuwa ikiwezekana vipindi vya lugha ya Kiswahili viongezwe vitoshane na vya Kiingereza. Wanashikilia kuwa Kiswahili kama lugha zingine ina vipengele mbalimbali vinavyopaswa kushughulikiwa. Muda mwingi unahitajika ili maandalizi tosha yafanywe kwa stadi zote nne (4) za lugha (kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika).

Takribani wahusika wote ambao walishirikishwa kwa mahojiano walipendekeza kuwa maafisa wanaotoa huduma wanafaa kujibidiisha kutumia lugha sanifu ndani na hata nje

ya afisi. Watu wengi wakitumia lugha ya Kiswahili wanafunzi wanaweza kuiga na kufuata nyayo, hususan wazazi. Badala ya kutumia Kiingereza nyumbani, wajaribu kuwa vielelezo bora kwa kutumia Kiswahili sanifu nyumbani watoto wakiwaona na kuwasikia.

Ikiwezekana kila shule itenge kando siku ya kutumia Kiswahili. Kutoka asubuhi mpaka jioni shughuli zote ziweze kuendeshwa kwa lugha ya Kiswahili huku walimu wakiwa vielelezo. Walimu wajitahidi kutoa hotuba zao katika mihadhara katika lugha ya Kiswahili. Walimu wanaweza kuwashirikisha wanafunzi katika maongezi ya mara kwa mara. Mijadala na mashindano kati ya madarasa yanaweza kufanywa na washindi kutunukiwa zawadi au kupewa uhuru wa kuzuru mahali pa usomi kama maktaba, nje ya shule. Shuleni, kazi na mazoezi mengi yanaweza kuwasaidia katika kusoma na kukumbuka.

Ujenzi na utunzi wa maktaba ni jambo linaloweza kuwasaidia wanafunzi kujiimarisha kibinafsi katika usomi wao. Waandishi wa vitabu wanahimizwa kuandika vitabu vingi na vinavyoeleweka kwa urahisi kwa walimu pamoja na wanafunzi.

Wanafunzi wanapaswa kuongozwa wakati wa kusoma kusudi wapate kuzielewa dhana badala ya kuzikariri kauli tu. Matumizi ya nyenzo yanaweza kuchangia pakubwa kwani wanafunzi wanaweza kuona au kushika vitu halisi na hivyo basi kuweza kushika mambo yanayofunzwa kwa wepesi. Walimu wanaweza kuwahusisha wanafunzi katika kukusanya

na kuhifadhi nyenzo kando na kuandaa pembe ya kujifunzia darasani. Ni vizuri kuyatumia mazingira ya karibu.

Matumizi ya vifaa halisi darasani yanaleta uhai darasani. Wanafunzi huchangamkia kuona na hata kushika vitu halisi. Warsha za mara kwa mara zikiandaliwa zinaweza kuwafaa wengi. Walimu wanaweza kupata fursa ya kujikumbusha na hata kujifunza mambo yaliyo katika silabasi na mitaala. Vile vile masuala ibuka huenda yakaangaziwa barabara.

Ni bora kama wanajamii watazidi kujielimisha juu ya nafasi na dhima ya lugha ya Kiswahili. Wakielewa umuhimu wa lugha hiyo, wanaweza kuipa kipaumbele katika shughuli zao. Kiswahili ni lugha ya kimataifa inayobeba tamaduni changamano za Waafrika. Ni lugha iliyo na uwezo wa kuwatambulisha watu mbalimbali kando na kuwaunganisha. Mfano bora ni kuwa mjini Garissa vijana wanaopewa kitambulisho cha nchi (stakabadhi rasmi), ni wale tu wenye uwezo wa kuongea vizuri lugha ya Kiswahili. Anayeshindwa kwa hicho kigezo hapewi kitambulisho na hata hushukiwa kuwa mkimbizi.

Ikiwezekana kama namna walimu wa Duksi hutoa huduma kwa wanafunzi mpaka wakahitimu, ni vizuri walimu kushikilia darasa kwa muda fulani bila kubadilishwa. Wanafunzi huweza kuzoea mwalimu muda wa kujifunza na wakati unapopita hata

wanafunzi huanza kumwamini kiasi cha kuwa huru kuingiliana naye.

Kwa mujibu wa sheria za Wizara ya Elimu, wanafunzi hawatajikani kupigwa viboko. Iwapo ni lazima waadhibiwe adhabu nyingine itumike. Matumizi ya kiboko yanafaa kukomeshwa la sivyo lazima mzazi ashuhudie kiboko kinapotumika. Elimu jumuiifu inastahili kutiliwa mkazo ili watoto waweze kuandaliwa na kutayarishwa mapema kwa elimu ya baadaye. Elimu ya kidini ikitangulia inaaminiwa kuwa ina uwezo wa kupanua akili ya mwanafunzi. Mtoto pia anaweza kupata nafasi ya kujifunza haraka tena mapema. Tayari kuna shule vielelezo hasa mjini. Wazazi waliochanuka ndio wanaopendekeza elimu zote mbili [2]. Tukiangalia nchini, elimu hiyo imeanza kutolewa kwingi. Baadhi ya vituo vielelezo ni kama chuo cha Abuhurera huko pwani, Nairobi Muslim South C, Young Muslim na Alforuk Garissa.

Jinsi ambavyo mitaala na silabasi ya Duksi hufuatwa, Wizara ya Elimu inafaa kufuatiliza ufunzaji na ujifunzaji. Wanafunzi wanafaa kujulishwa umuhimu wa kupata elimu ya kiwango cha juu. Wanapaswa kuelewa kuwa Duksi ni elimu inayowapa msingi tu, kisha madrassa, kiwango cha upili, Vyuo vya kati (kama vya Pumwani na Thika) na hatimaye vyuo vikuu kama Chuo cha Kisauni, mkoani Pwani.

Walimu wanakumbushwa wasiendelee na mazoea ya kuhalalisha makosa kwa kuwaambia wanafunzi kuwa wanapokosa kuupata msamiati mwafaka watumie tu

Kiarabu au Kisomali kwani lazima kazi itasahihishwa. Wanafunzi wanapaswa kuhimizwa na kushauriwa juu ya kujizoeshwa kutumia Kiswahili sanifu kila wakati. Hivyo basi wajiepushe na matumizi ya Sheng’.

Baada ya mafunzo ya Duksi, wanafunzi hujiunga na wanajamii wengine katika kutekeleza waliyojifunza hususan msikitini wanaposwali. Waumini wote hupiga magoti wakaomba sawia mbele zake Mwenyezi Mungu. Yaani mafunzo ya elimu ya Duksi hayana mipaka. Huendelea kutolewa popote pale hata mbele ya jengo na yeyote yule muradi awe anajua Korani barabara. Wanafunzi huyaraukia asubuhi, mchana na hata usiku. Marudio haya ya mara kwa mara husaidia wanafunzi kuelewa na kuyashika wanayofanya.

Maalim hutilia maanani ratiba ya kazi. Wanafunzi hupelekwa hatua kwa hatua kusudi wapate kuelewa jinsi ya kukariri aya katika Korani ( wakati wa kuswali). Shughuli ya kukariri hufanywa kwa sauti kubwa ili watoto wayapate matamshi sahihi. Kupitia ukariri huo, inaaminika kuwa akili za watoto huweza kupanuka. Kusoma pia hufanywa kwa sauti. Mwishowe, watoto hufunzwa jinsi ya kuandika kwa hati nzuri inayosomeka.

Kupitia kwa shughuli na kazi za kijinadhifisha, kusafisha darasa, kutengeneza wino wa kalamu, wanafunzi huweza kupata ujasiri na hata uwezo wa kuunganisha sauti, maneno na sentensi. Hivyo basi hupewa maandalizi na majaribio ya kushika kalamu na namna ya

kuandika. Kama tulivyoona wakati maalum hutengwa kwa somo la kuandika. Katika shule ya Young Muslim wanafunzi huandika jioni (siku kama ya Jumamosi na Jumapili). Siku zilizosalia hutumiwa kwa masomo na kazi tofauti tofauti kama ilivyobainishwa mapema katika sura ya pili na ya tatu.

Imebainika kuwa ratiba ya kazi inasaidia katika kukamilisha jukumu pana. Mpangilio wa kazi huwa unaokoa muda. Huhakikisha kuwa hakuna muda ambao unatumia vibaya. Kuratibisha kazi yake maalim, humwezesha kutumia muda wake vizuri. Mpangilio wa kazi humfanya maalim kutekeleza kazi yake kwa utaratibu, hatua kwa hatua kwani anapopanga, huwa anajitayarisha mapema. Mfano bora ni maandalizi ya kutumia ubao. Ubao ukiwa kifaa cha karibu na muhimu mno mwalimu akijua kuutumia huwa kielelezo darasani. Wanafunzi wanaiga mpangilio mzuri wa kazi na hata hati (mwandiko unaosomeka na herufi ziwe kubwa lakini za kutoshana).

Mbinu ya maigizo hutumiwa wakati mwingine ambapo wanafunzi huelezwa cha kufanya kisha wakafanya mazoezi ya kutosha na baadaye wakawasilisha habari hizo. Maalim wakati mwingine hutumia mbinu ya nyimbo. Maalim Huwafunza wanafunzi nyimbo kisha wakaimba kwa pamoja. Nyimbo hizo huchambuliwa baadaye ili ujumbe maalum upambanuliwe. Nyimbo hizo zinaitwa kasida. Kubadilishabadilisha mbinu za kufunzia hudumisha uhai darasani. Wanafunzi hawawezi kuchoka wala kusinzia.

Rekodi ya kazi ambayo imeshughulikiwa husaidia katika maandalizi ya wakati wao. Vile vile huongoza mwalimu wakati wa kutathmini wanafunzi. Matumizi ya nyenzo husaidia kurahisisha dhana ambayo ni ngumu. Imedhihirika kuwa maalim anapotumia vifaa halisi kama mafanani kuhadithi na matembezi (ziara za kiusomi) msikitini dhana nyingi huweza kueleweka kwa urahisi. Badala ya kusema maneno mengi, matendo na vitu halisi vinatosha. Wanafunzi wanapooona na kufanya wanaweza kushika na kukariri Korani kwa urahisi. Kuwahusisha huwafanya wanafunzi kuelewa habari haraka.

Aghalabu nyenzo humpa mwanafunzi nafasi ya kutangamana na kufurahia mazingira yanayomzunguka. Nyenzo hukuza stadi ya mwanafunzi ya kusikiliza kwani huamsha ari na moyo wa kutaka kusoma kando na kunoa mtazamo wake.

Mwalimu anapofunza lugha afanye hivyo kwa kuitumia lugha iyo hiyo. Yeye awe kielelezo bora hasa kwa kutumia lugha sanifu na matamshi sahihi. Wanafunzi wanastahili kuelekezwa kwa njia ambayo haitamvunja moyo bali ushauri ufanywe kwa uangalifu. Vivyo hivyo kwa utaratibu wanafunzi wapewe majukumu ya kutekeleza ili waelewe namna ya kuwajibika.

Pasipo na ziara za elimu, mafanani wanaweza kualikwa ili waelezee mambo kama masuala ibuka, utamaduni na historia. Fasiri ya silabasi na mitaala inafaa kufanywa chini ya uongozi wa watu wenye uwezo na tajriba. Wanafunzi wanafaa kuhimizwa kusoma

kwa mapana vitabu, magazeti, majarida na miswada.

Matumizi ya vyombo vya mawasiliano kama runinga, video na redio, kompyuta vinaweza kuchangia pakubwa. Tathmini na marudio ya mara kwa mara ambapo wanafunzi wanaonyeshwa uzito na upungufu kisha wanasaidiwa. Hali hii inaweza kuwafanya wanafunzi kutia bidii zaidi. Vile vile moyo wa mashindano unaweza kuimarishwa.

## MAREJELEO

- Ahmed, A. 2002: *Making Sense & Muslim History & Society*: Routledge Taylor & Francis Group, London.
- Ahmed, B. I. 1993: *Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya*: ( Kiswahili-Kiarabu-Kiingereza) Dar-es salaam University Press.
- Abdallah, K. 1977: *The Liberation of the Swahili: From European Appropriation*. East African Literature Bureau, Kenya Nairobi.
- Ashton, E.O. 1944: *Swahili Grammar* : Longman: London.
- Besha, R.M. 1991: *The Acquisition of Swahili by Adult Maasai Speakers Possible Areas of Conflict in*: Pottland, F. and Omondi, L. (wahariri). Processings of the third Nilo-Saharan Linguistics colloquium Kisumu, Kenya August 1986. Helmut Verlag Hansburg.
- Corder, S.P. 1981: *Error Analysis and Interlanguage*. Oxford University Press, London.
- \_\_\_\_\_ 1983: *A Role for Mother Tongue in Gass, S. and Selinker. (wahariri). Language in Learning* .Rowley, Newbury House.
- Dulay, H. C. &
- Burt, M. 1972: *Groofing; An indicator of Children' Second Language Learning*. Juzuu la 22.
- \_\_\_\_\_ 1974: *Errors and Strategies in Child Second Language Learning*. TESOL Quarterly Juzuu la 8.
- Ellis, R. 1985: *Understanding Second Language Acquisition*. University Press, Oxford.U.K.
- Ellis, R. na  
Barkhuizen, S. 2005: *Analysing Learner Language*. Oxford University Press, Great Claredon Street, Oxford, U.K. Linguistics.
- Fisiak, J.(Mhariri).1981: *Contrastive Linguistics and the Teacher*, Pergamon Press, Oxford. Ann Arbor.
- Fries, C.C . 1945: *Teaching and Learning English as a Second*

- Language*. University of Michigan Press, Oxford.
- Goodlunen, H. 1991: *Language Acquisition and Linguistic Introduction*. Blackwell Publishers Limited; U.K.
- Kebeya, H. 1997: *Investigating Linguistic Accommodation Between Two Luhya Dialects: Lulogoli and Lwitakho*. M.A Thesis. Kenyatta University. Kenya.
- Kenneth, W.H. 1991: *Faces of Islam in African Literature*: Heinemann. Educational Books: U.S.A.
- Kramer, L. M. 1975: *Teaching the Life Science*, Macmillan Education Limited: Great Britain: London.
- Lado, R. 1957: *Linguistics Across Cultures*. The University of Michigan Press. Michigan, U.S.A.
- Macaro, E. 2005: *Teaching and Learning of a Second Language*. Great Britain: London.
- Mathooko, P. 2004: *Towards An Intergrated Perspective of Linguistic Accommodation; Acase study of Kikamba & Kitharaka* Ph.D Thesis. Nairobi, Kenyatta University.
- Mbaabu, I. 1985: *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Kenya Literature Bureau: Nairobi.
- \_\_\_\_\_ 1996: *Language Policy in East Africa: A Dependancy Theory Perspective*. Educational Research and Publications: Nairobi.
- Milroy, L. 1987: *Observing & Analysing Natural Language*. Oxford, Blackwell, Basil. U.K.
- Mudhune, E.S. 1994: *A Contrastive Analysis Approach to the Learning of Swahili Morphosyntax by Luo Learners*. M.A Thesis, Nairobi: Kenyatta University.
- Musau, P.M. 1993: *Aspects of Interphonology: The Study of Kenyan Learners Swahili*. Bayreuth African Study, Bayreuth: Germany.
- Mwandoe, B.M. 2002: *The Teaching and Learning of English Poetry in Secondary School in Kenya*. M.Ed. Thesis, Nairobi: Kenyatta University.

- Nehemiah, M.N.2003: *Introduction to the Study of Religion*: Zapf Chancery Research Consultant & Publishers, Nairobi.
- Newmeyer, J.(Mh).1985: *2<sup>nd</sup> Language Acquisition Linguistics* .The Cambridge Survey. Cambridge University Press: London.
- Njogu, K. na Chimerah, R. 1999: *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Nkwera, F.M.V. 1978: *Sarufi na Fasihi, Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Polome, E.C. 1967: *Swahili Language Handbook*. Washington D.C, U.S.A.
- Scotton, C.M. 1967: *A Llook at Swahili of Two Groups of Upcountry Speakers of Swahili*, Journal of Institute of Swahili Research. JZ la 39/1.
- Selinke, L. 1992: *Rediscovering Interlanguage*.Longman, London.
- \*Sheikh, A.** *Qurani Tukufu; Taasis ya Zeyed bin Sultan, Al-Nahayan, Tarjama ya MUNTAKHAB.*
- Spolsky, B. 1989: *Conditions for Second Language Learning*, Oxford University Press. Walton Street: Oxford.
- Srindar, S.N. 1981: *Contrastive Analysis, Error Analysis and Interlanguage; Three Phases of One Goal katika Fisiak, J (mhariri) Contrastive Linguistics and the Language Teacher*. Pregamon Press, Oxford.
- \*Tayebjee, M.A.** *Maka ya Fasiri ya Korani Takatifu: "KUTUB KHANA ISHAATUL ISLAM INDIA"*.
- Trudgill, P. 1972: *Sociolinguistics*. Penguin Group: London.
- Wanyoike, E.N. 1978: *Vikwazo katika Mafunzo ya Kiswahili Nchini Kenya: Lugha Journal for Language Teachers Kenya*, Nairobi JZ la 5,35-42.
- Whiteley, W.H. 1974: *The Classification and Distribution of Kenya's African Languages*. Oxford University Press: Nairobi.
- Weinreich, U. 1953: *Language in Contact*: Publications of the Linguistic Circle of New York. U.S.A.

## KIAMBATISHO 1

### Hojaji ya Walimu na Maafisa wa Elimu

Jina:-----

Jinsia.....

Umri:

Tia alama ya mkwajo

Miaka kati ya (a) 5 –10

(b) 10 – 15

(c) 20 –25

(d) 30 – 35

(e) Zaidi ya miaka 40

Habari kuhusu elimu ya Duksi:

(a) Nimewahi kudhuria mafunzo ya Duksi

(b) Sijawahi kuhudhuria elimu ya Duksi

(c) Nimeshuhudia watu wakisoma Duksi

Kazi:.....

Mahali unapoishi.....

**Maswali yafuatayo yalizingatiwa.**

1. Neno *Duksi* lina maana gani? -----  
-----

2.(a) Je, elimu ya *Duksi* inahusu nini hasa?-----  
-----

b) Linganisha vipengele vifuatavyo katika taratibu mbili (2) za elimu (lugha ya Kiswahili na ya Kiarabu).

(i)Abjadi-----

(ii) Mtindo wa kuandika -----

(iii)Mpangilio wa maneno katika sentensi -----

(iv) Msamiati-----

3. Tofautisha kati ya elimu ya *Duksi* na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili? Zingatia

mbinu za kufunzia-----  
-----  
-----

4. Unafikiri mbinu zipi zinaweza kutumiwa ili ziimarisha na kuboresha ufunzaji na

ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili?-----  
-----  
-----  
-----

## KIAMBATISHO 2

### Hojaji ya wanafunzi

1. Andika alfabeti-konsonanti na vokali za lugha ya Kiarabu.( herufi zinazopatikana katika darasa la mafunzo ya elimu ya Duksi-----

-----  
-----

a) Andika maneno sita yanayotumiwa kwa kutaja sehemu za mwili. -----

-----  
-----  
-----  
-----

b) Tunga sentensi tatu ukitumia maneno uliyoyataja hapo juu -----

-----  
-----  
-----

c) Je, kuna tofauti gani kati ya mafunzo ya Duksi na mafunzo ya Kiswahili? Toa

mifano miwili-----

-----  
-----

-----

### KIAMBATISHO 3

#### Maswali ya Mahojiano

**Mahojiano kati ya mtafiti na walimu, wazazi na maafisa wa elimu yaliongozwa na maswali yafuatayo:**

1. Duksi ni nini? Eleza kwa ufupi. -----  
-----

2. Unafikiria, ufunzaji wa lugha ya Kiswahili shuleni una umuhimu wowote katika hili eneo? Eleza kwa ufupi . -----  
-----

3. Kwa maoni yako, unafikiri Elimu ya Duksi inaathiri vipi ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili-----  
-----  
-----

4. Pendekeza baadhi ya mikakati inayoweza kutumiwa ili kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili? Taja tatu.-----  
-----  
-----  
-----

## KIAMBATISHO 4

### Zoezi la Imla la Wanafunzi

A. Yaandike maneno yafuatayo kwa daftari

1. Maana
2. Kwapa
3. Paja
4. Pua
5. Pole
6. Insha
7. Pata
8. Pata
9. Pete
10. Poa

B. Yatungie sentensi maneno yaliyotajwa hapo juu



Wanafunzi wanafunzwa na maalim nyumbani